**17 APRILI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Nane – Tarehe 17 Aprili, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR - KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na maswali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Genzabuke.

Na. 93

**Hitaji la Jengo Jipya la Utawala – Hospitali ya Wilaya Kasulu**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Utawala Hospitali ya Wilaya Kasulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Kasulu ni moja ya hospitali 67 zilizoanza kujengwa katika awamu ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hospitali hiyo ilipokea jumla ya shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya huduma za wagonjwa wa nje, maabara, jengo la mionzi, stoo ya dawa, wodi ya wazazi, jengo la kufulia na jengo la utawala ambalo limekamilika na linatumika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Hospitali ya Mji wa Kasulu ilijengwa miaka 60 iliyopita na hospitali hiyo majengo yake yamechakaa na nyumba za watumishi pia zimechakaa. Je, ni lini Serikali itawajengea watumishi nyumba mpya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Hospitali ya Mji wa Kasulu ina mtaalam mmoja wa mionzi na mtaalam huyo hufanya kazi mwaka mzima bila kupumzika. Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kada mbalimbali wakiwemo wataalam wa mionzi katika Hospitali hiyo ya Kasulu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshafanya tathmini ya hospitali kongwe zote kote nchini, ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Tayari mwezi Septemba, 2023 Serikali ilishapeleka shilingi milioni 900 kwa ajili ya ukarabati na kazi za ukarabati wa hospitali zinaendelea. Mpango huu ni endelevu tutahakikisha pia tunapeleka fedha nyingine kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa hospitali nzima,

pamoja na kukarabati na kujenga nyumba za watumishi katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusiana na wataalam wa mionzi, ni kweli tuna upungufu wa wataalam wa mionzi katika hospitali zetu, lakini tayari Serikali imeshafanya jitihada ya kuwasomesha kozi maalum fupi wataalam wa mionzi na *Ultrasound* kwa ajili ya kuwapeleka kwenye hospitali hizo ili kupunguza upungufu wa watumishi hao. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutatoa kipaumbele pia katika Hospitali ya Mji wa Kasulu pale watumishi hawa watakapokuwa wametoka vyuoni watakapokuwa wameajiriwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Makorongo kilifunguliwa na Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kikiwa na upungufu wa majengo manne, lakini mpaka leo majengo hayo hayajakamilika. Naomba kujua *commitment* ya Serikali ya kuhakikisha majengo haya yanakamilika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Monni kwamba Serikali inatambua kwamba kituo hicho cha afya kina upungufu wa majengo muhimu ili kiweze kutoa huduma muhimu zinazotakiwa kwa ngazi ya kituo cha afya. Tayari Serikali imeshaainisha vituo vyetu vyote vyenye upungufu wa miundombinu muhimu na fedha zinatafutwa kwa ajili ya kwenda kujenga miundombinu hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru Serikali imejenga vituo vya afya viwili Kayenze

pamoja na Buswelo, lakini vituo vyote vile miundombinu yake haijakamilika na vingine pia unakuta havina wodi kwa ajili ya kulaza wagonjwa. Ni lini vituo hivi vitakamilika ili viweze kutoa huduma iliyokusudiwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, Kituo cha Afya cha Buswelo na hicho kingine ambacho amekitaja Mheshimiwa Mbunge, nilishafanya ziara pale. Tulianza na ujenzi wa awamu ya kwanza wa majengo ya vituo vya afya kote nchini. Nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tutakwenda awamu ya pili ya kukamilisha miundombinu inayopungua na tutaweka kipaumbele kwenye vituo hivyo alivyotaja Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo la *emergency* katika Kituo chetu cha Malawi Vituka pamoja na chumba cha kuhifadhia maiti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana hicho kituo cha afya kuwa na jengo la *emergency* kwa maana ya *Emergency Medical Department* kwa sababu ya idadi ya wananchi wanaotibiwa pale. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunalichukua hilo ili ngazi ya Wizara tukalifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na chumba cha kuhifadhia maiti, kwa kweli Manispaa ya Temeke ina uwezo wa kujenga chumba kile, kwani ni kidogo na hakihitaji gharama kubwa. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,

TAMISEMI kumwelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke kuhakikisha anaweka kipaumbele kwenye bajeti zake ili chumba hicho kiweze kujengwa na kianze kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yake.

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba.

Na. 94

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Kisorya, Kasuguti na Kasahunga**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya Kisorya, Kasuguti na Kasahunga – Mwibara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 na 2021/2022 Kituo cha Afya Kisorya kilipokea jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji, maabara, wodi ya akina mama, nyumba ya mtumishi, jengo la kuhifadhia maiti na jengo la huduma za kifua kikuu. Majengo yote yamekamilika na yanatumika isipokuwa jengo la kuhifadhia maiti ambalo taratibu za kupata jokofu zinaendelea kupitia Bohari Kuu ya Dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022, Kituo cha Afya Kasuguti kilipokea shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji, ukamilishaji wa jengo la mama na mtoto na nyumba ya mtumishi. Aidha, majengo yote yamekamilika na yanatumika isipokua jengo la upasuaji ambalo lilikuwa halina vifaa tiba. Hata hivyo, kituo kimepokea shilingi milioni 200 mwaka 2023/2024 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba na taratibu zinaendelea kupitia Bohari Kuu ya Dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 na 2021/2022 Kituo cha Afya Kasahunga kilipokea jumla ya shilingi milioni 510 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la maabara, wodi ya akina mama, wodi ya watoto, nyumba ya mtumishi, jengo la kufulia na jengo la kuhifadhia maiti. Majengo yote yamekamilika na yanatumika isipokuwa jengo la kuhifadhia maiti ambapo taratibu za kupata jokofu la kuhifadhia maiti zinaendelea kupita Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa hivi Vituo vya Afya vya Kasuguti na Kasahunga vimejengwa kwa muda mrefu, sasa ni miaka minne, inaenda miaka mitano: Ni lini majokofu kwa ajili ya mochwari yatapatikana kwenye vituo hivyo kwa sababu sasa imekuwa kama kero?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kituo cha Afya Hunyari kimejengwa lakini hakina jengo la upasuaji. Ni lini Serikali itajenga jengo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli majengo haya yamejengwa na yamekamilishwa. Hatua ambayo ilikuwa inasubiriwa ilikuwa ni kupata fedha kwa ajili ya kuanza kutoa huduma kwa majengo yale ya kuhifadhia maiti. Tayari Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alishapeleka fedha katika halmashauri hii na tayari fedha zimepelekwa katika Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* kwa ajili ya kununua majokofu hayo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha majokofu yanapatikana mapema ili wananchi waanze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na jengo la upasuaji, safari ni hatua. Tumejenga majengo ya awali, huduma za awali zimeanza kutolewa tunakwenda kujenga pia majengo ya upasuaji katika kituo hicho alichokitaja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Mheshimiwa Naibu Waziri, wananchi wa Kata ya Kabwe wamechoka na ahadi, tunataka kusikia kauli moja leo. Ni lini mnapeleka fedha za umaliziaji wa Kituo cha Afya Kabwe ili kianze kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Nkasi Kaskazini pamoja na Kata ya Kabwe kwamba Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inatambua sana na ndiyo maana ilishapeleka shilingi milioni 250 na majengo yamejengwa. Tunatafuta fedha, wawe na imani kwamba fedha itapelekwa, majengo yatajengwa na watapata huduma kama ambavyo tulianza kupeleka fedha nyingine. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Michael.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kwala unaendelea na ujenzi wa kongani ya viwanda na tumeanza ujenzi wa kituo cha afya ambacho hakijakamilika. Kwa umuhimu wa Mji wa Kwala kwa sasa, ni lini Serikali itapeleka fedha ya kumalizia kile kituo cha afya ili kiweze kusaidia wananchi watakaokwenda kupata huduma katika maeneo yale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mji wa Kwala unakwenda kuendelezwa sana na unahitaji kuwa na huduma za afya za uhakika. Nampongeza Mheshimiwa Mwakamo kwa namna ambavyo amefuatilia ujenzi na ukamilishwaji wa hicho kituo cha afya. Nimhakikishie tu kwamba tutahakikisha fedha ambazo zinatakiwa kukamilisha kituo hicho cha afya zinapelekwa. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi kumwelekeza mkurugenzi kufanya tathmini ya mahitaji ya hiyo fedha na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili Serikali iweze kufanya kazi yake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Dabaldi Wilayani Karatu kinahudumia wananchi wengi wakiwemo wananchi wa Wilaya jirani ya Ngorongoro, lakini kwa muda mrefu sasa jengo la mama na mtoto halijakamilika. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu yapo majengo ambayo yalipelekewa fedha...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umeshachukua hoja, inatosha. Mheshimiwa Furaha.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Misasi ni kituo kikubwa kinachohudumia wananchi wengi, lakini mpaka sasa hakina chumba cha kuhifadhia maiti na pia hakina wodi ya wanaume. Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hizi ili wananchi wa Misasi waweze kupata huduma? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishapeleka fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu, lakini tulishawaelekeza pia Wakurugenzi kutenga sehemu ya fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ambayo inapungua. Nitumie nafasi hii kumkumbusha mkurugenzi kutekeleza wajibu wake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Mushashu.

Na. 95

**Uhaba wa Walimu wa Hisabati na Sayansi Nchini**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaajiri Walimu wa kutosha wa somo la hisabati na sayansi ili kuliokoa Taifa letu kukosa Wanasayansi siku zijazo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari wa masomo ya sayansi kadiri ya upatikanaji wa fedha. Kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023 jumla ya walimu 18,016 wa shule za msingi na walimu wa sayansi wa shule za sekondari 10,917 waliajiriwa na kupangiwa katika halmashauri mbalimbali. Mchanganuo wa ajira za walimu wa sekondari wa hisabati na sayansi katika kipindi hicho ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020/2021 walimu wa sayansi na hisabati 3,000, mwaka 2021/2022 walimu 3,742 na mwaka 2022/2023 walimu 4,175. Serikali itaendelea kuajiri walimu wa masomo ya hisabati na sayansi na masomo mengine kadiri ya upatikanaji wa fedha na uwezo wa kulipa mishahara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mushashu.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Huu upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi na hisabati katika shule zetu unasababisha baadhi ya shule wasisome kabisa haya masomo au wasifundishwe kwa nadharia na vitendo kama inavyotakiwa na hii inasababisha watoto wanakosa *skills* wanazozihitaji. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kunusuru Taifa hili lisije likakosa wataalam wa sayansi na teknolojia wanaohitajika kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa ujumla Mkoa wa Kagera una upungufu mkubwa wa walimu 8,508 wa elimu ya msingi na 2,142 walimu wa shule za sekondari. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka walimu wa kutosha katika Mkoa wa Kagera katika shule za sekondari na za msingi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika,

Mheshimiwa Mbunge ana hoja ya msingi na Serikali inatambua upungufu na ndiyo maana Serikali imeanza na mkakati wa kufanya msawazo wa walimu ili kupunguza ukali wa upungufu. Pia Serikali imebuni mkakati wa matumizi ya TEHAMA kwa kutumia ufundishaji mubashara na mpaka muda huu, tayari kuna shule ambazo zimeanza kutumia teknolojia hii ikiwemo Kibaha Sekondari, Iyumbu Sekondari, na Dodoma Sekondari. Pia Serikali inatumia mkakati wa mafunzo kwa vitendo kazini kupata walimu ili waweze kwenda kupunguza upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali inaendelea kuajiri kwa kadiri fedha zinavyopatikana. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali inatambua na hasa kwa sababu amezungumzia walimu hawa wa sayansi na hisabati, Serikali itatumia mikakati kuhakikisha walimu hao wanapatikana waweze kuwahudumia wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia upungufu wa walimu katika Mkoa wa Kagera. Serikali inatambua upungufu huo na ndiyo maana Mei, 2023 Serikali iliajiri walimu 13,130 na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha Serikali itaajiri walimu wengine. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika mgao huo na shule za Mkoa wa Kagera zitapata mgao wa walimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana sana sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. Huo ndiyo uzuri wa wanasheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Mushashu, nitumie nafasi hii kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba Mheshimiwa Rais siku ya jana ametoa kibali cha kuajiri watumishi

wapya 46,000. Katika idadi hiyo, kibali cha ajira za walimu ni 12,000 na ajira za afya ni zaidi ya 10,000. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba katika kujipanga kwetu, kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI tutahakikisha kwamba upungufu wa walimu kwenye maeneo yetu unakwisha na hasa maeneo yale ambayo yana upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunafikiria kuwa na utaratibu mpya wa kuajiri kupitia kwenye mikoa yetu badala ya kuajiri *centrally.* Hili ni katika kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge, lakini tutashirikishana kadiri jambo hili linavyoendelea. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni jambo jema kuongeza walimu, lakini kuna walimu wanajitolea sasa hivi kwa takribani miaka tatu mpaka minne. Zinapokuja ajira, *they are not considered.* Sasa hii iwe kipaumbele kwa walimu wanaojitolea mwachukue wao kabla ya hawa wapya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Aloyce Kamamba.

Na. 96

**Kupandisha hadhi Shule za Sekondari – Buyungu**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapandisha hadhi Shule za Sekondari za Nyamtukuza, Muhange, Shuhudia, Kasanda na Gwanumpu kuwa za kidato cha tano na sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko ina jumla ya shule mbili za kitado cha tano na sita. Katika kuongeza shule za kidato cha tano na sita, shule za Nyamtukuza, Muhange, Shuhudia, Kasanda na Gwanumpu zimefanyiwa tathmini na hakuna shule hata moja iliyokidhi viwango kwa kuwa zote zina upungufu wa miundombinu. Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imepanga kupandisha hadhi shule hizi kwa kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2025/2026 na 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri wataweka vipaumbele katika kuhakikisha kuwa Shule za Sekondari Nyamtukuza, Muhange, Shuhudia, Kasanda na Gwanumpu zinaendelezwa na kupata hadhi ya kuwa kidato cha tano na sita. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ambayo yametolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 niliuliza swali kama hili na nilipata majibu haya, lakini ikumbukwe kwamba kuna halmashauri ambazo kipato chake au makusanyo yake ni kidogo na hivyo haziwezi kukidhi kujenga shule kwa fedha zake. Je, nini mkakati wa haraka na wa makusudi kuhakikisha kwamba Serikali inaisaidia halmashauri za wilaya ambazo uwezo wake ni mdogo ili ziweze kujenga shule hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Viongozi wangu wa Wilaya kuanzia Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya, Mwenezi na Katibu wa Wilaya wamehamasisha walimu na wananchi katika maeneo hayo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kufuatana nami ili twende tuzione shule na kuwatia moyo wananchi ambao wapo tayari kuwapokea walimu hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anapambania kweli maslahi ya Jimbo lake, lakini kuhusiana na suala la mapato madogo katika halmashauri za Wilaya na jinsi gani Serikali imejipanga kuzisaidia na kuziwezesha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ina mkakati wa kuwezesha halmashauri kuweza kuwa bunifu ili ziweze kubuni miradi endelevu ambayo itaziwezesha halmashauri kujimudu.

Aidha, Serikali itaendelea kusaidia ujenzi wa miundombinu kwa baadhi ya halmashauri hizi kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana Serikali itaona ni namna gani inaweza kuunga mkono jitihada za halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu mimi kuweza kufuatana naye kwenda kwenye ziara kuziona shule hizi, namkubalia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaambatana pamoja ili tukazione shule hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Bidya.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza ni lini Shule ya Sekondari Nguruka itapandishwa hadhi kuwa kidato cha tano na cha sita? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Uvinza aweze kwenda kufanya tathmini. Itumwe timu ikafanye tathmini ili kubaini kama shule hii inakidhi vigezo ili utaratibu uweze kufuatwa kwa kutuma maombi Wizara ya Elimu kwa Kamishna wa Elimu ili

watakapofanya taratibu zao waweze kuona kama shule hii inaweza kupandishwa hadhi kuwa kidato cha tano na cha sita. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Mwakasaka kwa niaba yake Mheshimiwa Rehema.

Na. 97

**Kuboresha Mfuko wa *TASAF***

**MHE. REHEMA J. MIGILLA K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, Serikali inafanya juhudi gani kuboresha Mfuko wa *TASAF* kwa wananchi wasiojiweza kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kutanua wigo wa maeneo ya utekelezaji wa mpango kutoka halmashauri 42 awamu ya kwanza hadi sasa kufikia halmashauri zote nchi nzima katika awamu ya tatu.

(ii) Uboreshaji wa taratibu za utambuzi wa walengwa ambapo katika awamu tatu za utekelezaji wa *TASAF* uliwezesha kutambuliwa kwa kaya milioni 1.2 sawa na asilimia 86 ya kaya katika

vijiji/mitaa/shehia zote nchini ambalo ni ongezeko kubwa la walengwa.

(iii) Aina na afua za miradi zimeboreshwa kwa kulenga kuwainua wananchi kiuchumi. Mathalani, awamu ya kwanza ililenga ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii, awamu ya pili iliendeleza ujenzi wa miundombinu pamoja na miradi ya kuongeza kipato kwa makundi maalum, na awamu ya tatu miradi imelenga mpango wa kunusuru kaya maskini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kufanya maboresho ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ili kuhakikisha manufaa makubwa yanaendelea kuwakwamua wananchi wasiojiweza kiuchumi ili kuondokana na umaskini uliokithiri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri na thabiti ya Serikali kuwasaidia watu wa kaya maskini, tunajua kabisa huu mradi tangu uanze walengwa wote wa *TASAF* bila kuangalia maeneo yao na mahitaji yao wanapata shilingi 20,000 kwa mwezi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha sasa hiki kiwango kinaongezeka zaidi toka shilingi 20,000 ili waweze kujikimu na mahitaji yao kulingana na kwamba hali ya uchumi kwa sasa hivi ni ngumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa watu ambao kipindi wanatambuliwa hawa watu wenye kaya maskini hawakuingizwa kwenye mpango. Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha kwamba wale wote ambao walirukwa kipindi cha utambuzi wanaingizwa kwenye mpango wa kusaidia kaya maskini? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa Serikali hamu yake kubwa au tamaa yake kubwa ni kuona kwamba malipo haya ya wanufaika yanakuwa ni makubwa sana, lakini kama mnavyojua, Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako mradi huu unafanyika kwa ushirikiano baina ya Serikali na wahisani na ziko fedha ambazo zinaingizwa ambazo ni asilimia zaidi ya 60 ambazo zinaletwa na wahisani katika maana ya kusaidia kutatua tatizo la umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge haya maboresho yote ambayo tumeyasema hapa ni sehemu ya kuona kwamba jinsi gani Mfuko huu unaendelea kutanuliwa au fedha zinaongezwa zaidi ili kuweza kufikia malengo makubwa ambayo Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako na wananchi wangetamani tufikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba Serikali imeendelea kufanya mazungumzo na wahisani katika kuona fedha hizi zinaongezeka ili ikiwezekana sasa tutoke kwenye shilingi 20,000 twende hata ikiwezekana shilingi 50,000 au hata shilingi 100,000 kama uwezo wa mfuko utahimili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, malalamiko ya utambuzi, nataka kulikumbusha Bunge lako kwamba, katika moja ya majibu ya msingi au maelezo ya kuhusiana na utaratibu wa utambuzi ndani ya Mfuko wa *TASAF* tulieleza kwamba Mfuko wa *TASAF* katika hatua yake ya kwanza mnapokwenda kutambua Mkutano Mkuu wa Kijiji, Shehia au Mtaa ndiyo ambao unatumika kutambua wahusika na baada ya utambuzi kuwa umefanyika, Kamati itakaa kutambua kama waliotajwa ni wahusika kweli au wengine wamechomekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza zoezi hilo, hatua inayofuatia ni kubandika majina ya wale watu wote ambao watakuwa wamepitishwa. Kwa wale ambao watakuwa hawajaridhishwa na maamuzi ambayo yameenda kuwaengua

aidha wao wenyewe au ndugu zao au wale watu ambao wana uhakika nao, basi utaratibu wa kukata rufaa kupitia vikao ambavyo vimeainishwa kwa mujibu wa taratibu kwa ajili ya kukata rufaa utafuatwa ili kuhakikisha kwamba watu wote wanaostahiki kuingizwa katika mradi huu wanaingizwa ili waweze kunufaika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, umezungumza vizuri sana kuhusu utaratibu. Kuna watu bado wanachomekwa baada ya mikutano hiyo na mfano mdogo ni kwenye Kata yangu ya Ilala. Nazungumza *through experience,* kuna mama ana miaka zaidi ya 70, lakini wameingizwa watu wenye umri mdogo sana, rufaa imekatwa wamekataliwa, na hii inaelekea labda ni nchi nzima. *Please*! Msiharibu jina la Serikali na nia njema ya Serikali kwa watu ambao wanaingiza ndugu zao kwa maslahi ya pesa ambazo zinawalenga wazee. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Maelekezo yako tunayachukua na tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo, nendeni, pelekeni na TAKUKURU wachunguze Kata ya Ilala Mtaa wa Sharrif Shamba.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Emmanuel Shangai.

Na. 98

**Tathmini ya Uharibifu katika Mto Juhe na Mto Pinyinyi – Ngorongoro**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya tathmini ya uharibifu wa mazingira ya Mto Juhe na Mto Pinyinyi uliotokana na mafuriko – Ngorongoro?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uharibifu wa mazingira ya Mto Juhe na Mto Pinyinyi, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* Kanda ya Kaskazini, inaendelea na kazi ya kutathmini athari za mafuriko kwenye maeneo husika ili kupata taarifa za kina za uharibifu mazingira uliotokana na mafuriko hayo. Taarifa hii itaisaidia Serikali kuona namna bora ya kushughulikia changamoto hizo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mvua zinaendelea kunyesha na uharibifu unaendelea kuwa mkubwa hasa kwenye eneo la Pinyinyi ambalo mafuriko yameendelea kwenda kwenye makazi ya watu pamoja na mto Juhe kuendelea kupanuka sana na kuendelea kufika kwenye makazi ya watu: Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kuhakikisha kwamba madhara makubwa hayatokei kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, Naibu Waziri yupo tayari kuongozana nami ili kwenda kuangalia madhara yanayotokana na mafuriko hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mafuriko haya yameleta athari kubwa, lakini zipo jitihada ama hatua za awali ambazo tunaweza tukafanya ili kuona namna ambavyo tunapunguza hii hali. Kwanza kutokana na kwamba mto huu

umekuwa unapanuka kwa sababu hali ilivyokuwa mwaka 2023 na mwaka 2024 iko tofauti, tumeona kuna haja sasa ya kufikiria kujenga kuta ili mto huu usipanuke. Kupitia mwongozo wetu ule wa usafishaji mito, tunakwenda kusafisha sambamba na kuondoa michanga na tope, pia kuzibua mitaro ambayo inaweza ikasababisha maji kutuama na kukwama na kusababisha mafuriko zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa kutokana na athari kubwa iliyojitokeza, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, nipo tayari kuambatana naye kwenda kuona hali ilivyo. Baada ya Bunge hili tutaenda kuangalia hali ilivyo na namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wananchi. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Hai kumekuwa na mafuriko yanayotokea mara kwa mara, wakati mwingine hata mvua zikiwa hazinyeshi. Juzi saa nane usiku mafuriko yametokea makubwa, yamevunja Daraja la kwa Msomali na maeneo mengine wananchi wamepoteza nyumba, madaraja na barabara zimeharibika sana.

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini kujua chanzo cha mafuriko haya ambayo hutokea kwenye Jimbo la Hai ili kutengeneza njia za kudhibiti kuondokana na kero hii ambayo inajirudia mara kwa mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kutokana na mvua kubwa za masika zinazoendelea, zimesababisha mafuriko na hata kuharibu maisha ya watu na mali kadhaa. Nitoe tu maelekezo kwa Meneja wa *NEMC* kwamba kanda ile waanze kufanya tathmini kuona namna ambavyo tunaweza tukaanza kutoa msaada katika Jimbo la Hai. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Simwanza Sitta.

Na. 99

**Ujenzi wa Karakana na Bweni la Chuo cha Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga karakana ya uchoraji, ufundi bomba, maabara ya kompyuta na bweni la wasichana katika Chuo cha *VETA* – Urambo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya vyuo vya *VETA* vya Wilaya kwa kuongeza majengo ili kufikia viwango vya idadi ya majengo ikiwemo Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Urambo. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilikipatia Chuo cha *VETA*, Urambo shilingi 514,127,605.29 kwa ajili ya ujenzi wa majengo yaliyokuwa yamekosekana katika chuo hicho ambayo ni bwalo, jiko na jengo lenye karakana za umeme na uashi ambapo kwa sasa ujenzi wa majengo hayo unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kujenga miundombinu zaidi kwa ajili ya kuboresha mazingira ya chuo hicho pamoja na vyuo vingine vya *VETA* vya Wilaya ili kuviongezea uwezo na ufanisi wa kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa wananchi yatakayowawezesha kupata ujuzi na kutekeleza shughuli zao za kiuchumi kwa weledi na viwango stahiki kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simwanza Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, katika jibu lake, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali itaendelea, sasa naomba Serikali itoe angalau kauli ya kuanza na jengo moja mwaka huu wa fedha 2024/2025

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tuna upungufu wa walimu tisa. Je, Serikali inasemaje kuhusu kutupatia walimu ili nasi tupate vijana watakaopata ufundi wa kuwasaidia maishani mwao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la kwanza la Mheshimiwa Sitta kuhusiana na suala la mpango wetu kama Serikali. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, kwamba katika mwaka wa fedha 2022/2023 tuliweza kutenga na kupeleka jumla ya shilingi milioni 514.12, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha tumeweza kutenga tena jumla ya shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kuna changamoto za mabweni pamoja karakana nyingine, kwa hiyo, tumeweza kutenga hizo shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo mengine na mwaka ujao wa fedha 2024/2025 tutatenga fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la upungufu wa walimu, ni kweli chuo chetu au vyuo vyetu vina upungufu wa walimu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri Waziri wa Utumishi alisimama hapa terehe 02 mwezi wa Tatu mwaka huu 2024, tumetangaza nafasi za kazi ya zaidi ya nafasi 239 na kati ya hizo nafasi 167 zitakuwa ni za walimu. Tutakapopata walimu hao,

tutahakikisha kwamba tunawapeleka hao walimu tisa katika chuo hiki cha Urambo. Nakushuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Profesa Palamagamba.

Na. 100

**Ujenzi wa Viwanja vya Michezo na Utoaji wa Vifaa katika Chuo cha Ualimu Ilonga – Kilosa**

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Viwanja vya Michezo na kupeleka vifaa vya michezo katika Chuo cha Ualimu Ilonga?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ualimu - Ilonga kina viwanja vitano vya michezo ambavyo ni kiwanja cha mpira wa mikono, mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa wavu na mpira wa kikapu. Viwanja hivi kwa sasa vinafanya kazi, lakini vinahitaji maboresho ili viweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho ya kukamilisha ukarabati wa majengo yote muhimu ya chuo. Baada ya kukamilisha ukarabati huo, Serikali itaboresha viwanja vyote vya michezo sambamba na kuwezesha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo nayapokea, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Je, ukarabati huo unaihusu pia Shule ya Mazoezi ya Ilonga ambayo walimu hao wanaitumia kufundisha ikiwa ni pamoja na masomo ya

michezo ukizingatia kwamba Chuo cha Ualimu Ilonga ni moja ya vyuo vitano tu vinavyofundisha Ualimu wa Michezo kwa shule za msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni nini mkakati wa Serikali kuimarisha elimu ya michezo katika eneo hilo ili Walimu wa Chuo cha Ualimu Ilonga wawe na wigo mkubwa wa kufanya mazoezi ya somo hilo la michezo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Kabudi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba kwa hivi sasa tunaendelea na ukarabati wa majengo muhimu ya chuo hiki, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka itakapofika mwishoni mwa mwaka huu, tutahakikisha kwamba ukarabati huu umekamilika. Ukishakamilisha ukarabati huo, tutakwenda kwenye hivi viwanja vya michezo ifikapo mwakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili kuhusiana na shule ile ya mafunzo au wanaojitolea kufundisha, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli tunatambua uwepo wa shule ile na hivi sasa tunakarabati majengo ya shule. Mara baada ya ukarabati wa shule hiyo, tutaenda kwenye ukarabati vilevile wa viwanja vya michezo vya shule hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mtaala wetu mpya tumeingiza fani hizi za michezo, siyo tu kwa chuo hiki, bali na vyuo vingine, na kwa sababu tuna sera na mitaala mipya ambayo itakwenda kusimamia eneo hili la michezo, tutahakikisha kwamba tunakwenda kufanya kwa umakini mkubwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia na Mheshimiwa Matiko jiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka mitano sasa Serikali haijaweza kuendeleza Kiwanja cha Michezo cha *Nyerere Stadium* kule Mbulu Mjini. Kwa kuwa hakuna hatua iliyochukuliwa, je, Waziri yuko tayari kwenda nami kule Halmashauri ya Mji wa Mbulu kutembelea ule uwanja ili Serikali iweze kuuendeleza? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Mheshimiwa Zacharia anasema niko tayari...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kufuatana naye.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba inakuwa na Kituo cha Michezo katika kila halmashauri *(sports centers)* ambazo zitatumika katika mashindano ya UMITASHUMTA, UMISSETA na UMISAVUTA? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Matiko, kwanza ushauri wake tumeupokea. Jana wakati Mheshimiwa Waziri wa Michezo akijibu hapa, tunakwenda kuanzisha zile *sports arena* kwenye maeneo mbalimbali. Kwa vile huu ni ushauri, kwanza tumeupokea. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

katika mtaala na sera yetu mpya ya elimu, kuna fani mbalimbali ambazo tumeanzisha ikiwemo na hii fani ya michezo. Kwa hiyo, tunaamini wakati wa utekelezaji wa mtaala huu jambo hili la michezo katika kila halmashauri litazingatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Michezo, nimekuona umesimama.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jibu zuri alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumweleza Mheshimiwa Esther Matiko kwamba mkakati wa Serikali ni kuwa na viwanja vya michezo mbalimbali katika kila Makao Makuu ya Mkoa, Wilaya na halmashauri. Tumeanza utekelezaji wa mpango huo katika majiji yetu mawili, tutakwenda kwenye majiji mengine, mikoa mingine na halmashauri zote.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Edward Olelekaita.

Na. 101

**Kulinda Bei ya Zao la Alizeti**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali katika kulinda bei ya Zao la Alizeti kwa kuongeza kodi kwenye mafuta kutoka nje ya nchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuongeza ushuru wa forodha kutoka 25% hadi 35% kwenye mafuta ya kula kutoka nje ikiwemo mafuta ya alizeti yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho. Aidha, Tanzania imeweka kiwango maalumu cha ushuru wa forodha wa dola 500 za

Marekani kwa kila tani moja ya ujazo kwenye mafuta ya kula kutoka nje ya nchi ili kulinda uzalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali inatoza asilimia sifuri ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yaliyozalishwa nchini kwa kutumia mbegu za mafuta ya kula, ikiwemo mbegu za alizeti ili kuhamasisha uzalishaji. Hata hivyo, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya matokeo ya hatua zilizochukuliwa ili kufanya marekebisho pale inapoonekana inafaa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa wananchi wa Kiteto walihamasika sana kulima alizeti kutoka tani 62,000 mpaka karibu 178 baada ya kuona Serikali imetia mkazo kwenye suala hili, kwa nini Serikali isinunue alizeti zilizopo kwa wakulima ambazo ni nyingi sana, na bei imepungua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali au umetoa ushauri tu?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama ushauri hivi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa huo ni ushauri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze kwa namna anavyohamasisha wananchi wake wa Kiteto kwenye ukulima wa alizeti. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Ali Juma Mohamed.

Na. 102

**Shirika la Ndege la *ATCL* Kubeba Watalii**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED** aliuliza:-

Je, sababu gani zinasababisha Shirika la Ndege la *ATCL* lisitumie fursa ya kubeba watalii wanaotoka nchi mbalimbali duniani kuja nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL* inatumia fursa iliyopo ya kusafirisha abiria wakiwemo watalii kwa kuanzisha vituo vilivyo karibu na vituo vya utalii nchini kama vile Kituo cha Kilimanjaro na Arusha kwa watalii wanaotembelea Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Ziwa Manyara, Hifadhi ya Tarangire na Mlima Kilimanjaro. Kituo cha Mwanza kuna Hifadhi ya Serengeti, Kituo cha Zanzibar kuna fukwe za bahari, Hifadhi ya Ghuba ya Johazi, Msitu wa Pongwe pamoja na maeneo ya kihistoria. Kituo cha Kigoma kuna Hifadhi ya Gombe, Kituo cha Mpanda kuna Hifadhi ya Katavi na Kituo cha Iringa kuna Hifadhi za Mikumi, Ruaha na Kitulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL* imeingia mikataba ya ushirikiano wa kibiashara *(interlining)* na mashirika makubwa ya ndege kama Qatar, Emirates, *KLM*, *Air India*, Ethiopia na *Oman Air* ambayo huleta watalii Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na *KIA* ambapo ndege za *ATCL* husafirisha watalii hao kwenda katika maeneo ambayo mashirika hayo hayafiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Mohamed.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina ushauri na swali moja la nyongeza. Nataka nilishauri Shirika letu la Ndege la *ATCL* kuwa kuna takribani mashirika mengi ya nchi mbalimbali huwa yanashiriki katika upelekaji wa watalii katika nchi mbalimbali duniani kwa kutumia *charter flights.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania* nashauri liingie katika biashara hii kwa vile Zanzibar kuna mashirika takribani zaidi ya sita huwa yanatoka nchi mbalimbali za *Europe* yanapeleka watalii na kuweza kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, nalishauri sana Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania* liingie katika biashara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu moja la nyongeza ni kwamba, mnamo mwezi wa Februari Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania* lilitangaza kuanzia tarehe 06 Machi litaanza safari zake za kwenda Kisiwa cha Pemba na wakaanza matayarisho ya kuweza kuuza tiketi, lakini mpaka leo tarehe 17 safari hizo bado hazijaanza. Nataka kufahamu, ni kipi ambacho kinazuia mpaka leo safari hizo hazijaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu mojawapo la Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Nampongeza Mheshimiwa Ali Juma Mohamed kwa ushauri wake mkubwa na mzuri alioutoa kwetu kuhusu *ATCL,* tumeupokea na tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake, kwa nini safari za Pemba hazikuanza pamoja na matangazo kutolewa mwezi wa Pili, sababu ni kwamba ndege tuliyokuwa tumeiandaa ilikuwa ni kubwa na mwitikio wa abiria ulikuwa ni mdogo. Hivyo, ndege hiyo ingeanza kufanya safari zake ingekuwa ni hasara kwa shirika. Tunategemea ndege nyingine ndogo inaingia pengine baada ya mwezi Mei tutaanza kupeleka hao abiria huko. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

Na. 103

**Vigezo vya Kuwatambua Wataalamu wa Hali ya Hewa Nchini**

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR K.n.y. MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza:-

Je, vigezo vipi vinatumika kuwatambua wanataaluma wa hali ya hewa Nchini kwa madaraja yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali huwatambua wataalamu wa hali ya hewa na kuwapa madaraja kwa kuzingatia vigezo viwili ambavyo ni Elimu *(Academic Qualification)* pamoja na uwezo *(Competency)* wa kutekeleza majukumu mbalimbali ya shughuli za hali ya hewa. Kwa mujibu wa Muundo wa Utumishi wa Kada za Hali ya Hewa, Serikali inawatambua wataalamu wa hali ya hewa katika madaraja matatu kama ifuatavyo:-

(i) Mtaalamu Msaidizi wa Hali ya Hewa *(Assistant Meteorological Officer)* anakuwa na elimu ya ngazi ya Astashahada au Stashahada *(Certificate* au *Diploma)* ya Hali ya Hewa au fani nyingine inayohusiana na hali ya hewa kutoka chuo kinachotambulika;

(ii) Mtaalamu wa Hali ya Hewa ambaye anakuwa na elimu ya ngazi ya Shahada *(degree level)* katika fani ya hali ya hewa au fani nyingine inayohusiana na hali ya hewa kutoka katika chuo kikuu kilichopo kinachotambulika; na

(iii) Mtaalamu Mbobezi wa Hali ya Hewa, anakuwa na elimu ya ngazi ya Shahada ya Uzamili katika fani ya hali ya hewa au fani nyingine inayohusiana na hali ya hewa kutoka katika chuo kinachotambulika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ameir.

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inatumia gharama kubwa sana kuwasomesha hawa wataalamu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa na ni kweli kwamba hivi sasa wamekuwa ni msaada mkubwa katika kutunusuru na majanga na matokeo mbalimbali ya mabadiliko ya tabianchi, wengi wao wamekuwa wakihama kutokana na maslahi madogo. Je, Serikali haioni kwamba umefika muda mwafaka sasa kuwaona kwa jicho la huruma ili nao waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na kukaimu kwa mkurugenzi kwa kipindi kirefu katika Mamlaka hii ya Hali ya Hewa jambo ambalo kwa namna moja ama nyingine limekuwa likizorotesha utendaji halisi. Je, ni kipi ambacho kinasababisha hali hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa swali lake la kwanza ambalo anaelezea umuhimu wa uwepo wa wataalamu hao na pengine kuondoka kwao kunaweza kuchangiwa na changamoto ya maslahi. Moja, tunaboresha *incentives package* zetu za taasisi sambamba na kuongeza maslahi yao hatua kwa hatua na mwaka kwa mwaka kwa sababu mahitaji ya nchi yetu ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tunahitaji tuongeze maslahi ya wataalamu wa hali ya hewa. Pia kuna upande wa barabara na kuna maji. Kwa hiyo, tunaongeza kidogo kidogo kulingana na uwepo wa rasilimali fedha. Hata hivyo, tumepokea ushauri wake, Serikali itaendelea kuufanyia kazi ushauri huo ambao ameutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa makaimu, kuna kuwa na sababu mbalimbali na mojawapo ni bajeti kwa wakati huu. Tumepokea hoja aliyoizungumza, tutakwenda kuifanyia kazi Serikalini ili kuona kwamba tunateua watu wa kujaza nafasi hizo kama ambavyo alikuwa ameeleza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Kamani.

Na. 104

**Serikali Kupunguza Faini za Bajaji za Mizigo**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja kupunguza faini za bajaji za mizigo kwa kukosa leseni ya usafirishaji kutoka shilingi 250,000 hadi shilingi 25,000?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)* kupitia Wizara ya Uchukuzi, imeshafanya mapitio ya Kanuni za leseni za Usafirishaji wa Magari ya Mizigo za Mwaka 2020. Miongoni mwa maboresho yaliyofanywa ni pamoja na kupunguza faini za pikipiki za magurudumu matatu (maarufu kama bajaji). Rasimu ya mapendekezo yapo katika hatua za majadiliano ya wadau ambapo *LATRA* itaandaa mikutano ya wazi kwa lengo la kujadili na kupitisha viwango vya faini vitakavyokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa watumiaji wa vyombo vya barabarani kuzingatia sheria za barabarani ili kuepuka kulipa faini zisizo za lazima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa hatua hizi za awali ambazo zinatia moyo. Kwa sheria na kanuni zilivyo sasa hivi, bajaji za mizigo iko kwenye daraja au *status* sawa na malori ya mizigo. Ukiangalia thamani ya vyombo hivi, haziendani na wanapigwa faini zilizo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja na ushauri. Swali langu la kwanza, ni lini hasa utaratibu huu au mchakato huu wa mabadiliko ya kanuni utakamilika ili tuzibadilishe sheria hizi na watu wa bajaji waanze kupigwa faini zinazoendana na thamani ya vyombo vyao?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kushauri kwamba kwa *spirit* ile ile ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipunguza faini za bodaboda kutoka shilingi 30,000 mpaka shilingi 10,000 basi na hata hizi faini za bajaji za mizigo ambazo waendeshaji wake wengi ni vijana, napendekeza zipunguzwe kutoka kwenye hiyo shilingi 250,000 ambayo ipo sasa hivi mpaka kwenye shilingi 25,000. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali tunapokea pongezi ambazo Mheshimiwa Mbunge wa Vijana na Mbunge makini kabisa amezitoa na anasimama kwa niaba ya vijana wengine kuelezea jinsi Serikali hii inavyojali na kuthamini vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunapokea ushauri wake. Tutakapofika hatua ya majadiliano, tutapima kulingana na hali halisi ya mahitaji ya wakati kama hiyo shilingi 25,000 au kiasi kingine

ambacho kitaonekana kinafaa kwa wakati huo. Swali lake anauliza ni lini? Tunafahamu anatamani kuona jambo hili lianze hata kesho. Tunamhakikishia kwamba, tunaamini maboresho haya yanaweza kukamilika kabla ya mwaka huu wa fedha na hivyo ianze kutumika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Hokororo.

Na. 105

**Ujenzi kwa Kiwango cha Lami Barabara ya Masasi – Nachingwea**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Masasi - Nachingwea kwa kiwango cha lami hasa baada ya kusainiwa Mkataba wa *EPC + F*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa *EPC + F* unahusisha kufanya usanifu wa barabara kabla ya kuanza ujenzi. Kwa sasa mkandarasi ameanza na anaendelea na usanifu wa kina. Aidha, Serikali na wakandarasi wanaendelea na taratibu za kupata fedha kwa ajili ya malipo ya awali kwa miradi yote ya *EPC + F* ukiwemo huu wa Barabara ya Masasi - Nachingwea hadi Liwale yenye urefu wa kilometa 175. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya msingi imeonekana changamoto ni

fedha, je, Wizara inawaambia wananchi wa Masasi, Nachingwea na Liwale wasubiri mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. katika Bunge lako hili, Wizara imewahi kujibu zaidi ya mara 15 kwamba Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale itajengwa kwa bajeti ya mwaka 2023/2024 na sasa imebaki miezi miwili. Je, bado tuendelee kuamini kwamba ujenzi huo utafanywa kwa bajeti hii ama vinginevyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa *EPC + F* kama nilivyosema kwa barabara zote saba, Serikali ina dhamira ya dhati kabisa kuzianza na kuzijenga. Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa mikoa ya Mtwara kwa maana ya Wilaya ya Masasi na Lindi, Wilaya ya Nachingwea na Liwale kwamba mpango wa Serikali ni kuanza kuzijenga hizi barabara kuanzia mwaka huu wa fedha. Tayari wakandarasi wako uwandani wakifanya zile kazi za awali. Kwa hiyo, dhamira ipo na hizo barabara tutazijenga. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, tarehe 3 Juni, 2022 niliuliza swali kuhusu barabara ya kutoka Iringa kwenda *Ruaha National Park.* Mheshimiwa Waziri akajibu kwamba wamepata fedha kutoka *World Bank* na wataanza kujenga Aprili, 2023 na sasa hivi ni Aprili, 2024. Sasa ni lini hii barabara itajengwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli fedha ipo na hii barabara ni kati ya barabara ambayo ipo kwenye mpango wa *TACTIC*. Tunavyoongea sasa hivi barabara imeshatangazwa. Sasa hivi tunaendelea kufanya *evaluation* ya hizo *tender.* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Tulisaini mkataba wa barabara ya lami kutoka Sengerema kuelekea Nyehunge mbele ya Televisheni ya Taifa, lakini mpaka hivi hakuna kinachoendelea. Nilipozungumza na Mheshimiwa Waziri aliniambia mkandarasi aliyepata *tender* ile alionekana hana uwezo na kwamba ulikuwepo mchakato wa kutafuta mkandarasi mwingine. Je, hatua hiyo ya kutafuta mkandarasi mwingine imefikia wapi; na lini barabara hii itaanza kujengwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli alichosema. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kuvunja mkataba, kuna taratibu zake ambazo haziwezi zikakiukwa. Hivyo, tayari hatua za kuanza kumtafuta mkandarasi mwingine zinaendelea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Tadayo kwa niaba ya Mheshimiwa Mwantona.

Na. 106

**Uhitaji wa Gari Ofisi ya Uhamiaji – Rungwe**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO K.n.y. MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, lini Ofisi ya Uhamiaji Rungwe itapatiwa gari kwa ajili ya kukabiliana na wahamiaji haramu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anton Mwantona, Mbunge wa Rungwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua ukosefu wa gari kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Uhamiaji, Wilaya ya Rungwe na kwa sasa kuna pikipiki mbili zinazotumika kufanya doria na misako. Serikali inaendelea kutatua changamoto ya ukosefu wa magari kila mwaka katika Idara ya Uhamiaji. Hivyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hali ya bajeti itakaporuhusu Ofisi ya Rungwe nayo itapewa kipaumbele. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Wilaya ya Mwanga ni Wilaya ya mpakani ambayo inakabiliwa na changamoto za wahamiaji haramu pamoja na changamoto nyingine za kiusalama. Je, Serikali iko tayari kuahidi kwamba katika mpango huo wa kutoa magari kwa ajili ya vyombo hivi vya usalama na Wilaya ya Mwanga itapatiwa hasa katika Idara ya Uhamiaji ambayo ina gari moja lililochakaa sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na changamoto ya hali ya kiusalama Wilaya ya Mwanga, kama alivyoeleza Mheshimiwa

Mbunge wa Mwanga, ambayo hata mimi naifahamu, namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika magari ambayo tunatarajia kununua mwaka huu wa fedha ambayo fedha yake imeshatoka, moja tutalipeleka Mwanga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea, muda wetu umekwisha. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Tarimba.

Na. 107

**Kusimama kwa Ujenzi wa Baadhi ya Majengo Dar es Salaam**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza: -

Je, ipi kauli ya Serikali juu ya majengo ambayo ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu Dar es Salaam pamoja na kuweka Sheria ya Ukomo wa Ujenzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba yapo baadhi ya majengo ambayo ujenzi umesimama kwa muda mrefu katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine nchini. Hali hii kwa kiasi kikubwa inasababishwa na baadhi ya waendelezaji kujenga majengo kwa kutumia fedha zao binafsi za kudunduliza na hivyo ujenzi wa majengo husika kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwezesha upatikanaji mikopo ya nyumba, Bunge lilitunga Sheria ya Mikopo ya Nyumba Na. 16 ya mwaka 2008 ili kuwezesha benki za biashara kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba. Hata hivyo, mikopo katika benki hizo imekuwa na riba kubwa jambo ambalo linawafanya

Watanzania wengi kushindwa kumudu mikopo hiyo pamoja na kusababisha gharama za nyumba zinazojengwa kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa kunakuwepo mazingira wezeshi ya ujenzi wa majengo ikiwa ni pamoja na kuhimiza ushindani katika sekta ya fedha ili kuwezesha kushuka kwa riba za mikopo ya nyumba mathalani kutoka asilimia 21 ya sasa hadi asilimia 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imekuwa ikihimiza uzingatiwaji wa Sera ya Ubia katika uendelezaji wa majengo nchini ili kuunganisha nguvu ya mitaji katika sekta binafsi na hivyo kuwezesha kukamilika kwa ujenzi wa majengo kwa wakati. Natoa rai kwa wote ambao hawajakamilisha ujenzi wa majengo hayo katika miji yetu watumie utaratibu wa Sera ya Ubia ili kukamilisha ujenzi wa majengo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia majibu ya Serikali kwenye swali langu hili. Bunge lako Tukufu mwaka 2007 liliwahi kutunga sheria inaitwa *Urban Planning Act,* ambayo inatoa ukomo katika ujenzi. Jengo lazima liwe limemalizika ndani ya kipindi cha miaka mitatu, lakini unaweza vilevile ukaomba ukaongezewa hadi miaka sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hiyo hiyo inatoa adhabu kwa yule ambaye anachelewesha kujenga. Je, swali langu, ni kwa nini Serikali isisimamie sheria hii ambayo imetungwa na Bunge hili pamoja na Kanuni za *Urban Planning Regulations* za Mwaka 2018?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni moja tu, naomba alipatie majibu. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, ujenzi mwingi unadorora kwa sababu ya muundo wa wale wajenzi kutoangalia namna nyingine ya kujiwezesha ili kukamilisha majengo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sheria ipo na katika mazingira ya kawaida, kutokana na mazingira haya ambayo yanakuwa na sababu za wazi juu ya kushindwa kwao kuendeleza ujenzi, ndiyo maana tunatoa wito kwa benki zetu kupunguza gharama za ujenzi ili kuwawezesha Watanzania wengi kwenda kupata msaada kwenye maeneo haya. Sasa sheria hiyo unaweza ukaitumia ndiyo, lakini uhalisia unaelekeza namna nzuri ya kuwawezesha Watanzania hawa kufikia malengo yao ya kujenga majengo kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. Sasa matangazo ya wageni.

Nitaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 70 wa Mheshimiwa Spika ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia *(MUST)* kutoka Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa Profesa Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambao ni viongozi wa CWT Wilaya ya Rombo na UVCCM Kata ya Holili kutoka Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wapo wageni 175 wa Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati ambao ni Wakurugenzi wa *TANESCO* Kanda, Mikoa na Wilaya Tanzania Bara. Kwa kweli sasa hivi *TANESCO* mnafanya kazi vizuri sana, hongereni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda ambaye ni mdogo wake kutoka Mkoa wa Mtwara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Tarime Vijijini, Mkoa wa Mara, karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Kakunda, ambao ni Wachungaji wa Kanisa la Moravian kutoka Manyoni, Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Florence Samizi, ambao ni kaka zake kutoka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni saba wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, kutoka Mkoa wa Geita, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 15 wa Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, ambao ni Watendaji Kata na Vijiji kutoka Wilaya ya Igunga, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Ally Makoa, ambao ni Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Kondoa Mjini, Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ambao ni wafanyakazi nane wa kampuni ya *Global Fortune* inayohusika na uuzaji wa viwanja katika Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa amemkaimisha Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kushika nafasi yake kwenye Bunge. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na Mheshimiwa Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Monni ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema na leo tuko salama. Pili, nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa heshima kubwa ambayo ametupatia Majimboni kwetu kupitia miradi mingi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kiteto lilinufaika sana, tumepata shule mpya za sekondari tatu, madarasa karibu 57 ya shule shikizi 18, tumepata *VETA, ambulance*, magari mawili, vituo vya afya na miradi mingi sana. Kwa dhati kabisa wananchi wa Kiteto wanamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi mingi sana. Nadhani amewajengea Waheshimiwa Wabunge heshima kubwa sana kwenye Majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mawaziri wa TAMISEMI, Makatibu Wakuu na watumishi wote kwa kazi ambayo wanaendelea kuifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia miradi ya TAMISEMI. Baada ya pongezi hizo, niseme kuhusu changamoto za Jimbo la Kiteto kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sisi mwaka 2021/2022 tulikubaliana hapa kwamba, kwa sababu kuna uhitaji mwingi wa vituo vya afya, tumalizane na vituo vya afya vya tarafa kwanza

kabla hatujaenda kwenye kata. Kiteto mpaka sasa tunadai vituo vya tarafa vitatu; Tarafa ya Makame, Kibaya na Dosidosi. Vilevile, tulileta maombi ya vituo vya kimkakati vya Matui na Dongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana watu wa TAMISEMI, tukisema tumalizane na tarafa kwanza, basi tumalizane na tarafa kwanza kabla hatujaenda kwenye kata nyingine. Itakuwa *very unfair* kama kuna wengine wanajenga za kata wakati wengine sisi tunahangaika na za tarafa. Safari hii nawaambia tu kwamba tunataka hizo za tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *TARURA*. Jimbo la Kiteto ni kubwa sana, ni *size* na baadhi ya mikoa. Mtandao wa barabara ni mkubwa sana, karibu kilometa 1,291 hivi. Bajeti tunayopata ni ndogo sana, ni *2.8 billion shillings*. Uhalisia ilitakiwa tupate zaidi ya shilingi bilioni 11, lakini kwa sababu sisi ni waungwana sana, tunataka nyongeza tu ya shilingi bilioni tano, tuongezwe kutoka shilingi bilioni 2.8. Ikifika shilingi bilioni tano tutaweza kuhangaika na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena kwa mvua zinavyonyesha sasa, miundombinu imeharibika sana. Ni kama hakuna mawasiliano kati ya Tanga na Kiteto kwa sababu barabara hiyo ni mbovu sana. Barabara nyingi zimeharibiwa na mvua, kwa hiyo, tunatarajia tathmini inayoendelea ya kuangalia miundombinu iliyoharibika, Kiteto mtupe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hospitali yetu ya wilaya, tunashukuru mmetupatia zile shilingi milioni 900 kwa ajili ya zile hospitali kongwe za wilaya. Kwa sababu Wilaya ya Kiteto ni kubwa, imezungukwa karibu na wilaya saba, bado kuna upungufu wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba TAMISEMI muangalie Kiteto, bado tuna jengo la dharura, *Emergency Medical Department, ICU, RCH (Reproductive, Child Health),* na jengo la *X-Ray*. Tukipata majengo haya itafanya Hospitali hii ya Kiteto iwe *full-fledged*. Kwa sababu inahudumia watu wengi sana na wilaya nyingi

zinazopakana, mkitupatia kipaumbele hicho, wananchi wa Kiteto watakuwa wamefurahi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni ushauri, ipo miradi ya wananchi ambayo ni mabweni, zahanati na madarasa. Wapo wananchi wa Kiteto ambao kwa nguvu zao wenyewe wamejenga zahanati, madarasa na mabweni mpaka kufikia kwenye lenta. Tunaomba TAMISEMI sasa, hebu mtafute fedha maalum ambayo kazi yake ni kuhangaika na kumalizia miradi ya wananchi ambayo wametumia nguvu nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda Mbigiri wana zahanati yao, Magungu wamejenga bweni, maeneo mengine kama Krashi, Zambia, Ilala; wananchi hawa ili tuwatie moyo na kwa sababu Sera ya Serikali ni kwamba wananchi wakishafikisha miradi yao mahali, Serikai itapokea na kumalizia. Kwa hiyo, kama mtaweza kutafuta fedha maalum kwa ajili tu ya miradi ambayo wananchi wamehangaika kufikisha mahali, itawatia moyo zaidi na kuwafanya waendelee kufanya juhudi za kushirikiana na Serikali kujenga miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *10 percent* ya fedha zinazotoka halmashauri, tumesikia hapa kwamba mmetengeneza *formular* ya kuanza na halmashauri karibu kumi hivi na nyingine ziendelee lakini mmesema sheria itabadilika, sasa ni vyema tukafahamu kama suala linaanza mwezi wa Saba mwaka huu, basi sheria na kanuni zinahitajika zikamilike mapema sana ili wananchi wasiendelee kuchelewa kusubiri mabadiliko ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiteto ina shule mbili tu za kidato cha tano na cha sita. Tulishaleta maombi TAMISEMI na timu ilitumwa kwenda kuangalia shule zetu hizo; Shule za Ndedo, Dongo, Njoro, Dosidosi na Sunya. Sasa tunaomba majibu, ni lini mtapandisha hadhi shule hizi ambazo TAMISEMI ilikuja kuziangalia kwa ajili ya kidato cha tano na sita?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiteto kuwa na shule mbili tu za kidato cha tano na cha sita siyo sawa. Kwa hiyo, tunaomba mtoe kipaumbele ili wananchi wa Kiteto wapate kunufaika na miradi hii ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa habari ya *CSR* na Serikali ina mapendekezo kwamba wanataka kutengeneza *formular* mpya kwa ajili ya *CSR*, kwa sababu Kamati inayosimamia TAMISEMI vilevile inakubaliana na wazo hili. Nadhani ni vyema mfanye hivyo haraka ili *CSR* ipate kuwa na manufaa kwa Watanzania wengi ambao wapo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa *DC* wangu na Mkurugenzi wa Kiteto, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Yale magari ambayo mnataka kununua, hizi wilaya ambazo ni mikoa, ni kubwa, ni afadhali mtoe kipaumbele ili wakapate kufanya kazi nzuri zaidi ya kuwahudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa shule za sekondari, bado nina kata karibu mbili hazina shule za sekondari; Kata ya Makame na Kata ya Laiseri. Nashukuru kwa zile tatu mlizotupa, lakini kwa sababu sera ya nchi ni kuwa kila kata iwe na sekondari, ni vyema basi mkatupa kipaumbele tukapata shule mbili mpya za sekondari tumalizane na habari ya kata. Halafu mbaya zaidi kati ya hizo kata, mojawapo anatokea Mbunge. Kwa hiyo, ni vyema mkatoa kipaumbele hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja tuwa-*support* TAMISEMI wapitishe bajeti yao. Ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma, halafu Mheshimiwa Monni ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika

bajeti ya Wizara ya TAMISEMI. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais na pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa sana walizofanya kwenye Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wanajimbo la Geita Vijijini, tunashukuru sana Serikali kwa kazi nyingi na nzuri ambazo hazijawahi kufanyika kwenye Jimbo hili la Geita. Pili, nampa pole sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kwa matatizo yanayoendelea huko kwake, tunamwombea Mungu ampe wepesi ili maafa yale yasiendelee kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nachangia kwa upole kwa sababu Mheshimiwa Waziri ana matatizo, itabidi nipige kidogo kidogo. Nimesikia kwenye hotuba ya Waziri amesema wamejipanga kuikagua na kuisimamia miradi ya *CSR*. Moja ya maeneo anzilishi ya *CSR* kwenye migodi mikubwa ni Geita. Hiki kimekuwa kilio chetu; mimi Mbunge wa Geita na Mbunge wa Busanda. Tuna matatizo makubwa sana ya usimamizi wa miradi ya *CSR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelalamika kwa Mheshimiwa Waziri wa Madini, lakini kuna kanuni ambazo zilisainiwa, tunaomba miradi hii ikaguliwe na hizi Wizara zote. Kama TAMISEMI inakagua, lakini pia na Wizara ya Madini muone namna ya kuifanya hii miradi kama miradi ya Serikali isionekane kama miradi ya hisani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Geita *DC* mwaka 2023/2024 tulipata fedha shilingi bilioni tisa kwenye *CSR,* lakini mpaka leo tunazungumza na bajeti ilikuwa imalizike mwezi wa 12, mpaka tunaenda kuandaa bajeti nyingine tumetumia shilingi bilioni moja. Sisi kama halmashauri, kwenye kanuni hazitupi nguvu ya kuikagua na kuisimamia ile miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mawazo ya Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, nadhani huu ni mwarobaini, kwa sababu tumekuwa na matatizo. Hatuna uwezo wa kuisimamia miradi, hatusimamii tenda, wanasimamia wao, lakini ikija ukaguzi wa *CAG* inayoangushiwa doa ni Halmashauri ya Geita na Halmashauri ya

Mjini. Kwa hiyo, kwa mwarobaini huu, ninamuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwamba kama kuna kanuni zilikosewa, zirekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kwenye hilo, naomba sana ukienda kwenye migodi inayosimamiwa na Barrick, hizi tenda zote zinashughulikiwa na halmashauri, halafu wao wanasimamia kiwango na kulipa. Geita imekuwa tofauti, yaani sisi ni watazamaji, *tender* watangaze wao, kusimamia wasimamie wao, wakiharibu waharibu wao, halmashauri inaanguka na hati chafu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, wazo lako hili kama litafanikiwa, tunakukaribisha *model* ya kwanza uje uchukue Geita kwa sababu ndiko kwenye miradi mibovu na mpaka mwezi wa 12/mwezi wa kwanza tumekataa kujadili bajeti mpya kwa sababu bado tuna shilingi bilioni nane na kitu kwenye halmashauri yetu na hatujawahi kuoneshwa bakaa toka mwaka 2018 tunapelekwa kama wakokozi. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, ziara ya kwanza ianzie Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka kusema kwamba, Watanzania wanaliamini Bunge. Mimi nina mwaka wa nane humu ndani, kuna vitu vinakuwa vinazungumzwa tunaona kama haviwaumizi wananchi, lakini kwa uelewa wangu kama Daktari wa Akili, ninaona tunakwenda kutengeneza Taifa la watumishi wezi kwa sababu wanalalamikia kila siku suala la kikokotoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijasoma sana, lakini nikiangalia, mtu anapata 30%, halafu 70% unamtunzia. Maana yale kama alikuwa analipwa mafao ya shilingi milioni 100, anakuja kutoka na shilingi milioni 30, ndiyo akaanze kujenga ka-*slope*, lazima niibe bana, kwa sababu najua hela zangu kule sitapewa. Hili ndilo Bunge na nimemsikia jana, nam-*quote* Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Bwana Nchimbi, ameeleza vizuri, amesema hapana, hakiwezi kuwa kilio cha kila siku na sisi tunajiwekea pamba masikioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Waheshimiwa Mawaziri na Serikali mkae chini mtafakari. Kama mnaweza kurudi kwenye asilimia 50 au tuone namna yoyote, kwani Watanzania hawawezi kuwa wanalia halafu sisi tunazungumza mambo yale yale toka miaka miwili, mitatu, haiwezekani. Kama kuna tatizo, tuambiwe. Hawa ni watumishi wetu, vinginevyo hakuna mtumishi atakuwa mwaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimebakiza miaka mitatu ndiyo watoto wangu wamemaliza digrii ya kwanza, halafu natakiwa nistaafu nikajitegemee wakati sina nyumba, nipo kwenye nyumba ya Serikali, halafu naenda kupata 30%. Lazima niondoke na mzigo, liwalo na liwe. Kwa hiyo, ni vizuri tusijiwekee pamba masikioni, tuone namna ya kuwasikiliza na kama kuna uwezekano wa kuweza kutatua hilo tatizo, basi tulitatue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tukisimama kwenye majukwaa, hakuna mtu anazungumzia mambo ya barabara tena. Watumishi wote wanalia, wanazungumza suala la kikokotoo, kila siku ni hayo hayo. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali tukae chini na sisi kama Bunge, tuishauri Serikali tuone namna ya kutengeneza furaha ya watumishi ambao wanakaribia kustaafu na wale wengine ambao wana nia nzuri na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana viongozi wa Serikali ni lazima msikilize na ninampongeza sana Katibu Mkuu wa chama kwa sababu naye ameliona, nadhani sasa tukienda Pamoja; chama na sisi Waheshimiwa Wabunge na kwenye huu muda mzuri wa kwenda kurudi kwa wananchi ndiyo mahali penyewe inabidi tukazie ili watumishi wetu waweze kupata amani na kuwa na matumaini na ajira zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la *TARURA*. Najaribu kuangalia, kwanza nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge tulivyopitisha bajeti ya mwaka 2023/2024 kuiongezea *TARURA*. Najaribu kuangalia kama tungekuja na wazo tena la kuongeza kidogo tu kwenye *TARURA*, nadhani baada ya

miaka mitano Bunge lijalo wale watakaokuwemo humu ndani, *TARURA* itafanya vizuri sana kama *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyokuwa kwenye barabara zetu kwenye majanga haya yaliyotokea, *TARURA* amekuwa mkombozi mkubwa sana. Nampongeza sana Mkurugenzi wa *TARURA*. Unajua kuna ofisi nyingine tunaogopa hata wakisikia kuna Mheshimiwa Mbunge yuko nje, anaanza kusema wakuda wanaingia, watu hao wanafiki. Ukiingia *TARURA* kwa kweli Mkurugenzi Mungu ampe maisha marefu, na hata kama ajira yake itakoma, mimi nakuombea Bwana Seff kama uko humu, kwa kweli uongezwe, uongezwe hata muda. Nimechapia, unajua mimi Kiswahili, usukumani kidogo tuna shida ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiingia ofisini kwake anakusikiliza. Leo ukienda mpaka majimbo ya vijijini kama kwetu, kuna lami, hongera sana Mkurugenzi wa *TARURA*. Naomba kama kuna chochote cha kuweza kuiongeza nguvu *TARURA*, nadhani tumeenda vizuri na ushauri wetu Serikali mmeufanyia kazi vizuri na hali zetu kidogo kule siyo mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia. Natoka Geita, nina miradi 780 inayofanya kazi, sasa hivi inasimamiwa na Injinia, halafu Mhandisi ni mmoja. Mradi mmoja upo kilometa 150. Naiomba Wizara, angalieni halmashauri ambazo zina maeneo makubwa na miradi mingi, tafadhali sana tuongezeeni ma-*engineer* kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kusimamia miradi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza hiyo!

**NAIBU SPIKA:** Bado, bado, bado, endelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, aah, bado, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali muone halmashauri ambazo ni kubwa, ziongezeeni watumishi. Huwezi kukagua miradi 780, hata wewe Waziri umewekewa Manaibu Waziri wawili na Makatibu Wakuu watatu kwa sababu wizara ni kubwa. Halmashauri ina kata 50, halafu ina vijiji karibu 600, miradi 700, mtu mmoja unawezaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo hata Wakaguzi wa Ndani, Halmashauri ya Geita ina Mkaguzi wa Ndani mmoja, miradi 780, matokeo yake badala ya kukagua kuzuia wizi, tunakagua baada ya wizi. Kwa hiyo, naomba sana, ni vizuri mkatuongezea watumishi kulingana na ukubwa wa maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri amekuja Mheshimiwa Waziri Mchengerwa. Naona Mheshimiwa Simbachawene ungetuachia tusikilizwe. Mheshimiwa Mchengerwa umekuja, nakuomba, nilishazungumza humu ndani, nina kituo cha afya kinaitwa Nkome, kila mwezi tunazaa shule, kijiji kimoja kina shule 13, kina sekondari tano, halafu bado zahanati. Zahanati inayozalisha watoto 400, mnasubiri nini kutupa fedha tukajenga kituo cha afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshaahidiwa mwaka wa nne huu. Mheshimiwa Waziri, usipokuja na majibu, wewe ni mshikaji wangu; akiwa Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy amekuja akaahidi, Mheshimiwa Dkt. Dugange amekuja akaahidi, Mheshimiwa Silinde amekuja akaahidi, hii ya mwisho. Hii sasa ni *swaga* ya mwisho. Nakutaarifu kabisa, shilingi yako naandika jina leo, kama hujaja na majibu ya kuniambia fedha inayoenda Kata ya Nkome kwenye zahanati inayozalisha watoto 420 kwa mwezi, mzee leo naondoka na shilingi, urafiki wetu utaishia leo. Najua kwa sababu una matatizo, una mafuriko nyumbani, huruma ile ile ya Rufiji nadhani utailekeza na kwenye jimbo langu ili wananchi wangu waweze kufurahia Serikali ya Mama Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tunavyo vituo vya afya, mlitupatia shilingi milioni 470, mpaka leo hatujawahi kumaliziwa, kimesimama. Tusaidie, sekondari vilevile tusaidie ili tuweze kumaliza. Vilevile halmashauri yangu ni mpya, mmetupa shilingi milioni 150 ya kujenga nyumba ya mkurugenzi, mmesimamia hapo hapo shilingi milioni 150, wenzangu wameshapewa shilingi milioni 300, wamejenga mpaka na *swimming pool*. Tunatamani sana na sisi watu wa kijijini kuwaona wafanyakazi wetu wanakaa katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na ninaamini Mheshimiwa Waziri Mchengerwa umepitiliza lile la kituo cha afya, pamoja na mambo mengine, ujiandae kuja na majibu, swaga nimeshapigwa nyingi, leo hii ni ya mwisho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni, jiandae Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia agenda iliyopo mezani kwetu. Kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ametujalia afya njema, ametujalia uhai na leo nimepata nafasi ya kusema hapa. Naomba pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ya kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kidogo kwenye elimu. Miaka mitatu iliyopita kulikuwa na changamoto kubwa sana ya madarasa hasa kwenye jimbo langu. Kulikuwa na changamoto kubwa sana ya shule za msingi, lakini pia kulikuwa na changamoto

kubwa ya shule ya sekondari, nataka kipekee kabisa kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa mwaka 2023 tu tumepewa zaidi ya shilingi bilioni tano ambazo zimefanya kazi kubwa kwenye elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka miwili hii tumefungua shule 11, shule za msingi zimeanzishwa na zimefunguliwa. Pia tumejenga sekondari tatu. Kwa hakika haya ni mambo makubwa sana yamefanyika na watu wa Chemba wanawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga shule za kutosha, na tumejenga madarasa ya kutosha, ila kuna changamoto moja ambayo sasa nafikiri ni lazima tuiangalie vizuri. Changamoto hii inakabili zaidi shule nyingi za vijijini au majimbo mengi ya vijijini. Ujenzi huu mpya unaofanyika wa madarasa, unakuja na madawati yake, lakini uhai wa madawati yanayotengenezwa sasa hivi, siyo zaidi ya miaka mitano au saba. Kwa hiyo, ndani ya miaka mitano au saba yale madawati tayari yanakuwa yamepotea au yamechakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakujawahi kuwa na mkakati wa makusudi wa kuhakikisha sasa shule zote za msingi au madarasa tuliyonayo kuna madawati ya kutosha. Nimejaribu kufanya tafiti kidogo, ukija kwangu Chemba, wanafunzi ambao hawana madawati ni asilimia 48. Mahitaji ya madawati ni 21,000 *plus*, yaliyopo ni 10,000, unaweza ukaona upungufu tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sehemu kubwa ya madawati haya yanatengenezwa na wazazi. Sasa kama Serikali ilivyoamua kuja na mkakati wa kujenga shule, ni lazima tuwe na mkakati wa makusudi wa namna gani sasa tunaimarisha kutengenezwa kwa madawati mara zote ili upungufu huu usiwe mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili ni changamoto ya walimu. Nataka kuishukuru sana Serikali, kwani nilisimama hapa mwaka 2021, upungufu kwa sekondari ulikuwa ni asilimia 38, lakini leo tunaongelea upungufu kwa walimu wa shule za sekondari ni asilimia kama 11 tu. Kwa hiyo, naishukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto kubwa ya walimu wa shule za msingi. Chemba ni karibu sana na mjini, karibu na Makao Makuu, hata shule za barabarani zenyewe zina upungufu mkubwa sana wa walimu. Mahitaji ya walimu kwa Chemba ni 1,600 na waliopo ni 800, upungufu ni zaidi ya asilimia 50. Nawaomba sana, najua kuna ajira hizo mpya zinakuja, mzingatie kwenye shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu uliopo sekondari unakubalika, nami nakiri na ninawashukuru sana Katibu Mkuu, Mheshimiwa Waziri na watumishi wote wa TAMISEMI kwa sababu naamini mlisikia ombi langu mkapunguza kwa kiwango. Naamini na leo mtasikia ombi langu kwamba upungufu uliopo kwa *primary school* ni mkubwa sana, ni asilimia 50. Nyie mnajua kwamba kuna hitaji sasa walau watoto wetu wasome kama watoto wa mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongea kidogo kuhusu *TARURA*. Wenzangu wameongea sana, lakini naomba hili lizingatiwe kidogo. Sina hakika. Narudia tena, sina hakika kama kuna takwimu sahihi za ugawaji wa fedha kulingana na urefu au idadi ya kilometa. Nimekuwa nikiona kuna shida kubwa kidogo.  kuna shida kidogo *TARURA*. Tumeongeza bajeti mwaka 2023, lakini fedha zinazokuja *ceiling* ni ile ile. Sasa ile tunayoongeza huwa inapelekwa wapi? Eti, sijui Waheshimiwa Wabunge wenzangu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namwuliza Mheshimiwa Mbunge mwenzangu hapa, hivi wewe zile fedha tulizoongeza mwaka 2023 kwenye bajeti umeziona? Nimeendelea kupewa *ceiling* ya muda mrefu ile ile wakati tumeongeza fedha. Sasa sijui nini kinaendelea? Naomba sasa hebu ifanyike tafiti ifahamike wazi kwamba jimbo fulani au wilaya fulani urefu wake wa kilometa ni kadhaa na wapewe fedha kulingana na kilometa zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukashangaa Kiteto au Chemba ina kilometa ndefu, lakini mtu ambaye ana wilaya zenye barabara za kilometa chache, anapewa fedha nyingi kuliko yule

ambaye ana kilometa nyingi. Sasa hii hapa naiomba ifanyiwe kazi. Mheshimiwa Waziri, hili jambo niliwahi kusema huko nyuma, niliwahi kusema kwenye *RCC,* lakini naomba sasa wewe mwenyewe ulichukue. Ni lazima hizi rasilimali, hizi fedha zinazotolewa zigawiwe kwa uwiano sahihi ili zikatibu changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Chemba zimekatika, naomba kukwambia, kwa Mtoro – Swagaswaga tuliomba fedha za dharura kwa sababu mvua iliyonyesha imekata hii barabara. Tukaomba Ilasehani shilingi milioni 94.8, tukaomba kwa Mtoro – Sanzawa shilingi 263,000,000, barabara hizo zimekatika na huko ndiko mashamba yaliko, na huko ndiko alizeti inapolimwa, huko ndiko mazao yote yanapolimwa, sasa sijui ni nini kinaendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tukaomba fedha Kidoka – Pangalua shilingi milioni 146, tukaomba fedha za Soya – Majengo shilingi milioni 101. Mheshimiwa Waziri, tunavyoongea hivi, saa nyingine wewe mwenyewe unaogopa kupokea simu za watu wanaopita huko kwa sababu magari ya minadani yanakwama, magari yanayochukua mazao yamesimama na fedha zote tumeomba shilingi milioni 600 kwa ajili ya dharura, lakini mpaka leo tumepewa shilingi milioni 62.2 ambayo inatosha kutengeneza daraja moja tu. Kwa hiyo, njia nyingine tano hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba inawezekana hamwelewi ukubwa wa hili jambo, hali siyo nzuri, hali siyo salama, mazingira ni magumu sana. Kwa hiyo, nawaomba sana sana sana, tumeomba fedha za dharura, naomba fedha hizo ziweze kutolewa walau kunusuru hali iliyopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuongea kuhusu watumishi wa afya. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumejenga vituo vya afya vya kutosha, tumejenga zahanati za kutosha, lakini pia mwezi wa tano tunategemea kufungua zahanati nne mpya. Watumishi wanaohitajika ni 854, waliopo ni 200 na kitu. Sasa hii ni asilimia 30 tu ya watumishi wanaohitajika, ndiyo waliopo. Sasa tunaenda kufungua kituo cha afya kipya, na tunafungua zahanati

nne mpya. Sasa ni namna gani tutafanya ili kuhakikisha walau tunapunguza kwa asilimia kadhaa? Hali ni nzuri kwenye miundombinu ya ujenzi lakini changamoto kubwa ni watumishi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wakati wanapanga watumishi, wasikie sauti yangu kwamba Chemba kuna changamoto kubwa sana ya watumishi wa kada ya afya. Ni asilimia 30 tu kati ya wale wanaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea kidogo, ni kuhusu watumishi wetu ambalo wenzangu wengi wameliongelea. Kwa hakika sisi Waheshimiwa Wabunge tunakuwa wanyonge sana linapoongelea suala la kikokotoo. Mwenzangu Mheshimiwa Musukuma kaeleza, lakini tunafahamu shida tunazopata kule na kule saa nyingine inaonekana kama ni jambo ambalo sisi hatuliongelei kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana sana, tuangalie namna ambavyo tunaweza kufanya kama dhamira ya Rais ilivyo ya kurekebisha ili hali iwe salama. Hatuwezi kuendelea kuishi na watu ambao wana manung'uniko makubwa na wao wanatusaidia kazi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, wenzangu wote wamesema kuhusu magari ya ma-*DC*. Gari yetu iliharibika, ikapotea, ikatafutwa gari nyingine ndiyo inayotumika sasa hivi pale. Jimbo la Chemba ni jimbo kubwa, refu, nami ndiye Mbunge pekee ninayepakana na Wabunge wenzangu tisa. Unaweza ukaona ninateseka kiasi gani kuwa hakuna gari salama la uhakika ambalo linaweza kuzunguka jimbo zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa unagawa magari hayo ambayo amedhamiria kuyanunua na kuyapitisha kwenye bajeti hii, aangalie namna gani ambayo anaweza kuleta gari moja kwa ajili ya Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wenzangu ninaofanya nao kazi Chemba, ambao wanafanya kazi vizuri sana. Nasema ukweli kwamba injinia wa *TARURA* anafanya kazi kubwa, Mkurugenzi na Wakuu wa Idara wanafanya kazi kubwa na mambo yanaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana wakati tunatangaza Wakuu wa Mikoa, *Comrade* Daniel Chongolo hakuwepo, alikuwa na majukumu ya kitaifa. Naomba kumtambulisha kwenu sasa. Karibu sana *Comrade* Chongolo katika Bunge. *(Makofi)*

Vilevile kulikuwa na wageni tuliwaita lakini walikuwa hawajaingia, wageni 70 wa Mheshimiwa Spika, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia kutoka Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwanza Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa nchi yetu na kwa Wilaya yetu ya Magu kwa miradi mbalimbali ambayo ameweza kutuletea kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma, lakini bado nchi hii ina mahitaji mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapompongeza Mheshimiwa Rais, tunaendelea kusema kwamba Bunge hili linapopitisha bajeti, fedha hizi ziende kwenye miradi hiyo ambayo tunataka kuishauri Serikali. Pale Magu tunalo jengo la halmashauri

ambalo limekaa kwa muda mrefu sana. Mheshimiwa Naibu Waziri umelitembelea na ulienda na Kamati yako ya TAMISEMI. Kwa kweli ni jengo zuri, likikamilika watumishi wetu watatoa huduma inayostahili kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tumekuwa tukipewa fedha kidogo kidogo sana na bahati mbaya mmewaweka wakandarasi SUMA JKT, nao fedha zikiisha wanasimama. Kwanini Serikali isitoe fedha ili jengo hili likamilike? Tunahitaji shilingi bilioni 2.9 tu jengo hili likamilike. Naomba sana sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, hebu toa fedha kuliko kuwa na jengo ambalo limemaliza miaka zaidi ya 12 lipo, lakini halitoi huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia *value for money* inakosekana sasa. Thamani ya fedha inakosekana kwa sababu jengo hili limekaa kwa muda mrefu sana. Tupatie shilingi bilioni 2.9 ili tuweze kukamilisha jengo hili na halmashauri ihamie hapo, watumishi wote waweze kutekeleza majukumu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaweka shilingi milioni 50 kwa kila zahanati kwa zahanati tatu, lakini wananchi wamejenga maboma mengi sana. Hapa ninapoongea, sasa hivi Magu tunayo maboma 38 ambayo yako katika hatua mbalimbali, mengine yameezekwa, mengine bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji fedha za kukamilisha ili wananchi wetu wapate huduma ya afya karibu. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie, pamoja na kazi ambayo mmeifanya hebu tumalizie haya maboma ili tusiwakatishe tamaa wananchi. Mimi kwa upande wa Magu nahitaji shilingi 2,315,000,000 tunamaliza, na wananchi hawa watatibiwa karibu kila Kijiji hapo. Hebu tuwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji wananchi wanatembea kilometa 20. Akina mama wajawazito, akina mama wenye watoto, wanatembea kilometa 20, ni mbali sana. Hebu tuwasaidie, tutoe

fedha hizi ili tuweze kukamilisha ujenzi huu na hapo ndipo tutakuwa tunatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi iliyosema kila kijiji kiwe na zahanati. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, jambo hili liweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu elimu ya msingi. Wananchi wetu wamejenga maboma ya kutosha na Waheshimiwa Wabunge hapa kila mmoja anazungumza juu ya jambo hili. Maboma mengi yamejengwa na wananchi na wengine watoto wetu wanatembea kilometa 15 au 17 kutoka shule ilipo kwenda kwenye shule nyingine. Kwa hiyo, tukiweza kukamilisha ujenzi wa maboma haya ya shule ambayo wananchi wameuanzisha katika vijiji vyao, tutakuwa tumetatua jambo muhimu sana la kuwapatia watoto elimu sehemu ambayo ni ya karibu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Mheshimiwa Waziri afikirie mtoto wa chekechea anatembea kilometa 15, au 16, huyo kweli atapata elimu bora? Kwa kuwa mpaka anapofika shuleni anakuwa tayari ameshachoka, anaanza kusinzia, huyo atasikiliza! Hata yule wa darasa la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, tuone umuhimu wa Serikali kuangalia namna ambavyo inaweza kupata fedha ili tukamilishe haya maboma. Maboma haya ya Shule za Msingi Magu, natarajia nikipewa shilingi bilioni 2.6 nitayakamilisha na watoto watasoma. Ninaomba sana tuwahurumie watoto hawa, ni wa kwetu, tunajenga Taifa ambalo watakuwa viongozi wa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya sekondari, hivi karibuni, Magu mmetupatia shilingi bilioni 2.6 na Wabunge wengine pia wamepewa hizo fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya sekondari ili ziweze kuanza, kwa sababu watoto wanatembea umbali mrefu. Fedha hizi zimekuja, lakini tatizo ni mfumo, fedha hizi hazishuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui mnanisikiliza? Naona mnaongea hapo watatu, mngenisikiliza kwanza halafu saa saba mtaenda kujadiliana, lazima tuwe *serious* na jambo hili! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kuna tatizo la mfumo, fedha hazishuki. Kwenye halmashauri yangu zimetoka kwenda shule za sekondari, lakini kule shule za sekondari hawajapokea. Tulitarajia mwezi wa tatu hawa watoto wahamie kwenye hizo shule kwa sababu wanatembea umbali mrefu, leo mwezi wa nne tumeumaliza tunakwenda mwezi wa Tano, sasa hizo shule tutazimaliza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi wangu ameandika barua kuja Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Katibu Mkuu hebu angalia ni mfumo gani huu usioona hizi Shule za Sekondari za Magu kuwekewa fedha ziende zikafanye kazi? Kwa sababu, hela zisipoenda haraka maana yake ni kwamba hata gharama za *material* zinapanda. Kwa hiyo, naomba sana hili lishughulikiwe. Katibu Mkuu kama upo hapa, wape *memo* watu wako waanze kulishughulikia sasa ili tupate majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA*. Ukiwasikiliza Waheshimiwa Wabunge hapa, wengine wanaomba maeneo ya utawala yapunguzwe, siyo kwamba wameshindwa kuyahudumia, hapana. Tatizo ni mgao wa fedha usiowiana kwenye barabara. Kwa mfano, kuna watu wana kata nane, sisi tuna kata 25, lakini mgawo wa fedha za barabara tunapata sawa, haiwezekani. Ni lazima tuangalie uwiano wa eneo lilivyo kwa *population* na *square meter* za eneo hilo. Kwa hiyo, huwezi kugawa shilingi bilioni 2.8 kila jimbo au kila wilaya, haiwezekani. Lazima tuangalie hawa wana shida gani? Pia tuangalie na hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Magu ni ya mwaka 1974, imezaa miji kadhaa. Mji wa Kisesa unastahili kuwa Makao Makuu ya Wilaya, lakini hauna barabara, hauna mitaro, unatenga fedha ambazo zinalingana na kata nane! Haiwezekani. Hata Busega kwa rafiki yangu hapa, watu wangu wakienda kwenye kilio

kule Busega wakirudi wanasema Busega ina barabara nzuri kuliko Magu, angalia eneo ulilonalo, yaani kwa kweli inauma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mchengerwa aangalie wilaya zilivyo na mgawo ulivyo. Huwezi kuwa unauliza, kwenye kikombe cha chai niweke sukari vijiko vingapi? Angalia kwanza kikombe chenyewe, wewe unasema vijiko vingapi? Angalia kikombe chenyewe kilichobeba chai kinastahili vijiko vingapi? Kwa hiyo, hebu angalia Magu, Mji wa Kisesa unastahili kuwekewa fedha tofauti ili kuuboresha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kabila hauna barabara, yaani kwa kweli unafika mahali mpaka unakosa majibu. Mji wa Mahaha, Mji wa Nyanguge, Mji wa Lugeye, Mji wa Ilungu, Mheshimiwa Mchengerwa, vipi haya maneno? Bunge hili ndilo linaloishauri Serikali kuongeza fedha za *TARURA*. Ninaomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwenye *TARURA* lazima ziwekwe fedha za dharura. Mimi nina barabara ya kutoka Kisesa kwenda Kayenze, haipitiki na ndiko Shule ya Mkoa imejengwa. Hata leo kama kuna Mheshimiwa Waziri au Rais anataka kwenda kule, hawezi kufika. Nimeomba hela za dharura sipewi, aah, hivi niseme nini sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si huwa tunaandika shilingi? Naandika hapa shilingi halafu naondoka kwenda Dar es Salaam, mtanifuata huko Dar es Salaam ili kuifuata hiyo shilingi. Tufike hapo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tufike hapo. Haiwezekani watu wanazungumza maneno…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, ahsante sana, na hoja yako imechukuliwa na Waziri. Namwita Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, jiandae Mheshimiwa Dkt. Chaya. *(Kicheko)*

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Vilevile namshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya ndani na nje ya mipaka ya Taifa letu la Tanzania, hongera sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza tena Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi ambayo nimesema ni kubwa. Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan amegusa maeneo yote ambayo ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu. Amegusa kwenye eneo la elimu, afya, miundombinu ya barabara, maji, ambayo tunaambiwa bila maji hakuna maisha, maji ni uhai; haya maeneo yote ameyafikia kwa kiwango kikubwa sana. Tuna kila sababu ya kumpongeza mama kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nawapa pole Watanzania kwa kadhia kubwa iliyotokea ndani ya Taifa letu kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Mvua zimenyesha nyingi kila kona na hatimaye kuharibu miundombinu ya barabara kwa kiwango kikubwa ambapo miundombinu hii ilikuwa imetengenezwa sehemu nyingi. Pole sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu. Poleni sana kwa sababu, hii ni kazi ambayo inabidi muifanye baada ya kumalizika kwa mvua hizi nyingi zinazonyesha. Mheshimiwa Mchengerwa, binafsi nakupa pole sana kwa mafuriko yaliyotokea kwenye Jimbo lako la Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Jimbo la Rufiji pamoja na maeneo mengine ni mbaya, haijawahi kutokea. Kwa mfano, ukienda kwenye Mkoa wetu wa Lindi, na hapa ninatumia fursa hii kuwapa pole kwa mafuriko wananchi wa Mkoa wa Lindi katika majimbo yote na hasa Manispaa ambayo ina Majimbo mawili; Jimbo la Lindi Mjini na Jimbo la Mchinga ambalo ndilo Jimbo langu.

Katika Jimbo la Mchinga watu wawili wamepoteza maisha wakiwa wanavuka kutoka eneo la *Mchinga One* kwenda Mchinga Mbili na tayari wamezikwa. Tuwaombee kila heri Mwenyezi Mungu awapumzishe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitachangia katika maeneo makubwa matatu; eneo la elimu, eneo la afya pamoja na kwenye miundombinu ya barabara. Tunajua na tunaamini kwamba elimu ni haki ya mwanadamu, elimu ni haki ya mtoto wa Kitanzania, na bila elimu hakuna chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka mtambue ya kwamba kiongozi wetu ndani ya imani yetu alipoambiwa aongoze waumini wa Kiislamu, Nabii Muhammad *(S.A.W.)* alipopewa Mamlaka na Mwenyezi Mungu alisema mimi sijui kusoma. Mwenyezi Mungu akamwambia hapana, utaweza tu, nitakufanya ujue na kitu cha kwanza akamteremshia ile aya *Iqra Bismi Rabbika Alladzi Khalaq,* yaani ni kwamba, nenda soma kokote uendako, soma mpaka China uitafute elimu na elimu hii utakayoitafuta siyo elimu ya dini tu, bali elimu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini maana yake? Ni kuonesha umuhimu wa elimu kwa mwanadamu na Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan kwenye hili akasema lazima nihakikishe kwamba watoto wa kitanzania wanapata elimu, akaondoa ada. Baada ya kuondoa ada, sasa hivi elimu ni bure kuanzia awali mpaka kidato cha sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kule vyuo vikuu ina maana kwamba, wameongezewa viwango na watoto wengi sasa hivi wanasoma kwa kupitia mikopo ambayo Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan anaitoa. Tunampongeza sana. Kabla ya hapo wanafunzi walikuwa 425,713, lakini sasa hivi wameongezeka zaidi hadi kufikia 156%, hiki ni kiwango kikubwa sana. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo ya kwenye eneo la elimu, sasa naenda kwenye jimbo langu. Jimbo la Mchinga lina shule za sekondari zipatazo 12, mahitaji ya walimu ni 198, lakini walimu waliopo ni 102 ambapo upungufu ni walimu 96. Mheshimiwa Rais ameonesha jitihada kubwa kwa kutoa vibali vya ajira kwenye eneo la elimu na afya, lakini bado kiasi hicho ni kidogo sana kwa kuzingatia changamoto iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, pindi ajira zitakapoongezwa, vibali vitakapotolewa, Jimbo la Mchinga ambalo lina upungufu mkubwa wa walimu lifikiriwe tena. Kwa upande wa shule za msingi, walimu waliopo ni 237, upungufu ni walimu 162 na shule zilizopo ni 43. Kwa hiyo, tunaomba nalo hili mtufikirie kwa mapana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna suala zima la afya. Kwenye afya nako tuna upungufu mkubwa, tena makubwa sana. Tunahitaji tupatiwe watalamu kwa ajili ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa narudi tena nyuma. Kwa mfano, kule kwenye shule za msingi nataja shule moja tu, Shule ya Kilolambwani, ina mwalimu mmoja tu na Mheshimiwa Ndejembi wakati akiwa Naibu Waziri alifika pale. Kwa hiyo, tunaomba tuangaliwe kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niongelee masuala ya kiutawala. Jimbo la Mchinga tulikuwa kwenye Halmashauri ya Lindi Vijijini, tukaondolewa kutoka Lindi vijijini tukapelekwa Manispaa. Kwa hiyo, tunapoondolewa kutoka vijijini kupelekwa manispaa, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri ni kuangalia maslahi ya watumishi wanaobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kilichotokea ni maslahi yale ambayo ilikuwa wawapatie Jimbo la Mchinga ambalo lilikuwa Mtama, mpaka leo bado wanapeleka Mtama. Stahiki za watumishi zinaenda Mtama. Ina maana mpaka leo hawajalipwa, hata pesa za uhamisho zinakwenda Mtama, *OC* zinakwenda Mtama na bado

kama manispaa, wanapewa kiwango kile kile walichokuwa wakipewa kabla ya Jimbo la Mchinga kuhamishiwa Manispaa. Naomba hili liangaliwe. Ninashauri zile stahiki zote wapatiwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, pesa ambazo zinatakiwa zije manispaa kuanzia sasa, mara baada ya kuhitimisha hii bajeti, Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri mahiri, Waziri Msikivu, Waziri unayejali maslahi ya wananchi, wako unaowaongoza, tunaomba zije manispaa badala ya kwenda eneo lingine. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Salma hiyo ni kengele ya pili. Mheshimiwa Dkt. Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi. Kipekee namshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, hususan kule kwetu Manyoni, kuna miradi mingi sana imefanyika, nadhani nikiitaja naweza nikatumia muda wangu wote, lakini nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Sisi watu wa Manyoni tunamuahidi mwakani kwenye Uchaguzi Mkuu, kura atazipata za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namshukuru Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia nawashukuru na ninawapongeza Manaibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Dugange pamoja na dada yangu hapo Mheshimiwa Katimba kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza timu yote ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kweli huwa inatupatia ushirikiano mkubwa sana. Kule upande wa elimu, Dkt. Msonde, upande wa afya na hata Serikali za Mitaa, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa

Mchengerwa umewa-*shape* vizuri watu wako, kwa kweli wanatupa msaada mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maeneo manne ninayopenda kuchangia kama muda utaruhusu. Nitachangia upande wa *TARURA,* maboma, upungufu wa watumishi na muda ukiniruhusu nitachangia kuhusu kikokotoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TARURA,* naipongeza sana Ofisi ya *TARURA* pia TAMISEMI kwa ujumla wake wamefanya mambo makubwa sana. Kulikuwa kuna madaraja sugu, tangu uhuru hayajawahi kujengwa. Daraja la Chikola walitoa shilingi milioni 300, limeshajengwa. Daraja la Ntumbi wametoa shilingi milioni 500 na tayari mkandarasi amepatikana, wiki ijayo anaenda kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna daraja la Ngonjigwe lilijengwa mwaka 2017, likaanguka, lakini wametoa shilingi milioni 450, mkandarasi ameshapatikana na wiki ijayo anaenda kuanza kazi. Haya ni mafanikio makubwa sana. Haya ni madaraja ya kihistoria ambayo wananchi walikuwa wakipiga kelele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Mchengerwa, na kipekee namshukuru Rais kwa kuona kwamba anawajali wananchi wa vijijini ambao wengi wao ni wakulima. Nina ombi moja kwa Mheshimiwa Mchengerwa. Mheshimiwa Rais alipokuja Manyoni mwaka 2023, tulimwomba atuongezee mtandao wa barabara za lami kilometa 10 pale Manyoni. Nakumbuka Mheshimiwa Rais aliwaagiza kwamba, nendeni mkalifanyie kazi. Mheshimiwa Waziri naomba hili utusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manyoni ni kitovu sasa hivi, ni eneo ambalo kimsingi Dodoma inapumulia Manyoni. Tuna uwekezaji mkubwa sana pale wa Korosho. Kwa hiyo, Manyoni inakua sana, lakini barabara zetu nyingi za mtaa ni za vumbi. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri na kwa sababu Mheshimiwa Rais alitamka pale,

wananchi wananiuliza sana, mbona Rais alitamka! Alimwagiza Waziri, mbona hatuoni kinachoendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tuna barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Singida na Dodoma, barabara ya Kintinku – Makanda, inaenda Wilaya ya Chemba na inaenda Wilaya ya Kondoa. Hii barabara ipo *TARURA,* lakini kimsingi hii barabara inatakiwa ihamie *TANROADS*. Tulishapeleka hili ombi kule kwenye *RCC* na niliambiwa kwamba tayari mchakato unaendelea. Namwomba Mheshimiwa Waziri vilevile hili alichukue, kwani hii barabara ni ya muhimu sana kwa sababu inaunganisha hii mikoa miwili; Mkoa wa Dodoma na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusu maboma. Wenzangu wengi wameongea, nami nisemee hasa hasa maboma ya elimu na upande wa afya. Tumehamasisha sana wananchi kujenga na kusimamisha haya maboma, lakini sasa kasi ya kuyakamilisha imekuwa ndogo sana. Mheshimiwa Mchengerwa mimi nakuamini sana na niliwahi kukutabiria kwamba utakuja kuhamia TAMISEMI. Suala la maboma haliwezi kukushinda. Kama uliweza kufanya vizuri sana kwenye Wizara nyingine; Utumishi na Michezo, maboma hayawezi kukushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za msingi na sekondari pekee yake, tuna maboma zaidi ya 70 Manyoni. Upande wa afya tuna maboma zaidi ya 10 Manyoni. Haya ni maboma ambayo wananchi walijichangisha hela zao mfukoni, wakajenga haya maboma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji fedha ya dharura kama tulivyofanya kwenye barabara. Namshauri Mheshimiwa Waziri, apeleka fedha ya dharura, akamilishe haya maboma kabla ya uchaguzi wa mwakani. Wananchi watatuuliza kwamba mlituhamasisha tujenge haya maboma, lakini hamjayakamilisha. Kuna maboma yangu yana miaka minne sasa hivi, mengine yana miaka mitano sasa hivi, kwa kweli nashauri hili tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna shule kongwe na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, mimi kule kwangu tumejenga shule kongwe takribani tatu, lakini kuna shule kongwe nyingine tatu zina hali mbaya sana na hizi shule zilijengwa kwa tope. Kwa mfano, Shule ya Msingi Iseke, Shule ya Msingi Mbola, Shule ya Msingi Sasajira na Shule ya Msingi Udimaa. Najua kuna mpango ule wa shule kongwe, Mheshimiwa Waziri naomba vilevile uendelea kuziangalia hizi shule ili wananchi hawa waendelee kuwa na imani na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni kuhusu upungufu wa watumishi. Kwa upande wa Manyoni upungufu wa watumishi wa afya kwa ujumla wake ni 50.9%. Kwa upande wa elimu, upungufu wa watumishi upande wa sekondari ni 24.5% na upande wa shule za msingi ni 45%. Tumejenga shule nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu nimesajili shule za msingi mpya 19, lakini kata zangu zote sasa hivi zina shule za sekondari. Alipoingia Mheshimiwa Rais Mama Samia, nilikuwa na kata tano hazina sekondari. Tuliweza kujenga shule katika hizo kata tano zote ndani ya mwaka mmoja. Kwa hiyo, kata zangu zote zina shule za sekondari na tayari nimeanza kuongeza kata nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Kata ya Manyoni tumejenga sekondari mbili na tuna mpango wa kujenga tena shule nyingine ya sekondari kwenye Tarafa ya Kintinku na tumeshaweka miundombinu. Mheshimiwa Waziri wewe ni mbunifu, weka nguvu kwenye watumishi sasa hivi ili manung'uniko ya wananchi kwamba, walimu hawapo tuna majengo mazuri, tuna maabara nzuri hayo yaondoke. Hilo niliona nikushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kikokotoo. Bahati nzuri mimi nilikuwa mtumishi wa umma, lakini nilistaafu mapema nikaingia huku kwenye siasa. Inawezekana nami ningekuwa huko nje, ningekuwa na hiki kilio cha kikokotoo. Wazo la kuhamisha kikokotoo cha 50% kwa 50% kupeleka 67% kwa 33% lilikuwa wazo jema, lakini

niseme inawezekana hatukulifanyia utafiti mzuri, hatukuangalia *expectations* za watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosumbua sasa hivi ni *expectations.* Mtu alisha-*set expectations* zake kwamba nikistaafu nitapewa labda *50% of 100 million. All of the sudden,* anaambiwa kwamba utapewa *33% out of hundred*. Tayari hiyo ndiyo shida. Kwa hiyo, kinachosumbua hapa ni *expectations.* Sasa tunawezaje ku-*manage expectations* za wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali na bahati nzuri Mheshimiwa Mchengerwa watumishi wengi wapo upande wako. Walimu na watu wa afya wamenituma nikwambie umshauri Waziri wa Utumishi, uliangalie upya suala la kikokotoo. *It is an ideal* kama tutarudisha *50/50. It is a difference* ya *seventeen only. Seventeen* kwa Serikali siyo *issue.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimemsikia Katibu Mkuu wangu wa CCM ameliongelea, ni suala ambalo nadhani linapigiwa kelele. Nashauri tuangalie ni kitu gani tutakiweka ku-*motivate* watumishi wetu? Turudi kwenye *drawing table,* tufanye utafiti wa kutosha ili tuone kwamba ni njia ipi itakuwa bora ya kusaidia wazee wetu wanapostaafu pia tu-*meet expectations* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Kituo cha Afya cha Nkonko hakina gari la wagonjwa. Ni kituo ambacho kimsingi kipo mbali sana. Juzi hapa ulinipa Kituo cha Afya, tutakipeleka Tarafa ya Kintinku. Tunaomba utusaidie gari la wagonjwa la Kituo cha Afya cha Nkonko, lililopo limeharibika. Kwa hiyo, tunakuomba na niliongea na Mheshimiwa Dkt. Dugange akaniahidi kwamba atanipa gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Nkonko, nawe upo hapa leo, basi naomba mnisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakupongeza sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Njalu Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Sekiboko na Mheshimiwa Tarimba ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya TAMISEMI, ambayo imebeba maudhui ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana na wasaidizi wake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameweza kuifanya pamoja na watumishi wa Serikali za Mitaa kule mikoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru TAMISEMI kwa kazi kubwa na utafiti mzuri ambao wameufanya kwa kuanzisha halmashauri 10 za kimfano, kutoa 10% ya vijana, wenye ulemavu na akina mama, Halmashauri yangu ya Itilima ikiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kusema kwamba, hatutawaangusha, tutasimama vizuri kuwasimamia Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha kwamba, azma ya Serikali ya Awamu ya Sita tunaisimamia vizuri ili kuwa mfano kwa wilaya nyingine na mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kila Bunge tukija tunazungumzia maendeleo kwa wananchi. Moja ya maendeleo ni kuhakikisha kwamba kila Mbunge na kila Serikali na kila tunapoandika Ilani ya Uchaguzi, tunazungumza tutafanya nini? Tumefanya mambo mengi. Tumejenga vituo vya afya, zahanati, hospitali na vifaa vimeletwa katika maeneo yetu. Changamoto kubwa, hatuna watumishi wa idara ya afya kwenye maeneo yetu na vile vifaa inafika mahali vinakuwa ni vifaa chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu Itilima kwenye sensa ya mwaka huu nina zaidi ya watu 430,000, lakini watumishi wa kada ya afya wapo 210, ni upungufu wa 76%. Tumeendelea kuongeza,

tumejenga zahanati, 10 zimefunguliwa na bado zahanati nne tunaendelea kuzikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tusipoangalia tutakuwa tunapoteza fedha za Serikali, vilevile na matarajio yetu ambayo tunayozungumza. Tusipofikia mahali pazuri, hatutafika mahali ambapo tunapatarajia, kwa sababu afya ni muhimu na ndiyo jambo la msingi duniani kote kuhakikisha kwamba tunaanza na afya halafu na mengine yanafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri mwenye dhamana aende kwenye utaratibu wa *D by D* na ikiwezekana kama Serikali imefika mahali inaona kuna ukakasi, basi halmashauri zirithishwe kuajiri watumishi wa afya ili wananchi waweze kupata huduma safi na bora kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya uanzishwaji wa TAMISEMI kwa maana ya *D by D,* ni mambo ambayo yako kisheria na yako kimsingi. Nilikuwa nikiangalia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, zaidi ya halmashauri 50 zimewekewa 20% ya mapato. Sasa ni changamoto kubwa sana pale tunapofanya kuziongezea halmashauri na tunahimiza wananchi wetu wazalishe mazao yenye kupata ushuru, lakini tunapeleka 20%. Jambo hili kidogo linakuwa ni gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri mwenye dhamana aangalie na atumie taratibu na bahati nzuri ni Mwanasheria msomi, aende kwenye sheria na utekelezaji wa majukumu. Tuachane na mambo ya kubuni, huwezi ukaweka 20% wakati sheria inasema 40%. Jambo hili haliwezekani. Haiwezekani Mbunge unazunguka, una makusanyo ya shilingi bilioni mbili unazungumza shilingi milioni 400 iende kwenye maendeleo na una vijiji 110 na kata 23. Jambo hili ni gumu, na utekelezaji wake ni mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, hili jambo aliangalie kwa mapana zaidi na

alitafakari. Twende kwenye kutekeleza kwa kusimamia sheria, taratibu, na misingi ya utawala bora kuliko haya mambo ya kuamka tu na kuandika 20% badala ya 40% au 60%. Kama mapato ya halmashauri ni madogo na matumizi yao yawe madogo, lakini fedha nyingi iende kwa wananchi kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *TARURA*. Najua Serikali ilitangaza mabadiliko ya hali ya hewa, tunajua hilo, lakini Serikali inapotoa taarifa kwa wananchi wake, lazima ijipange kuhakikisha maeneo ya muhimu yanapitika, lakini leo ni kilio cha nchi nzima. Namwomba tu mwenye dhamana ya TAMISEMI, haya yapo kwake, tunampa pole lakini kubwa zaidi tuna maeneo machache kwenye maeneo yetu ya kiuchumi yanahitaji fedha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina barabara ya kutoka Nanga kwenda Laini Mwaswale, nina barabara ya kutoka Lagangabilili kwenda Migato, kuna barabara ya kutoka Luguru kwenda Sawida, hizo barabara zikikatika Itilima haipitiki. Mwisho wa siku inaonekana tunachokizungumza humu ndani kila siku ni changamoto. Tunajua *TARURA* wanafanya kazi kubwa na nzuri sana, lakini sasa bila fedha hakuna kitakachokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea tu kusema kwamba, Mheshimiwa Waziri kule kwenye wilaya zetu, mipango tunaipanga vizuri sana na tunaamini kwamba ikifika kwenu ni kutekeleza na kutimiza. Changamoto tuliyonayo, mambo mengi yakifika kwenye meza yako Mheshimiwa Mchengerwa yanakwama na yakikwama unatengeneza mazingira ya matatizo. Mheshimiwa Kiswaga hapa amelizungumza jambo moja kwamba, hela mnatutumia zinaanza kukwama kwenye mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi ukishatumia hela tunaenda kutangaza kule kwamba fedha tumeshapata. Sasa ukienda *trip* nyingine huna majibu ya kusema kwa sababu fedha haijaonekana kwenye lile eneo. Naomba sana, jambo hili basi liishe liwe na mipaka yake. Kama fedha hazijawa tayari, hakuna sababu ya kutuletea

kwamba kuna fedha zimekuja na huku tunaenda kutangaza na fedha hazipo. Jambo hili kidogo linakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la watumishi wa afya ni janga la Kitaifa. Tumeenda kwenye msingi wa kurudia bima ya afya, sasa bima hii kama hakuna watumishi, wataenda kutibiwaje wananchi sasa kule kijijini? Mifano hii tupo humu ndani tunatoka katika mazingira mbalimbali. Naiomba Wizara ya TAMISEMI, ndiyo mama mlezi asimamie taratibu na sera ili kusudi mambo haya tuyakamilishe na mambo yaende vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sekiboko, jiandae Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata fursa ya kusimama kwenye Bunge lako Tukufu, kuweka mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu ya wananchi, Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya na kunijalia kusimama mbele yako hivi leo. Vilevile, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunaposema tunapongeza na kushukuru ni kwa sababu: kwanza, ametekeleza kazi nzuri ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi; pili, ameimarisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi tunaowawakilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna sababu ya kumung'unya maneno kwenye jambo hili. Kwa umri wangu nimeshuhudia hiki ni kipindi cha tatu cha utawala wa Marais. Ni kipindi pekee ambacho nimeshuhudia shule zinaota kama uyoga, ni kipindi pekee nimeshuhudia miundombinu inaenda kurekebishwa ndani ya muda mfupi pamoja na majanga ya mvua yanayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *la shukur Allah, la shukur nas* (tusipomshukuru mwanadamu mwenzetu tunayemuona kwa macho, itatuchukua muda sana kumshukuru Mungu ambaye hatumwoni kwa macho). Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na kuwapongeza pia Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, Manaibu Waziri wawili kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya TAMISEMI. Nampongeza sana mwana-UVCCM mwenzangu, Mheshimiwa Zainab Katimba kwa kupata uteuzi wa Rais na leo kukaa kwenye dawati la TAMISEMI kama Naibu Waziri wa TAMISEMI. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo upo kwenye maeneo makubwa mawili au matatu. La kwanza ni *Decentralization by Devolution (D by D)*. Ukiangalia utekelezaji wa miradi mbalimbali katika maeneo yetu ya utawala, sisi kama wawakilishi wa wananchi, ninaona kuna haja ya Serikali kufanya tathmini *(review)* kama kweli tunaenenda kulingana na *Decentralization by Devolution (D by D)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Ukiangalia kwenye Hotuba ya Kamati ya TAMISEMI, kwenye maoni, eneo la kwanza kabisa la Maoni ya Kamati, wanaelezea namna ambavyo hawaridhishwi na ukamilishaji wa maboma ya zahanati, maboma ya shule (madarasa) na hapo niongeze na maboma au majengo ya maabara na maktaba ya shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 niliwahi kusimama hapa wakati wa bajeti kama hivi, nikasema, kama tunataka kupata elimu bora, lazima tuangalie nyenzo muhimu za kupata hiyo elimu. Hatuwezi kuiacha kando maabara na maktaba katika kupata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia maboma katika maeneo mengi, bado wanafunzi wanasoma *theory,* wanasoma mambo ya kisayansi kwa kufikiria kwa kuangalia picha. *Alternative*

*to practical,* hakuna maabara zinazotosheleza wao kujifunza kwa vitendo. Sasa ili tuweze kunasuka kwenye eneo hilo, lazima Serikali iamue kwa mkakati wa dhati kuhakikisha kwamba majengo ya maabara na maboma ya madarasa yanakwenda kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia upande wa afya, tuna kituo cha afya ambacho kinafikiriwa kujengwa kwenye eneo la Pagwi kule Kilindi. Ukizungumzia Kilindi, ni wilaya ya mwisho kwa umbali kijiografia kutoka kwenye wilaya zote nane za Mkoa wa Tanga. Yenyewe iko pembeni, barabara hakuna, iko pembeni ambako inapakana na wilaya zingine kama Kiteto na Kilosa ambazo nazo huduma ziko mbali. Sasa namna ya kuwasaidia Kilindi ni kuwasaidia kupata kituo cha afya pale Pagwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Pagwi ambayo ipo zaidi ya kilometa 65 kutoka Songe kwenye Hospitali ya Wilaya, hakuna kituo cha afya wala zahanati. Hivi ninavyokwambia, mvua zinavyoendelea kunyesha, akina mama wanajifungulia barabarani. Ni kitu ambacho siyo cha kuambiwa, siyo *story,* ni jambo linatokea Kilindi Kata ya Pagwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwasaidia wale akina mama wa Kilindi, nimwombe sana Mheshimiwa Mchengerwa, afanye kusudi ku-*rescue* maisha ya watu wa Pagwi kwa kupeleka kituo cha afya, ama kukamilisha zahanati na kuipatia vifaa ambavyo wale akina mama, watoto na wazee wanaweza wakapata huduma hiyo badala ya kwenda kuihemea kule Songe yalipo Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inafanana na kule Lukozi. Jana hapa, Mheshimiwa Shangazi alikuwa anazungumzia ubovu wa barabara ya Magamba kutoka Lushoto kwenda Lukozi. Kituo cha afya kile wananchi wamesha-*mobilize* baadhi ya vifaa vya ujenzi, wameshapata eneo la kujenga, lakini uwezo wa wananchi kwenda kujenga moja kwa moja umekuwa mdogo. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali iangalie yale maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa na yako mbali

na huduma, basi yapewe kipaumbele ili wananchi waweze kupata huduma hiyo kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nikizungumzia hapo hapo kwenye *Decentralization by Devolution*, kuna kukatika kwa mawasiliano kutoka huku kwenye sera kwa maana ya Wizara nyingine, lakini kwenda kwenye *Regional Administration*, kwenye halmashauri na kadhalika. Kwa nini? Kwa sababu Sekretarieti zetu za kwenye mikoa pale kuna namna mawasiliano yanakatika kwenda kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, mwaka 2023 hapa tulipiga kelele sana tukasema, kwa sababu tunafahamu Serikali yetu inaajiri taratibu na hapa nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo tumetangaziwa zaidi ya ajira 46,000 zimemwagwa kwa ajili ya Watanzania. Sawa, lakini uwezo wa kuajiri vijana wote walioko kule vijijini waliosoma hasa wenye mafunzo ya elimu kutoka kwenye vyuo vyetu mbalimbali, kama Serikali hatuwezi kuwaajiri wote kwa mkupuo mmoja, *although* hawa walioko mtaani, ukiangalia takwimu za uhitaji wa walimu tunawahitaji wote na bado pengine wasitoshe katika upungufu wa walimu uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa ushauri hapo kwamba ni vizuri Serikali iandae mpango wa kutoa mwongozo watu kwenda kujitolea. Wale walimu waliohitimu wakajitolee huko ili Serikali inapokuwa inachukua walimu iwachukue walimu ambao wako *fresh*. Kwa nini? Hata chakula kinaliwa kikiwa cha moto. Ili chakula kiwe kizuri, hata kama umekosa kukila mara baada ya kupikwa, utakitafutia *hotpot* kihifadhiwe ili tu kiliwe kikiwa cha moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukasema hao walimu wanaojitolea wapelekwe huko, pawe na utaratibu maalum ili kuimarisha kwanza uwezo wao na wasiweze kusahau yale *materials* ambayo wamejifunza kwa ajili ya kwenda kufundisha watoto. Pili, muda huo huo tunakuwa tumefaidika na hao walimu waliokwenda kujitolea kwa sababu kwa namna moja ama nyingine, wamekwenda kupunguza upungufu wa walimu katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ya leo umelizungumza hapo, lakini nataka nikwambie, *Decentralization by Devolution* bado inahitaji tafakuri ya hali ya juu. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeshaandaa mpango. Ni Sera, wameshamaliza, watekelezaji ni wenye shule ambao ni halmashauri zetu, TAMISEMI. Wao wamekaa, tunawaona huko vijana wanahangaika kwenye boda boda, wanahangaika kwenye Mama Lishe, wanahangaika kwenye Machinga, vijana wenye *Degree* za Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna upungufu wa karibia asilimia 46 ya walimu kwenye shule zetu nchi nzima. Sasa hawa wangekuwa wamepelekwa wakajitolea huko kwa mpango maalumu, kwanza, kama alivyosema tumepunguza, lakini pili tungeendelea kukiweka chakula kiwe cha moto ili wakati wa kuliwa kisiwe na shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalize kwa kusema hivi, hii nchi ni yetu sote, wananchi walioko huko nje, wametutuma sisi kuja kuwawakilisha katika Bunge lao. Itapendeza sana kama yale ambayo tunayashauri kwa nia njema tukaona yanakwenda kutekelezwa na wananchi wanaiona tija ya kuwa na Wabunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili hiyo.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba, jiandaye Mheshimiwa Livingstone Joseph.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kulihutubia Taifa kutoka maeneo haya ya Bunge, nizungumze na wananchi wa Kinondoni nikiwa hapa. Kwanza, naomba nitamke mapema kabisa kwamba naunga

mkono hoja hii ya Waziri wa TAMISEMI, ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa na ninaomba Wabunge wenzangu tuweze kuipitisha kwa nguvu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022, Jimbo la Kinondoni lina watu 333,000. Ni Jimbo la 62 kati ya Majimbo 265 yaliyopo Tanzania kwa idadi ya watu kwa maana ya watu wengi. Pale tuna Kata 10 na wastani wake ina maana kwamba kila Kata ina watu 33,000. Ni watu wengi sana katika eneo moja dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaona kwamba, kwa kuwa tuko katika eneo moja ambalo ni dogo, lakini lenye Kata nyingi, na mahitaji ya elimu, afya, maji, usafi na mazingira, barabara, ustawi wa jamii, usalama wa watu pamoja na mifereji, kwa sababu eneo lile ni eneo ambalo karibu asilimia 60 hadi asilimia 70 ni maeneo ambayo hayajapimwa, ni *squatters*.

Mheshimiwa Naibu Spika Mheshimiwa Mchengerwa anafahamu kwa sababu naye ni mkazi wa Kinondoni, anajua shida tuliyonayo pale Mwananyamala kwenye kata zote kasoro kata moja. Kwa hali hii katika mkutano wangu na wana-CCM na wananchi tuliofanya mwisho wa mwezi uliopita, tulikuwa tunafanya tathmini ya jinsi gani tumeweza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 na tukaona kwamba Serikali imeweza kutusaidia kutekeleza miradi na mambo ambayo yanahusiana na ahadi ambazo tumezitoa pale Kinondoni kwa zaidi ya asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya kazi kubwa sana na hapa ni lazima nimpongeze Mheshimiwa Rais. Naipongeza TAMISEMI na wale wote ambao wamesababisha kwa mara ya kwanza katika jimbo lile kuweza kufanya miradi mingi sana. Naomba tu nitoe mifano michache, pale kwenye Kata za Kinondoni na Tandale, tangu nchi hii iumbwe haijawahi kuwa na ya sekondari. Watu 33,000 lakini hawana *secondary school*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia takwimu pale katika jimbo tuna *secondary schools* tisa, maana yake ni kwamba kila miaka sita katika Uhuru wa Taifa hili tumekuwa tukijenga shule moja, lakini nataka niwaambie Wanakinondoni na Watanzania kwamba, ndani ya kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wa Mheshimiwa Rais tumejenga shule mbili ambazo katika kipindi cha miaka 60 hakukuwa na shule kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kinondoni tuna shule ya sekondari ya ghorofa, Tandale tunajenga shule ya sekondari ya ghorofa na zote zimeshachukua wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Kata hiyo ya Kinondoni haijawahi kuwa na kituo cha afya wala zahanati kwa kipindi cha miaka 60. Kinondoni ndiyo inachukua jina la Jimbo, Kinondoni inachukua jina la Wilaya, lakini haikuwa na zahanati wala kituo cha afya. Mheshimiwa Rais ametujengea kituo cha kisasa, Waingereza wanakiita *State of the Art*, cha kisasa. Kituo cha afya cha kisasa na jengo la mama na mtoto la ghorofa moja lenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 linaenda kumalizika ndani ya mwezi huu. Hayo ni mambo ambayo nayazungumza tu kwa uchache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kubwa ambalo ni lazima tujivunie, tumeanzisha juhudi ya kuwa na *high school* na pale kwenye Kata ya Makumbusho, Makumbusho *Secondary School* tayari inafanyiwa utaratibu kugeuzwa iwe kidato cha tano na cha sita, kwa mara ya kwanza jimbo lile ambalo halikuwahi kuwa na *high school* linakwenda kuwa na *high school*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza tena Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga Mto Msimbazi. Hakika wananchi wanaumia sana maeneo ya Mto Msimbazi. Hata kule Jimboni kwa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye tunapakana naye, maeneo yale yanakwenda kuboreshwa. Kata ya Kigogo, Kata ya Mzimuni, Kata ya Magomeni zinakwenda kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza, ninavyolihutubia Taifa, tayari Serikali imeshalipa mafao kwa watu wanaopitiwa na ule mradi. Maana yake ni kwamba, kazi inaenda kuanza. Wale wanaojua ambao wanapita barabara ya lile daraja la Magomeni ambalo mvua zikiwa nyingi hapapitiki, tayari Serikali imeshafanya maamuzi, inakwenda kujenga daraja lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mengi ya kuzungumza. Nilikuwa naangalia hata mtandao wa barabara, Jimbo la Kinondoni lina mtandao wa barabara za lami kilometa 56. Sasa nilikuwa nikipiga hesabu, nikiangalia katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wetu, ina maana tulikuwa tunajenga nusu, yaani chini ya kilometa moja kwa mwaka. Ukiangalia tu kitakwimu, ndani ya uongozi wa Mama Samia Suluhu Hassan tumezigusa Kata tano katika kujenga barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kata nyingine ambazo zimebakia, kwa mfano, tunakwenda kujenga pale barabara ya Togo katika Kata ya Hananasif, barabara ya Mzee Kimaro au msikitini pale kwenye Kata ya Hananasif, maana yake ni kwamba Jimbo la Kinondoni linakwenda kujaa barabara mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili hata nikiangalia limenisukuma mimi kwenye kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo. Fedha zile nimezitumia kujenga kituo cha mionzi *(radiology centre)* na hivi ninavyozungumza tayari tumeshafunga *X-Ray Machine, Ultrasound Machine* na nimemwambia ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa twende kule tukaizundue kwa bashasha kabisa tuweze kuonesha kazi ambazo tumezifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia hii, unaona ni kwa jinsi gani dhamira ya Mama Samia Suluhu Hassan anaionesha kwa Watanzania. Ametukwamulia Jimbo la Kinondoni ambalo katika kipindi cha miaka 60 naweza kusema lilikuwa likisuasua. Leo hii sisi tunang'ara sana. Kama kuna watu ambao hawana macho, mimi ni mtu wa Mungu sana, ningependa niwaelekeze katika kitabu na safari hii siji na *Quran* nakuja na Biblia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaosoma Marko 8:18, waangalie Mathayo 13:13 -15; hebu tusome Marko. Marko anasema, "Mbona mna macho lakini mnashindwa kuona?" Kumbe Mungu aliona miaka mingi kwamba itatokea mijitu, unafanya kazi, wao wenyewe wana macho lakini hawaoni. Sasa, hao mafarisayo, mimi leo nataka niwaite hao kwenye Isaya 43:8. "Waleteni mbele watu ambao wana macho lakini hawaoni, wana masikio lakini hawasikii." Waleteni hapa tuwaambie, waje wakajifunze Kinondoni kumefanyika nini kwa Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumwa na Wanakinondoni, Mheshimiwa Mchengerwa nisikilize vizuri. Nimetumwa na wananchi wa Kinondoni nije niseme na nitamke, Kinondoni tunakwenda na Mama Samia Suluhu Hassan. Fanyeni dhihaka zenu, tukaneni, lakini nataka niwaambie sisi tumeiona thamani ya Mama Samia Suluhu Hassan. Mungu amweke na ampe uzima na faraja tele, atende kazi aje awatumikie wananchi wa Tanzania. Hii ni ibada kwake, hii ni ibada kwako Mama Samia unawatumikia binadamu wenzako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema yafuatayo: Jiji la Dar es Salaam pamoja na pale Kinondoni, nimesema maeneo mengi sana ni *squatters*. Naomba nimshauri ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa, Dar es Salaam inachukua uchumi karibu asilimia 80, lakini kila ukienda kwenye jimbo lolote naamini utakuta *squatters*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyokuwa Diwani pale Hananasif, tulifanya kitu kimoja kwa mara ya kwanza Tanzania, *squatters* tulipapima na tukatoa Hati na pale tukatengeneza na mifereji na tukatengeneza barabara. Maana yake ukipima *squatters* unaweza ukawapelekea wananchi wanaoishi katika maeneo yao utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nawaomba TAMISEMI twendeni tukapime katika maeneo ya Kinondoni, Kata ya Makumbusho, Kata ya Kigogo, Kata ya Tandale, Magomeni,

Ndugumbi, Mwananyamala, Kijitonyama na Mzimuni, kule kwenye *squatters* mtatuondelea shida ya wananchi kuweza kupata matatizo. Ninaanimi Dar es Salaam ikitengenezwa itakuwa na uwezo mzuri wa ku-*produce* zaidi na kulisaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, najua unisaidie kwamba kuna suala linalohusiana na mito midogo midogo. Naomba hili niliseme kwa fadia ya Watanzania kuhusu mafuriko.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba, muda wako umekwisha.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia dakika moja au chini ya dakika moja. Nakuomba Mheshimiwa Waziri uruhusu wataalam wako wa TAMISEMI waende katika Kata za Mzimuni....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba utaratibu unamwandikia Waziri au unamfuata unamwambia, kwa sababu unachukua muda wa mtu mwingine sasa.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi naunga mkono hoja na nakushukuru sana.

*Usikasirike sana, najua tarehe 20 ndivyo utaratibu utakavyokuwa.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge.]**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Livingstone Joseph, ajiandae Mheshimiwa Leah.

Hiyo kauli ya mwisho inaondolewa kwenye *Hansard.* *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Livingstone, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu ni wa wote wala siyo wa kwao pekee yao. Kwa hiyo, kwa kuwa Mungu ni wa wote, watashuhudia tofauti na wanavyofikiri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais inayoshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa. Kabla ya kuzungumza, nataka nitoe pole kwa wananchi wa Kata ya Nghambaku katika Kijiji cha Ndogowe katika Kitongoji cha Ihimbwa ambapo asubuhi ya leo ndovu wameua wananchi wenzetu wawili. Hizi taarifa nimepewa na Mzee Paselela, nami nawapa pole sana, Mwenyezi Mungu awaweke mahali panapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Wizara hii ina viongozi shupavu akiwemo Waziri pamoja na timu yake yote, nami nataka niwape hongera kabisa kwa kazi nzuri ambayo mnafanya. Hata huu ushauri ambao tunatoa, tuna hakika kwamba mkiuzingatia mtakwenda kufanya kazi nzuri zaidi ya hii ambayo mmeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya Sensa ya Watu na Makazi, kuna tatizo kidogo kwa Maafisa Mipango. Kumbe Sensa ilikuwa ya nini? Maana yake ukishajua kwamba Kata ya Mvumi Misheni ina watu 19,000 au Kata ya Makang'wa ina watu 8,000 au Kata ya Manda ina watu 19,000, mipango yako lazima ielekee kuwapa wale watu huduma kulingana na idadi yao. Ni lazima uangalie kituo cha afya kilichopo pale kama kina-*cover* huduma za watu 19,000. Maji yanayopatikana pale kama yanakidhi watu 19,000. Barabara inayopita eneo hilo kama inaweza kusaidia watu 19,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maana ya kufanya Sensa maana yake ni mipango yetu ya maendeleo iende ikawiane na Sensa ya Watu na Makazi ambao tumewahesabu. Sasa, tulipokuwa tunafanya kampeni kuisaidia Serikali ili watu wajitokeze, Waheshimiwa Wabunge wote tulikwenda kuwaambia watu

jitokezeni mhesabiwe ili kuipa urahisi Serikali wakati wa kupanga maendeleo ipange kulingana na idadi yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamejitokeza wameshahesabiwa, lakini kila wakiangalia hawaoni mipango inayowagusa moja kwa moja kutokana na takwimu zao walizoandikishwa pale. Hii maana yake mnatupatia ugumu wa sensa inayofuata. Kwa sababu, ukishawaheshabu watu unajua baada ya miaka miwili kutokana na *speed* ya kuzaliana, hawa watu watakuwa idadi kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishawahesabu watu, lazima ujue baada ya miaka mitano watakuwa watu kadhaa. Kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali yetu ikajielekeza kwenye idadi ya watu na hii itaondoa upendeleo. Kwa sababu tunaona kuna baadhi ya maeneo yana watu wachache, lakini yana huduma zote muhimu zinazotakiwa, kuna maeneo yana watu wengi, lakini yana huduma kidogo, sasa hii si sawa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii, na ninashukuru kwa mchango wa Mheshimiwa Mbunge. Ninamtaarifu tu kwamba matokeo ya sensa yametoka rasmi mwaka 2023 na yanaendelea kwa maana ya kuanza kuchapishwa na yanaendelea kuchapishwa. Hapa tunapozungumza lakini Wizara zote ambazo zinawasilisha bajeti hapa, bajeti zao kuanzia mwaka huu na mpango wa maendeleo umezingatia takwimu za sensa tuliyoifanya mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nibu Spika, kwa hiyo, hoja yake ni ya msingi na ninamhakikishia kwamba tumelizingatia hilo katika bajeti ambazo tunaziwasilisha hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Sasa nataka tu nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, kuna Shule ya Msingi ina wanafunzi 1,200, Shule ya Msingi Igando ina wanafunzi 1,296 lakini kuna shule ambazo zimetia fora kama Shule ya Msingi Mpwayungu ina wanafunzi 1,550. Shule ya Msingi Manda ina wanafunzi 1,744. Kwa hiyo, kwa kuwa mmezingatia nina hakika, baada ya uzingativu wenu tutaona tofauti mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani tunazungumza habari ya watu wanaofanya kazi ya kujitolea. Kuna vichekesho vinatokea sana wakati wa kuomba ajira. Watoto wanaofanya kazi ya kujitolea katika kada za Ualimu na Afya wakienda kuomba kazi wakati ajira zimetangazwa, wanaambiwa njooni na viambatanisho vinavyoonesha mlikuwa mnajitolea wapi? Matokeo yake kwa sababu nchi yetu ina wajanja wengi, kila anayeomba kazi anakwenda na viambatanisho, wengine wanakwenda navyo *fake*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna haja gani ya kumwambia njoo na viambatanisho wakati anapojitolea mkurugenzi anajua? Kwa nini vile viambatanisho vyake mkurugenzi asivipeleke yeye TAMISEMI kuwatambulisha kwamba katika halmashauri yetu wanaojitolea wako kadhaa badala ya kuwaomba wale wanaoomba ajira? TAMISEMI si inayo orodha yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapojitolea mkurugenzi anajua, wakiomba ajira anasema njoo na kiambatanisho, kutoka wapi tena wakati wewe mkurugenzi unajua kwamba mimi najitolea hapa? Kwa utaratibu huo, watoto wengi wanaachwa. Mimi nilikuwa nataka nitolee mfano hapa, kuna Mwenyekiti mmoja wa Tawi la CCM Muungano anaitwa Naoel Ndalu, anauza zabibu hapa mjini kwa kutumia mabega kubeba. Amemsomesha kijana wake mpaka

amehitimu kozi ya udaktari, akaja kujitolea kijijini watu wote wanaona, mkurugenzi anaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetoka ajira, Arnold akaomba ajira pale, akaambiwa lete barua zako za kujitolea, kapeleka. Kutoka majibu, hayumo, kijana yule kahangaika kaenda JKT, sasa hivi karibu anamaliza JKT miaka mitatu ya kujitolea, nayo vilevile ajira bado tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu mzee anayeuza zabibu ambaye wananchi wote pale kijijini wanamwona, wanamwona ni Mwenyekiti wa chama, wanamwona anabeba zabibu kwa kutumia mabega, wanaona mtoto wake namna anakosa kazi na alikuwa yupo pale kijijini, watakuwa na moyo gani tena wa kuendelea kujitolea kusomesha watoto wao? Bora tungefanya mpango basi hata wa kuonekana wale watu ambao wanajituma, wanaonekana wanafanya kazi zao waonekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kujituma kwa Mheshimiwa Mchengerwa katika kazi na tunafahamu kwamba ameleta nidhamu kubwa na hii inatakiwa iendelee, kwa sababu kuna baadhi ya watu wamekuwa mchwa badala ya kuleta maendeleo, wanatafuna hela za watu. Tukushukuru sana, pesa uliyotupa kwa ajili ya kujenga Daraja la Chinugulu inaendelea kufanya kazi na pale wananchi wanafurahia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Manda limejengwa na tutaomba Mheshimiwa Waziri aende akalitembelee ili tuone uimara na ubora wa lile daraja. Daraja la Mlowa Barabarani ambalo nimekuwa nikilisema sana hapa, ametupatia pesa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, nalo vilevile limeanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Mchengerwa na Wizara yake kwa sababu wanasimamia *discipline* ya watumishi. Tunaomba kwenye baadhi ya maeneo ambayo yana mlundikano wa wanafunzi wengi, watusaidie, hizi shule za ghorofa

siyo lazima zijengwe mjini tu, zinaweza kujengwa hata vijijini kutokana na idadi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wakiwa wengi, hatuwezi kujenga madarasa mtawanyiko yakazagaa kila sehemu, baadaye tutaonekana tuna matumizi mabaya ya ardhi. Kuna wanafunzi 1,700 na kitu, kuna sababu gani hapa ya kujenga tena shule ya kuendelea kutawanya? Weka ghorofa hata kijijini watu wasome wakiwa wapo hewani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanalalamika. Nimeona kuna baadhi ya wachambuzi wanachekesha, wanasema watu wanamtaja sana Mheshimiwa Dkt. Samia badala ya kutaja kazi zilizofanyika, lakini ukikaa kwenye mpira unaona wanamtaja sana Chama, wanamtaja Pacôme. Sasa mtu unayemtaja si mwenye mpira? Mtu anayemiliki mpira ndiyo anatajwa sana. Mheshimiwa Dkt. Samia anamiliki mpira wa maendeleo katika nchi hii ndiyo maana tunamtaja sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wewe utakuwaje unasema tu wanakwenda Yanga, wanakwenda Yanga bila kutaja mwenye mpira nani? Wanakwenda Simba, wanakwenda bila kumtaja mwenye mpira! Unasema wanakwenda Simba anakwenda Chama, wanakwenda Yanga anakwenda Aziz Ki. Kwa hiyo, tunamtaja kwa sababu vitu anavyotufanyia ndugu zangu, sisi ni Wabunge miaka 15 tumekuwa hapa, hatujaona Serikali ikishusha pesa kwa wananchi vijijini kama anavyofanya Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo mengine yote yanayotokea, tuendelee kumwombea Rais wetu, Mwenyezi Mungu ampe moyo wa subira, awe mvumilivu kwa sababu akitukanwa Mheshimiwa Rais, tumetukanwa sisi wote, limetukanwa Taifa. Kwa hiyo, habebi peke yake. Hii dhima ya matusi wanayomtukana Mheshimiwa Rais, hatukanwi peke yake, tunatukanwa sisi na tunamwambia Mheshimiwa Rais kwamba tupo pamoja naye, iwe katika shida iwe katika raha, au tabu, tumeamua tunakwenda naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siyo msomi sana wa *Quran* lakini tunaona namna Mtume, kiongozi wa umma wa waislamu alivyopata shida kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Alifika mahali mpaka alipigwa. Tumeona Yesu alivyopata shida. Sasa Mheshimiwa Dkt. Samia ni nani asiyapitie hayo? Naye ni binadamu. Kwa hiyo, kwa kazi kubwa anazozifanya ni lazima baadhi ya watu wenye roho za kutu watamzushia mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaambia hivi, wanapoteza muda bure. Mheshimiwa Rais, tutaendelea kumwombea na kumpigania na kumsemea kwamba shida anayopitia ni kwa ajili yetu, matusi anayotukanwa ni kwa ajili yetu. Kwa hiyo, hayupo peke yake, tupo pamoja naye wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Mheshimiwa Mchengerwa atutembelee katika Jimbo letu la Mvumi aone shughuli za maendeleo na upungufu tulionao atusaidie. Tunaomba kuna baadhi ya maeneo atuongezee huduma za msingi. Kwa mfano, ukiangalia Tarafa nzima ya Mvumi na idadi ya watu kutokana na Sensa na Makazi, pale tumeomba tuongezewe *ambulance* kwenye Kituo cha Afya cha Andali mtusaidie. Pale kuna watu wengi sana na kuna…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Lusinde, kengele ya pili imeshalia. Umetoa mifano mizuri ya Mheshimiwa Rais…

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nisije nikapotezwa. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Taletale na Mheshimiwa Mafuwe ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komanya, subiri kidogo. Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge ambao hawajachukua mchele kuwa zoezi la kugawa huo mchele linaendelea mpaka saa saba mchana na siku zimepita sana. Kwa hiyo, mnaombwa *by* saa saba mwende *basement* mkachukue mizigo yenu.

Mheshimiwa Komanya, endelea.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipatia nami niweze kutoa maoni yangu katika hoja iliyopo mbele yetu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa na manaibu wake na wataalamu wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kazi nzuri inayofanywa ya kutekeleza miradi katika maeneo yetu. Kipekee nampongeza na kumtia moyo Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maendeleo anayotupatia hususan ndani ya miaka mitatu, amefanya mabadiliko makubwa katika Jimbo la Meatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Meatu ya leo siyo sawa na ile ya 2020. Naomba nimtie moyo kwamba tupo pamoja naye na kawaida mti mzuri wenye matunda mazuri ndiyo hushambuliwa na mawe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais, haya yote yanafanyika kwako kwa sababu ya kazi nzuri unayoifanya. Wanataka wakudhoofishe urudi nyuma. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Meatu nakutia moyo, upo vizuri, tupo pamoja katika yote unayoyapitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze sasa katika hoja iliyopo mbele yetu. Mwaka huu tutakuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilivyowasilisha mbele yetu, lakini sambamba na hilo, tutakuwa na uboreshaji wa daftari la wapiga kura. Nilitaka tu nishauri, wakati wa uboreshaji wa daftari la wapiga kura, uende sambamba na kuongeza vituo vya kupigia kura katika maeneo ya pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani, katika Kata ya Bukundi mwananchi anatembea hadi kilometa 36 kwenda kwenye kituo

cha kupigia kura, anatembea kilometa 22, anatembea kilometa 15. Kule ndiyo kwenye wapiga kura ambao wanajitoa bila changamoto yoyote na wenyewe tuwape haki sawa ya kupiga kura kama Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maboma limeongelewa na Wabunge wengi. Kuhusu maboma, ilianza wakati wa mradi wa uendelezaji miradi katika Serikali za Mitaa. Wananchi walitakiwa kuchanga na kuanzisha maboma, kisha Serikali iweze kukamilisha, lakini mradi huu ulipokoma, maboma mengi yaliachwa. Hata tunapoongelea maboma haya, mengine ni zaidi ya miaka 10 na mengine yameanzishwa hapa karibuni wakiamini Serikali inaendelea kukamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Meatu katika vyumba vya madarasa tunavyo zaidi ya 100, zahanati zaidi ya 12 vyote ni nguvu za wananchi ambazo walianzisha wenyewe. Nilitaka kuishauri Serikali, pamoja na fedha inayoletwa kupitia tozo kwa kasi iliyopo, hatuwezi kuyakamilisha maboma haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuomba tutafute chanzo tuweze kukilinda ili tuweze kukamilisha maboma haya na mojawapo nilitaka kupendekeza fedha ile ya *property tax* ambayo ilikuwa inakusanywa na *TRA*, katika mwaka wa fedha ilipaswa kurudi halmashauri, lakini haijarudi mpaka ninavyoongea leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu iliyopita, mwaka uliopita 15% ilienda kununua pikipiki za Watendaji wa Kata. Naomba basi kwa mwaka huu zielekezwe katika ukamilishaji wa maboma kwa kuwa halmashauri hazijaanza kuzikusanya na siyo mapato tena ya *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mkurugenzi wa *TARURA*, *Engineer* Seff kwa kazi nzuri anayofanya pamoja na Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Simiyu na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Meatu, kwa kweli kwa ushirikiano wao wanaonipatia, tumeweza kutekeleza vizuri barabara kwa fedha tulizoletewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatie moyo kwa kazi nzuri wanazozifanya, nami Mbunge wa Jimbo la Meatu nipo pamoja nao, nasikiliza ushauri wao, lakini tuna changamoto ya Daraja la Mto Mwamanongu lenye urefu wa mita 120. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hili ni kero, limefanyiwa upembuzi yakinifu, fedha inayotakiwa kujenga pale ni shilingi bilioni saba na tayari tuliahidiwa shilingi bilioni 3.5 tuanze ujenzi wa daraja hilo. Daraja hilo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais akiomba kura akiwa mgombea mwenza. Ukiacha kuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, lina usumbufu mkubwa kwa sababu linakata mawasiliano kwa kata nne; linakata mawasiliano katikati ya Wilaya na kule pembezoni ukizingatia kata hizi zipo mbali na Makao Makuu ya Wilaya. Naomba basi mruhusu tuanze kulijenga ili tuondokane na hii adha tunayoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa vifaa tulivyopokea katika Kituo cha Afya Bukundi. Mimi Mbunge nimekabidhi *ambulance*, nimekabidhi vitanda na magodoro 15, mashuka 60, pamoja na kwamba tuliletewa pia kitanda na taa kwa ajili ya upasuaji. Kazi ni nzuri, wananchi wanamshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna anavyofanya kazi katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Wabunge wenzangu na Wizara ya TAMISEMI kwamba, kwa kuwa ajenda ya Mheshimiwa Rais ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na *ambulance* hizi tumeletewa tuweze kupambana na vifo vitokanavyo na uzazi, tusikubali kamwe mama mjamzito akaombwa mafuta pindi anapotakiwa kufuatwa ili tusiweze kufifisha hizi juhudi ambazo ni ajenda ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Jimbo la Meatu. Awamu ya Tano hatukuweza kupata kituo cha afya, Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Mama Samia, tumepata kituo cha afya kimoja. Bado tuna uhitaji mkubwa wa vituo vya afya katika Kata ya Ng'hoboko. Nilipendekeza tupewe pale kutokana na vijiji 12 vinavyoizunguka kata hiyo, kutokana na kwamba Chuo cha *VETA*

kinajengwa pale na shule ya sekondari kupandishwa hadhi kuwa ya kidato cha sita, hivyo kutakuwa na ongezeko la wanafunzi na pia ni sehemu ambapo itapita barabara kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tujenge kituo cha afya tupunguze msongamano katika Hospitali ya Wilaya. Vilevile napendekeza Zahanati ya Mwabuzo tuipandishe hadhi kwa sababu ni kilometa 45 kwenda Makao Makuu ya Wilaya na pale Mheshimiwa Rais katuletea mabweni mengi kwa sababu kuna ongezeko la wanafunzi kutoka 200 mpaka 880. Wasichana wametoka sehemu mbalimbali ya nchi yetu, kwa hiyo, kuna ongezeko kubwa sana la wanafunzi na kata nne zinazunguka pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia kituo cha afya. Mheshimiwa Dkt. Dugange unapafahamu kwa sababu ulikuwa *RMO* katika Mkoa wa Simiyu. Tunaomba tuongezewe *ambulance* mbili kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya na Kituo cha Afya Iramba Ndogo. Hospitali ya Wilaya hawana *ambulance*, zile tulizopewa tumepeleka katika Kituo cha Afya Bukundi, ambacho kina uhitaji mkubwa na kiko katika maeneo magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa sekondari mpya mbili tulizopewa; Mwamanima na Mwanuzi. Tumepunguza msongamano wa wanafunzi lakini tuna uhitaji wa sekondari mpya, Mbushi na Kata ya Kabondo. Nashukuru kwa Shule mpya ya Msingi moja ya *BOOST,* ambayo ni Shule ya Msingi Mwanuzi, lakini tunaomba shule kwa ajili ya Kijiji cha Magulya na Kijiji cha Maweni ambapo wananchi tayari wameanzisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu ameboresha shule ya wasichana Nyalanja kwa kuiletea mabweni mapya matano na madarasa 12, hivyo tukawa na mabweni saba. Kuna ongezeko kubwa la wanafunzi kutoka 200 mpaka 880 ukijumlisha pia ni shule ya kutwa, lakini kuna watumishi, kuna jamii pale sasa ya watu 800…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Leah…

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba uzio, jiko, bwalo pamoja na gari la wanafunzi ili tuweze kuwanusuru wale wanapoweza kubebwa na bodaboda…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah, ahsante.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taletale atafuatiwa na Mheshimiwa Mafuwe na Mheshimiwa Tumaini Magessa ajiandae.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa yale anayoyafanya kwenye nchi yetu na kubwa ni kwenye Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua dada yangu aliyekuwa jirani yangu wa hapa, Mheshimiwa Zainab Katimba, hongera sana na siti yetu imekuwa ina bahati ya watu kuhamia mbele. Naona Mheshimiwa Zainab Katimba uende ukamsaidie vizuri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niendelee kumpongeza kaka yangu, babu yangu Mheshimiwa Mchengerwa. Kwanza pole kwa yanayotokea Rufiji, lakini pia nakupa pole kwani naona leo mnasimama hapo bado una *drip* mkononi, bado ni mgonjwa. Hiyo ni kitu kikubwa sana unatuonesha kwamba punda afe mzigo ufike. Hongera sana Mheshimiwa Mchengerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama hapa mwaka 2022, nawe pia ulielekeza. Sisi watu wa Morogoro Vijijini na watu wa Morogoro Kusini Mashariki, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea huduma ya afya. Tuna vituo vya afya vya kutosha.

Ninavyozungumza leo hii, tumeletewa Kituo cha Afya kwenye Kata yetu ya Mkulazi kituo kipya, tuna Kituo cha Afya Kata ya Mikese na Kituo cha Afya Kata ya Mkuyuni, lakini hivi vituo vyote tulivyonavyo havina sehemu ya kuhifadhia maiti. Hii ni mbaya sana. Leo hii tukipata maiti Morogoro Kusini Mashariki lazima twende tukahifadhi Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani kwa kusema hivi. Mtu anaona mtu anakwenda ku-*rest in peace,* hapa ana-*rest* na *stress.* Tuongee ukweli, mtu umefiwa halafu bado utafute gari ya kwenda kuhifadhi maiti mjini! Siyo wote ambao wakifa wanazikwa hapo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mchengerwa, sisi Wanamorogoro Kusini Mashariki tunakukubali sana na tunaomba amfikishie salamu zetu Mheshimiwa Rais, amwambie Morogoro Vijijini, Morogoro Kusini Mashariki yeye alale usingizi mnono, sisi tunakwenda kumpa yeye 2025. Mheshimiwa Mchengerwa naomba nikwambie tunakupongeza kwa kutuletea gari la wagonjwa katika Kituo chetu cha Afya cha Mkuyuni, lakini pia unapopongezwa lazima uombwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kituo chetu cha Afya cha Ngerengere, tunavyozungumza tuna gari ya wagonjwa ambayo ina miaka 15 na imeshakufa. Kwa kifupi, hatuna gari ya wagonjwa. Kituo chetu cha Afya cha Ngerengere tunavyozungumza nawe Mheshimiwa Waziri, hatuna sehemu ya jengo la mama na mtoto. Katika Kituo cha Afya Ngerengere, Ngerengere ni kikubwa lakini ninavyozungumza hapa, akifa mtu lazima tupeleke maiti Morogoro Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii hakuna sehemu ya kupumzika ya mama na mtoto. Katika pongezi ninazokupa, mimi naomba Mheshimiwa Mchengerwa, wewe ni jirani yangu pale, nakuomba utenge muda uje Morogoro Kusini Mashariki. Tunajua tunakupenda sana maana nikimwomba Naibu Waziri wako, usije ukasema mengine. Nakuomba wewe Mheshimiwa Mchengerwa,

simtaki Mheshimiwa Katimba, nakuomba wewe uje Morogoro Kusini Mashariki uangalie kero zetu. Ikiwa sisi leo hii tunakuombea dua, ulilala, umeamka, upo kazini na *drip* yako mkononi, na unapiga mzigo wa Mama Samia, hongera sana, lakini ili upige mzigo vizuri, tunaomba uje utembee uone changamoto zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitengo cha afya, sisi tunaanza Kituo cha Afya cha Mikese ambacho kipo kwenye *Morogoro corridor*. Mpaka leo kituo hiki kinaonekana kama zahanati. Kituo cha Afya kimekamilika, lakini hatuna vifaatiba. Sasa tuangalie kwamba umetuletea vituo vya afya vya kutosha, lakini kama hatuna vifaatiba hivi ni vya nini? Tunakwenda kwenye kulia na iyena iyena ya Mama Samia, lakini tunataka tuwe na afya ili tuwe na afya tukamilishieni hivi vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho naomba nizungumze na niwape pongezi sana *TARURA*, amezungumza babu yangu pale wa kisukuma kwamba hawa *TARURA* tuwaongezee mfuko. Hawa *TARURA* wanafanya vizuri sana ila cha ajabu mimi kiukweli natamani kuiona lami Morogoro Vijijini. Kama *TARURA* wanaweza kuweka lami baadhi ya sehemu nyingine, wanashindwaje kutuletea lami sisi watu wa Morogoro Vijijini barabara za *TARURA*? Wanashindwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nampongeza na kumshukuru sana, sisi wakazi wa Kiloka, leo hii ametufungulia barabara ya Kiloka – Mfumbwe. Tuna changamoto *of course,* mvua ni janga kubwa hata yeye ni mhanga wa hizi mvua, nasi pia ni sehemu ya wahanga wa hizi mvua. Jana nilikuwa ninaongea na kaka yangu Mheshimiwa Innocent Kalogeris, kule Kidunda kwenye bwawa letu lile mvua imekuwa kubwa, sasa mamba wanatoka, wanatalii mtaani. Kwa hiyo, hivi ni vitu vya kawaida, pole lakini ni pole yetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba barabara ya *TARURA,* sisi watu wa vijijini tuna hali mbaya sana. Hizi mvua zimekwenda kuharibu miundombinu yote. Tunavyozungumza sasa hivi, mvua imesababisha kukatika kwa barabara na madaraja ambayo chini

yalikuwa yanapita mabomba yaliyokuwa yanatokea Morong'anya kuja Mikese. Leo hii Mikese haina maji kabisa kwa sababu madaraja yameharibika. Leo hii tunaendelea kuiombea *TARURA* ipate pesa ya kutosha iende ikamalize changamoto ambazo sisi Wanamorogoro Vijijini tunateseka nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kidogo kwenye suala la elimu. Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mchengerwa, kwanza nampongeza kwa kuniletea shule za sekondari za kutosha. Leo hii sisi wakazi wa Kata za Kidugalo, Kibuko pamoja na Tegetero tumepata Sekondari mpya, ila hizi haziwezi kuwa nzuri kama hakuna walimu. Tuna changamoto kuwa sana ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa Sekondari yetu mpya ya Kidugalo, imeshaisha, lakini wametuletea walimu watano na mpaka sasa hivi hawajaingia kazini. Sasa hatuji wapo wapi? Tuna Shule ya Sekondari pale Fulwe, sasa hivi tuna kidato cha kwanza, cha pili na cha tatu. Hata hivyo, hii shule hakuna hata jengo la walimu. Hii shule tunakwenda Kimungu Mungu wakati tunamwamini sifa zake Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapomwomba Mheshimiwa Waziri aje jimboni, nataka aje kututatulia changamoto ambazo sisi kama Wanamorogoro Kusini Mashariki ambao tumesema tunalia na Mama, jambo la Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia ni jambo letu. Maana yake yeye ni wa Mama Samia, ndiyo maana yuko hapo anatuwakilisha na anamwakilisha. Tunamwomba aje, Mikese ni kata kubwa, Mikese ni mjini. Leo hii wanafunzi wengi wanasoma katika Shule ya Fulwe pale Mikese, lakini hatuna madarasa. Sasa, ni nani wa kumlilia kama siyo wao TAMISEMI?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tukiangalia Kata yetu ya Kiloka ina shule ya sekondari, lakini wanafunzi wanatembea kilometa 18 kwenda, 18 kurudi. Wanafunzi hawa kweli ikifika kwenye matokeo ya kidato cha nne ni rahisi sana kufeli. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, tumetoa eneo tayari kwa ajili ya wao

kutujengea sekondari kwenye Kata yetu ya Kiloka. Tunawaomba wakiweza kutusaidia watusaidie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo sisi tunaliomba, sisi tunatokea kwenye halmashauri, Mheshimiwa Waziri tuna sekondari ambayo nimemwomba hata Mheshimiwa Waziri wa Elimu, sisi hatuna *VETA* kwetu. Naomba shule ya sekondari na ufundi kwetu. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, ameniahidi kwamba itawezekana, lakini ili liwezekane linawezekana kutoka kwake Mheshimiwa Mchengerwa. Watu wa Morogoro Vijijini tunataka shule ya sekondari na ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu hawawezi kutuletea *VETA* kwa utaratibu walioupanga wenyewe. Naomba hii shule ya sekondari na ufundi iende ikakae pale kwenye Tarafa ya Mkuyuni ili nami siku moja nikizeeka nione kumbukumbu yangu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili hiyo.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Magessa na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, anafanya kazi nzuri sana. Hongera kwake pamoja na Naibu Mawaziri wake. Ninampongeza dada yangu Mheshimiwa Zainab Katimba kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais. Kwa kweli ninawapongeza Mawaziri wote na Naibu Mawaziri wote wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, tunatembelea kwenye Majimbo mengi. Waheshimiwa Wabunge, ninachukua nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, wote mnafanya kazi kubwa mno inayoonekana. Kuna ile historia ya kuonesha *trend* kubwa ya Waheshimiwa Wabunge huwa wanabaki. Awamu hii tutavunja rekodi, Waheshimiwa Wabunge wengi watarudi kwa sababu Jemedari wetu Mama Samia Suluhu Hassan, hili ni Bunge lake, anafanya kazi kubwa mno na sisi tumepita huko tumeona. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge msiwe na mashaka, tunakwenda kubadilisha historia, wengi mtarudi humu, endeleeni kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwa utulivu kabisa. Wananchi wa Jimbo la Hai ambao waliteseka kwa miaka 15, leo wameniambia nisimame hapa niseme Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi kubwa mno. Haya nitakayoyazungumza hapa ni utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambapo utekelezaji wake unaanzia kule chini kwa Watendaji wa Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji, unakuja kwa Waheshimiwa Madiwani wa pale Hai, wanafanya kazi nzuri sana, na baadaye unakuja ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaye Jemedari wetu Mkuu wetu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mheshimiwa Nurdin Babu, huyu anafanya kazi kubwa sana. Kimsingi, ninawapongeza watumishi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wajibu wa kusema. Pale kwetu Hai sasa hivi tuna chuo kinajengwa cha Kikuletwa ambapo takribani shilingi bilioni 37 zimemwagwa pale. Ukienda pale Bomang'ombe sasa hivi kuna barabara za lami zilizojengwa vipande takribani 11, lami na taa juu. Sasa hivi pale Bomango'mbe ni kama Kinondoni. Kwa nini tusiseme Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na shida ya maji pale Bomang'ombe, ameleta shilingi bilioni 3.39, maji yanapatikana, na sasa hivi watu wanajenga Bomang'ombe. Mheshimiwa Rais,

ametuletea vituo vya afya, amekarabati Hospitali ya Wilaya ya Hai na ametuletea na magari. Kubwa zaidi Soko la Kwasadala, ndugu zangu, wote mnafahamu nilivyokuwa ninapiga kelele kuhusu Soko la Kwasadala, shilingi bilioni 11.2 ameshatutengea na hivyo tunakwenda kujenga Soko la Kwasadala la kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama kanuni zinaruhusu kuuliza nani kama Mheshimiwa Mama Samia? Niseme kwa kweli hakuna. Mheshimiwa Rais, anafanya kazi kubwa na nzuri sana. Kiwanda cha *Machine Tools* sasa hivi kinafanya kazi, Mheshimiwa Mama Samia ametusaidia kupata fedha hizi. Kwenye ushirika nimepiga kelele hapa, mambo yameanza kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hayo machache ambayo nimeyaeleza. Kwa sababu ya muda niseme. Tarehe 14 Aprili, saa nane usiku Wilaya ya Hai ilipata majanga ya mafuriko. Majanga haya yamesababisha uharibifu mkubwa sana. Ninavyozungumza sasa hivi, nyumba 26 watu hawana makazi. Hii ni kutokana na mifereji na mito kujaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Sanya, Mto Kikafu na Mto Weruweru yote imefurika. Kwa bahati mbaya sana hapa niliuliza kwenye swali langu asubuhi kwamba hatujui haya maji yanatokea wapi? Kuna haja ya Serikali kufanya *intervention,* lile daraja la kwa Msomali kila mwaka linavunjika, watu wanaathirika, wanapata shida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza sasa hivi, Kijiji cha *Sanya Station* kimeathirika katika miundombinu ya shule, barabara hazipitiki, Kikafu Chini, Chemka, Mronga na Mbwera kote huko ninakokuzungumza uharibifu umekuwa mkubwa sana na kusababisha Shule ya *Sanya Station* kuezuliwa, maji yamejaa ndani. Kule mabwawa ya Samaki, miundombinu, mashamba ya mbogamboga, mifugo, vitu vimeharibika na kwa kweli tuna hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimbebeshe Mheshimiwa Mchengerwa, ninajua watu wa *TARURA* wanafanya kazi kubwa sana. Hizi barabara ninazozitaja hapa kwa kweli peleka fedha haraka ili zikasaidie kuokoa hizi barabara. Kwa mfano, barabara ya Bomang'ombe – Kikafu imeharibika na haipitiki. Barabara ya Rundugai – Tindigani, barabara ya Mkalama – Kikafu, barabara ya Mkalama – Kikafu Chini, barabara Rundugai – Chemka, barabara ya Miembeni – Kware, barabara ya Mungushi – Kware, barabara ya Vijana – Marukeni, barabara ya *KNCU* kwenda Itunu, barabara ya Masama kwenda Mwinjuru kule Tema, barabara zote hizi nimwambie Mheshimiwa Mchengerwa hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi mnakula ndizi kutoka kule Hai, sasa hivi mtatoa wapi ilhali hizi barabara ndizo zinasafirisha mazao ya mboga mboga kutoka kule Mkalama? Kwa hiyo, naomba atusaidie kupeleka fedha haraka kwenye maeneo haya na kwa hati ya dharura. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama yupo hapa, wananchi hawana chakula kwa sababu mazao yameondoka. Tangu juzi ninaendelea kupambana hapa na Mkuu wangu wa Mkoa na *RAS,* hawajapelekewa chakula. Namwomba tafadhali, ikiwezekana leo usiku, ninamjua mama anavyonipenda na anavyotupenda watu wa Hai, naye ndiye mtu wa kwanza kushangilia nilipotangazwa kwa kwanza na akanipigia simu. Sasa nimwombe anisadie sana kupeleka vyakula na vifaa ili wale watu waweze kupata mahitaji yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais. Kwanza tunamshukuru Mheshimiwa Rais, mimi nadhani ni Mbunge wa kwanza ninayeongoza kwa kutembelewa na Mheshimiwa Rais mara nyingi, maana akishuka pale *KIA* kaingia Hai, nami ninahesabu amekuja zaidi ya mara kumi. Mheshimiwa Rais amekuja, Mheshimiwa Makamu wa Rais amekuja, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Sisi watu wa Hai tunajidai kweli kweli kwa sababu viongozi wetu wanatupenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa zipo ahadi ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi. Mheshimiwa Makamu wa Rais amekuja juzi amefanya mkutano, akaelekeza Serikali kwamba, hizi ahadi zitimizwe. Tuna barabara ya Bomang'ombe – Chekimaji – *TPC*. Hii barabara ni kero kubwa, lakini ndiyo barabara muhimu ambayo ni *diversion* ya Mkoa wa Kilimanjaro. Hii barabara ikijengwa inaenda kwenye utalii wa Kituo chetu cha Chemka, inaenda kwenye Chuo chetu cha Kikuletwa pale ambapo Mheshimiwa Rais ametupatia shilingi bilioni 37, inakwenda kuunganika na *TPC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Mchengerwa anisikilize kwenye hii barabara ambayo imeahidiwa, nami nikaenda kufanya mkutano nikawaambia wananchi kuwa fedha inakuja, na tukaja hapa tukapambana kwenye Kamati tukawaombea *TARURA* shilingi bilioni 360. Nina mashaka kama fedha zimekwenda. Anatikisa kichwa maana yake Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hajapeleka hizi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Waziri wa Fedha aje hapa atuambie, kwa nini hakupeleka zile shilingi bilioni 360 *TARURA* wakafanye kazi yao? Matokeo yake sisi anatutundika msalabani Waheshimiwa Wabunge wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda kule nikafanya mkutano mkubwa nikawaambia wananchi, mnajua Mheshimiwa Mama Samia anavyowapenda? Wakasema ndiyo. Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM alikuja hapa akaahidi barabara wakasema ndiyo, Mheshimiwa Makamu wa Rais ndiyo, kilometa saba tunaanza nazo, lakini mpaka leo hazijatangazwa. Hii haikubaliki. Tunaomba sana Wizara ya Fedha, na wale wadada wema kule, mimi huenda sana Wizara ya Fedha pale kufuatilia hili, na dada zangu wazuri wale wanavaa viatu virefu, naomba wahangaike kuleta hizi fedha zije watu wakajenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara nyingine ya Kwasadala – Uswaa, hii barabara iliahidiwa na Mheshimiwa Rais Hayati Benjamin William Mkapa. Juzi nilienda msibani pale

mchungaji alinionesha niangalie mti aliopanda Mheshimiwa Rais, Hayati Benjamin William Mkapa alipotuahidi barabara. Mti unakaribia kuzeeka ilhali Barabara ya Uswaa haijajengwa. Pale kwenye Bonde la Uroki wananchi wanapata shida kusafirisha mazao yao. Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ninaomba itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Barabara ya *KIA*, kutokana na mgogoro wa muda mrefu, wananchi wamekosa barabara. Naomba, hebu tekelezeni maagizo haya ya Mheshimiwa Rais pamoja na maagizo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais aliyosisitiza alipokuja juzi. Pia akaagiza, shule nyingi za Hai zilijengwa miaka mingi, wanapofanya tathmini pale TAMISEMI wao wanahesabu Hai kuna shule nyingi, lakini ni shule chakavu ambazo zimejengwa miaka 1952 na kuendelea, nyingi ni chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimpeleka andiko maalum kwa Mheshimiwa Waziri kumwonesha shule zilivyo na picha nikamwekea. Naomba tupate fedha maalum za ukarabati wa shule zetu. Tunamkushukuru ametuletea fedha nyingi lakini zinakuja kwenye ujenzi wa shule mpya, na hizi ambazo ni chakavu zilizo nyingi hazifanyiwi kazi ilhali zimechakaa sana. Ukienda pale katika Shule za Sekondari za Ng'uni, Narumu, Weruweru na kule Mronga shule zimekuwa chakavu sana. Ninamwomba, na kwa kweli kitu cha kumlilia ni hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tuna soko letu linatutesa sana, Soko la Mula. Pamoja na kwamba wametupa Soko la Kwasadala, lakini soko mlisho ni hili. Wananchi sasa hivi wanipigia simu, yaani simu yangu ina-*stuck* kwa sababu ya picha za pale Mula. Wanauzia kwenye matope. Ninamwomba sana, hatutaki soko kubwa, tunataka soko dogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Hai mapato yake hayatoshelezi, hata tukihangaika. Tuliweka bajeti ya shilingi milioni 40, tumehangaika zaidi ya miaka mitatu hatujapata ya kutengeneza lile soko. Namwomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa, ninamshukuru sana na

tena apokee maua yake kutoka kwa Mchungaji wa Lyamungo alitusaidia harambee nzuri na wanamsubiri. Nitampeleka kwenye hilo soko akija pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuhusiana na hizi barabara zinazoingiliana, zinazounganisha kata, nyingi zimekuwa chakavu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumze kwa ujumla sasa kwa kusisitiza, bajeti ya mwaka 2023/2024 Serikali ilitenga…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, kengele ya pili hiyo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimalizie kwa kusema, Mheshimiwa Waziri unasimamia TAMISEMI, kaangalieni kikokotoo, kinaumiza watumishi wa umma ambao wanafanya kazi nzuri sana ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Magessa atafuatiwa na Mheshimiwa Mtenga na Mheshimiwa Dkt. Kabati ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipatia. Napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi aliyonipatia kuongea tena Bungeni siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mchengerwa kwa hotuba nzuri aliyowasilisha jana. Yapo mengi ambayo tumepitia wakati wa kusoma, tumeona kabisa hotuba ile ilikuwa nzuri na ni kwa faida ya nchi yetu. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Festo Dugange na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa msaada mkubwa ambao wameendelea kumpa Mheshimiwa Waziri kufikia hiki

ambacho tunakiona sasa hivi. Ninawapongeza wataalamu wanaoongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Adolf Ndunguru kwa kazi kubwa ambayo tunajua ndiyo wamemfanya Mheshimiwa Waziri aje kufanya hiyo *presentation* nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Amirijeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi mzuri wa Serikali hii, ambapo tumeendelea kuona fedha nyingi zikienda kwenye majimbo yetu likiwemo Jimbo la Busanda. Bila kumsahau ndani ya Serikali Mkuu wa Mkoa wangu *RC* Shigela na Mkuu wa Wilaya yangu, Ndugu Komba kwa kazi kubwa wanayoifanya kuweza kutafsiri kile ambacho Mheshimiwa Rais anakisema kwenye maeneo yetu kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nitoe pole kwa wananchi wengi ambao sasa wanakutana na majanga na mafuriko kwenye maeneo mbalimbali ya nchi hii. Tumemsikia mchangiaji aliyepita tu amesema watu 26 wapo kwenye tatizo, tumeona Rufiji, tumeona *landslide* kule Mbeya na maeneo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninatengeneza swali dogo. Je, TAMISEMI ina kitengo kinachotafsiri, ku-*translate,* ule utabiri unaotolewa na *TMA* ili kuwapa wananchi *awareness* na vilevile kuingiza kwenye mazingira ya kibajeti? Kama kitengo hicho kipo, basi kiendelee kufanya kazi kwa nguvu zote na kitafsiri vizuri haya yanayosemwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa Dar es Salaam juzi wakasema, tarehe 13 na 14 mvua itanyesha sana, lakini wananchi wanaona tu wasitoke nje. Kama wakipewa taarifa nzuri ambayo inaonesha shida itakayotokana na mvua inayokuja kunyesha huenda tukawa tunaepuka majanga mengine ambayo yanaonekana yanatokea bila taarifa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ya ukusanyaji wa maduhuli unavyoongezeka. Nimeona hapa ukurasa wa 76, mwaka 2022/2023 kulikuwa na shilingi

trilioni 1.01, mwaka 2023/2024 kulikuwa na 1.14, ambayo sasa hivi umeshafikia takribani shilingi bilioni 800 mpaka mwezi wa Machi. Sasa hivi tunalenga kufikia shilingi trilioni 1.6 ambayo itakuwa na ongezeko la asilimia 39, shilingi bilioni 456. Inaonekana kuna mahali fulani tunakwenda. Kuna kitu fulani kinafanyika kwenye Serikali kupitia uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa napenda sana kuangalia bajeti ya maendeleo. Mpango mzima wa bajeti hii unatupeleka kwenye shilingi trilioni 3.41 kwa ajili ya maendeleo. Hapo ukisoma utagundua yapo mambo mengi yamezungumziwa kama vile hospitali 118 zitakwenda kukamilishwa kwenye maeneo yetu mbalimbali na vilevile vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa kwenye hospitali 118 mimi ninayo hospitali yenye hadhi ya wilaya pale Katoro ambayo inahitaji fedha ili iweke kukamilishwa na wananchi waendelee kuhudumiwa vizuri. Naomba sana TAMISEMI tunapokwenda kwenye utekelezaji wa bajeti hii sasa, ninaamini kabisa inawezekana wameisahau, lakini naomba waipelekee fedha takribani hata shilingi milioni 500 ili iweze kukamilishwa wananchi waweze kupata huduma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya vituo vya afya ambayo ukiangalia Ukurasa wa 84 umeonesha kuna vituo vya afya takribani 76 vinategemewa kuingizwa kwenye bajeti hii kwa ajili ya utekelezaji. Bahati mbaya sana huko Jimboni Busanda ambapo sensa ilituambia tupo 659,000 tangu tumeanza Bunge hili hatujapata kituo cha afya hata kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vya tarafa vilivyowekwa mwaka 2021, kwangu nina tarafa mbili na watu 659,000, unaweza ukajua tabu yake kama hatuna kituo cha afya hata kimoja. Naomba sasa tupate upendeleo wa vituo vya afya. Tuliomba vitatu, lakini hatujapata hata kimoja. Naomba sasa Serikali kupitia TAMISEMI, watupatie vituo vya afya angalau viwili vya kutufuta machozi tunapoenda kwenye uchaguzi mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye elimu ya msingi. Naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa fedha nyingi ambazo nimeona kama elimu ya msingi kwa miaka takriban mitatu hii kuna takribani shilingi bilioni nne imeingia kwenye maeneo ya shule ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kwa sababu eneo hilo ni kubwa, lina Kata 22 na watu zaidi ya 659,000 hao ina maana kwamba fedha iliyokwenda bado haijaonesha uboreshaji mkubwa sana kwenye shule za msingi. Kuna shule chakavu nyingi. Nimeuliza swali juzi juzi hapa nikionesha kwamba kuna Shule inaitwa Lubanda, ukifika tu pale utajua hii shule haifai tena, kuna Shule inaitwa Lulama hali yake siyo nzuri, kuna shule pale Katoro Mjini inaitwa Kabahele hali yake siyo nzuri, kuna shule inaitwa Kaduda hali yake siyo nzuri, zipo nyingi. Kwa hiyo, niombe sana kwenye bajeti hii tuangalie. Tunafanya, kuna Mradi wa *BOOST*, *LANES* na mingine mingi lakini bado hali ya shule za msingi siyo nzuri. Kwa hiyo, niombe sana tufanye maamuzi yatakayohakikisha kwamba tunapata fedha za kutosha kupambana na uchakavu wa shule za msingi ambazo tumezisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maboma ambayo yamesemwa na Wabunge wengi hapa, nina maboma ya shule ya msingi takribani 124 na maboma ya sekondari 66 yanahitaji kumaliziwa. Sasa hoja ni kwamba, walitenga fedha ya ndani iweze kumaliza haya, wamejaribu lakini bado hayaishi. Niombe Serikali itusaidie upande huu kupitia TAMISEMI yaweze kuisha, wananchi walishaweka nguvu zao kwenye maeneo haya na sisi tusaidie sasa ili yakamilike na yaweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya miundombinu, nimekuwa nasema mara nyingi hapa Bungeni, Mheshimiwa Rais mwaka 2022 alipita pale Katoro, tukaeleza wazi Mji Mdogo wa Katoro ambao una watu takribani 250,000, maeneo hayo hayapitiki na tukaomba bilioni 15, akatoa ahadi kwamba watatoa kidogo kidogo. Hata hivyo, kila nikichungulia kila bajeti inayokuja sioni imetengwa kiasi gani, maana yake naona *TARURA* huwa

wanapewa shilingi 2,000,000,000 na naendelea kuiona hiyo shilingi 2,000,000,000, maana yake hizo barabara ambazo zinatakiwa kujengwa Katoro hazijatengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana, mji ule una makusanyo makubwa, mji ule una benki nne, huu mji mdogo lakini hiyo shilingi 15,000,000,000 inaonekana aliyekuwa anarekodi huenda hakuandika akaleta TAMISEMI. Maana yake inawezekana kuna mtu alisikia Mheshimiwa Rais anasema na yeye akaacha hapo hapo, akamalizia ziara yake. Hebu TAMISEMI waiangalie hii ahadi ya Mheshimiwa Rais ipo au haipo? Kama haipo tuwarushie *clip* ili waweze kuona ukweli wa hicho ambacho Mheshimiwa Rais alitoa ahadi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo nataka niiseme pamoja na haya ambayo nimeyasema. Kuna mikopo ya 10%, Mheshimiwa Waziri jana alisema vizuri, ukiangalia ukurasa wa 63, ameonesha kwamba kuna fedha imeendelea kutengwa kwenye mikopo hii ya asilimia kumi na sasa kuna takribani shilingi bilioni 64 hivi, lakini bado hata wale wanaorejesha kuna pesa ipo. Sasa hii fedha ni lazima twende kwenye maamuzi tunafanyaje. Tukiendelea kuwa na fedha ambayo hatujafanya maamuzi tunaenda kwa njia gani kuwakopesha hao wananchi, mwisho wa siku tutakuta maneno ya *CAG* yanaonesha hela imepotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana, lengo la hiyo fedha ni kuwasaidia wananchi kwa maana ya vikundi vidogo vya akinamama, vijana na walemavu. Tuhakikishe kwamba hicho kilichokusanywa na ambacho kinaendelea kukusanywa sasa kinaenda kwenye matumizi, tusipolifanya hili litafika mahali fulani litatuchanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni hii fedha tuliyoambiwa kwamba kuna fedha ya dharura kule *TARURA*. Nimemuuliza Meneja wangu asubuhi ya leo kama hiyo fedha ilikwishafika, akajibu haijafika, lakini miundombinu ya *TARURA* ina hali mbaya kule tuliko. Hii fedha ya dharura nasikia wengine wanasema

tunapata shilingi milioni 200 wengine shilingi milioni 400, lakini kule Geita sijaisikia, kwa hiyo, baada ya mvua kupita hali imeendelea kuwa kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu lingine ni kwamba, *TARURA* bajeti ile tunayopewa ya shilingi 2,000,000,000 labda, tuna madaraja ambayo yanatakiwa kujengwa kwa mfano kutoka Jimbo la Geita kuja Jimbo la kwangu ambalo linatakiwa lijengwe kwa shilingi bilioni 1.6. Hii fedha kwenye bajeti haionekani mahali popote. Maana yake hili halitajengwa milele, kama bajeti ya *TARURA* itaendelea kuwa kama ilivyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Magessa kengele ya pili

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Kabati na Mheshimiwa Kavejuru Felix.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza. Pili, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mama yetu Samia Suluhu Hassan, nina kila sababu ya kuzungumza ni kwa nini namshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mtwara Mjini ni jimbo la historia na tunapozungumzia historia kwa wananchi waliokuwepo Mtwara wanajua kwamba historia ya kutokupata maendeleo kwa muda mrefu kwao ilikuwa kama ni sera, lakini toka Awamu ya Sita ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iingie madarakani tumepata maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Waziri Mchengerwa pamoja na Naibu Mawaziri wako wamekuwa wasikivu, ni miongoni mwa Mawaziri ambao Wabunge wakikukuta sehemu yoyote anasimama na kuzungumza nao na akawasikiliza, Mungu ambariki na aendelee na tabia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara tuna takribani shule saba ambazo zimejengwa miaka ya 1960 na kwa masikitiko makubwa shule hizi zimekuwa chakavu. Mvua hizi ambazo zinanyesha takribani kwa miezi miwili, kwa kweli watoto wanashindwa kwenda kusoma kwa sababu madarasa yote yanavuja. Nimwombe Waziri, katika zile fedha ambazo amezitenga za kupeleka kwenye majimbo au halmashauri na manispaa, basi Mtwara Mjini iwe ni sehemu ambayo inawezekana tukaokoa jahazi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo shule kongwe ya *Mtwara Girls*, shule hii kwa sasa hatuna bwalo la kulia chakula. Shule hii ni shule ambayo ni kongwe na inafahamika na ni shule ambayo ni ya kitaifa. Kwa masikitiko makubwa, juzi nilikuwa naongea na Mwalimu Mkuu, anasema watoto wanakwenda kulia vyakula kwenye bweni. Sasa niombe kwa Mheshimiwa Mchengerwa kwamba, bwawa hili tunalihitaji waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine, TAMISEMI ndiyo uti wa mgongo wa Serikali yetu, ukiangalia kwenye maeneo mengi, sisi tunapita kwenye Kamati, ukiangalia kwenye halmashauri nyingi, utakuta gari zilizokufa zipo nyingi na gari zile zinafikia mpaka kuoza. Nataka niishauri Serikali, twendeni tukayauze magari yale, kwa sababu gari ambalo leo wamelisimamisha limetengenezwa mwaka 2018 na limekaa *yard* kwa muda wa miaka mitano inanyeshewa mvua, gari lile linaharibika na linakosa *value* likienda kuuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupa mfano, leo utakuta kuna *V8* ipo inaoza. Ilisimama pale kwa ajili ya rejeta, lakini ina miaka minne, mitano mpaka leo hii. Tungeuza ile *V8* hata kwa shilingi 50,000,000 au shilingi 40,000,000 kwa gari zilizopo kwenye *yard* za Ofisi za

TAMISEMI, tungekuwa tumeokoa mamilioni ya shilingi. Hili nimelizungumza, Mheshimiwa Rais anahangaika sana kututafutia fedha na lazima Mawaziri wenye dhamana katika sekta zote tujue kwamba Mheshimiwa Rais wetu anahangaika kututafutia fedha Watanzania. Sasa kama anatutafutia fedha basi hata zile ambazo tunaweza kusaidia ili fedha zile zirudi kwenye Serikali tuchukue jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mkurugenzi wa *TARURA*. Kwa kweli *Engineer* Seff ni sehemu ya msaada kwa kila Mbunge humu ndani, Mungu ambariki sana na aendelee kutuwezesha Wabunge ili tusimame. Hata hivyo, nataka niiombe Wizara, pale Mtwara Mjini tunatumia barabara moja na barabara hii ninayoizungumzia ni Barabara ya kutoka Mtwara Mikindani kuelekea Lindi, lakini sisi tunavuka kwenye eneo la bahari na sasa hivi mara kwa mara bahari huwa inachafuka na inapochafuka maji yanavuka mpaka ukingo wa bahari, hatuna njia ya kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe *TARURA*, niiombe Wizara kwamba kuna barabara mbadala kama watatuwekea lami kutoka Mtwara kupitia Barabara ya Lwelo, ikitokea *distance* yoyote ya *jam,* basi tutumie hii barabara nyingine ambayo inawezekana wananchi wakaingia Mtwara kwa muda wanaotaka hata mafuriko yakitokea. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri watusaidie kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kuhusu jengo letu la Mtwara Manispaa. Jengo lile limejengwa mwaka 1959 na kwenye Bunge hili, miaka miwili nazungumza, watutengee fedha ili tujenge ofisi nyingine ya kisasa, ile ofisi ukiingia unadhani labda wanalala popo mle ndani. Inasikitisha mno, tunaitwa manispaa, lakini hata wageni wanapokuja wanauliza manispaa ndiyo wana hadhi ya kuwa na jengo hili? Kwa hiyo, niombe Wizara kwenye bajeti ya kujenga majengo tena, naliomba hili na Mheshimiwa Mchengerwa akiweza Bunge hili tuongozane twende akaangalie kule lile jengo lake lilivyo, labda atakuwa na uchungu na ataweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine niiombe Wizara, gari ya mkurugenzi wangu ni mbovu sana na ni kwa mara ya kwanza kuona gari ya mkurugenzi linawekwa galoni la maji kule nyuma (gari linachemka). Sasa tunakwenda kwenye uchaguzi, tuna mkurugenzi ambaye hata akiitwa Dodoma atembee muda wa saa 12 au 14 kutoka Mtwara hawezi kutembea kwa gari lake, kwa hiyo, niiombe Wizara watupatie gari nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna shida nyingine ya gari la *DC*, sasa hivi *DC* lazima amwombe mkurugenzi gari, sasa kwa nini nataka kulizungumza hili? *DC* ndiyo msimamizi wa maeneo yote ya kiwilaya, lakini leo anapofika mahali akapewa hisani na mkurugenzi kupewa gari, hivyo imetokea bahati mbaya mkurugenzi ana shida kiutawala, hivi huyo *DC* atakuwa kwenye hali gani hasa ya kuweza kulisimamia? Kwa sababu mamlaka husika ndiyo imefika mahali imempa usafiri atembee, kwa kweli siyo jambo jema sana, naomba tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, kuna huu Mfumo wa *NeST*, mimi nina fedha za Mfuko wa Jimbo, toka nimeambiwa zimepandishwa, huo mfumo sijui wanapandisha na ngazi sijui wanapandisha na nini? Hata sijui huko waliko, toka nimeambiwa unapandishwa, hii ni wiki ya nne. Mfuko wa Jimbo haujapata mamlaka ya kutumika, wale wakubwa wameshapandishwa, wanasema lazima upandishwe huo mfumo ili wao waendelee kufanya mambo yao wanayoyafanya. Sasa nataka niseme, ipo mifumo mingine inakwenda kutumaliza kisaikolojia bila sisi kuelewa mifumo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaambie wataalam kwamba, Watanzania wanahitaji matokeo. Kila Mtanzania aliyepo kwenye eneo anahitaji matokeo ambayo yatafika mahali akajua kwamba Serikali yake inamhudumia nini. Kwa hiyo, niombe hilo ni suala ambalo kwa kweli limekuwa ni gumzo la huo mfumo…

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba mfumo huu wa *NeST* kwenye Jimbo la Msalala, asilimia kubwa ya Jimbo la Msalala halina mawasiliano kabisa na fedha za Mfuko wa Jimbo tumepeleka kwenye maeneo yale ili waweze kutangaza tenda, lakini halmashauri wanawataka wale ma-*local* fundi waweze kutumia mfumo kuomba kazi zile. Mpaka tunavyozungumza hivi kwa sababu ya ukusanyaji wa *network* na hawauelewi ule mfumo mpaka sasa zile fedha za Mfuko wa Jimbo hazijatumika kwenye maeneo yale. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea na Mungu ambariki sana. Sasa hili ni janga ambalo inawezekana wenzetu hawajasema, lakini maeneo mengi huo mfumo bado unatutatiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tuna kituo chetu cha afya, kituo chetu cha afya ni kituo ambacho ni kikubwa kinahudumia zaidi ya majimbo matatu kwa sasa, lakini kituo kile tunahitaji tupate wodi mbili za wanaume na wanawake.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mtenga, kengele ya pili.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Kavenjeru Felix, tuna muda wa kutosha tutaendelea na Mheshimiwa Rehema.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya TAMISEMI. Kwanza kabisa naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri sana ambazo amekuwa akizifanya, lakini tunakupa pole sana kwa mafuriko katika jimbo lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Dugange - Naibu Waziri, pia nimpongeze Mheshimiwa Zainab Katimba kuteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara hiyo, tumeona kazi yake na amtangulize Mwenyezi Mungu ili iweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendelee kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa wa Iringa Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye tulikuwa naye hapa Bungeni na tunaona ameanza kasi ya kwenda kwenye halmashauri zote kuongea nazo. Tunaomba kasi iendelee, Iringa ni maendeleo na kazi. Siwezi kumsahau Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Halima Dendegu ambaye kwa kweli amefanya kazi kubwa sana katika Mkoa wa Iringa, namwomba mtunzeni sana huko Singida, sisi tunampenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niendelee kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli kwa hii miaka mitatu ameonesha kazi kubwa sana hasa katika nchi nzima na Mkoa wetu wa Iringa. Tunamwombea Mwenyezi Mungu, sisi Wanairinga tunamwombea dua Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda, wale wote wanaomletea matatizo washindwe na walegee kwa jina la Yesu. Nimwambie tu, kama kiongozi wala hahitaji kujibu mashambulio ya watoto, bali hekima itaonekana kwa kazi zake nzuri ambazo amekuwa akizifanya, dunia nzima inajua na Watanzania wote wenye macho wanaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye *TARURA*, barabara zetu za *TARURA* kwa kweli niungane na wote waliompongeza Mtendaji Mkuu *Engineer* Seff, hongera sana,

hajawahi kutuangusha, *big up* sana, sisi tutaendelea kumwombea ili barabara zetu ziendelee kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nzima sasa hivi mvua ni nyingi, barabara nyingi zimeharibika. Mkoa wetu wa Iringa una mvua nyingi sana na barabara zote hazipitiki. Kusema ukweli hizi barabara ndiyo barabara za kiuchumi, hizi barabara sasa hivi akinamama wajawazito wanapata shida sana kwa sababu kuna kata nyingi hakuna vituo vya afya, hakuna zahanati, kwenda kujifungua wanapata shida, wanapanda bodaboda. Kwa hiyo, tunaomba sasa *TARURA* wapatiwe fedha za dharura za kutosha ili barabara hizi ziweze kupitika kwa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya halmashauri zina mapato makubwa, waanze kutenga fedha kwa ajili ya matengezo ya hizi barabara ili muda wote ziweze kupitika, ndiyo uchumi ambao tunategemea katika Mkoa wetu wa Iringa. Kuna baadhi ya barabara nazitaja, sitataja zote kwa sababu nyingi ni mbovu; ukienda kwenye Mkoa wa Mufindi, utakuta kuna ile Mdabulo-Ihanu, Kilosa-Ibwanzi, Ilogombe-Kipanga hadi Ufiwa, Saadani Ikwea-Uliwaya, unakwenda Magunguli-Ihomasa, barabara haipitiki kabisa kuna mlima pale. Kuna daraja la Mtakuja mpaka Itandula, kuna ile Itika mpaka Makambako haipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija Kilolo sasa, utakuta pale kuna Mtandika- Msosa, Mtandika-Nyanzwa, Water-Lisoli, Udekwa-Mlafi Isagwa, Makungwi, Ipalama, Ikwega, Ikwega-Kimala, Kimala-Idunga, Msosa, Ndengisivili-Kimala, Ihimbo-Itimbo, Itimbo-Kitelewasi. Jamani ningezitaja zote lakini watanisamehe Wanairinga kwa sababu barabara nyingi hazipitiki na siku hiyo nilipouliza swali Mheshimiwa Katimba ulituahidi kuja Iringa kuona. Kuna ile barabara ya Ilula-Imaga Ibumu, nilisema nawaomba jamani, Injinia wetu Mfugale alitokea pale Image, kama barabara haipitiki kwa kweli amefanya kazi kubwa sana katika nchi hii, waje waweke lami kabisa ili barabara iweze kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa Serikali ilete mwongozo kwa wafanyakazi ambao wanajitolea katika halmashauri zetu, kumekuwa kuna tatizo kubwa sana na hasa kwa watendaji wa Serikali za Mitaa, za Vijiji hata Mheshimiwa Kikwete alipokuja pale alikuta kuna changamoto kubwa, wafanyakazi wamejitolea kuanzia, miaka minne, miaka mitatu, miaka miwili, au mwaka mmoja, lakini zinapokuja ajira na Iringa kwetu kazi nzuri imefanyika, Mheshimiwa Halima Dendegu anajua, kusafi sana; na kazi kubwa ilikuwa ya watendaji. Inapokuja ajira kama hawaajiriwi, tunajisikia vibaya sisi kama viongozi, sisi kama wazazi, kwa kweli tunaomba huo mwongozo uletwe haraka sana ili wanaojitolea basi waweze kuajiriwa na naomba wale ambao walikuwa wanatakiwa warudishwe, basi warudishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kwa ujenzi wa shule katika Mkoa wetu wa Iringa, ikiwemo shule ya wasichana ambayo imejengwa katika Wilaya ya Kilolo. Tunaomba Serikali ifanye maboresho makubwa kwa walimu wetu. Walimu hawana nyumba, katika shule zinazojengwa wajenge kabisa na nyumba, yapo maboma ya nyumba za walimu ambayo hayamalizwi kujengwa. Pia, waweke *furniture,* madawati yanapoletwa walimu wanakalia madawati ya watoto badala ya *furniture* za walimu. Tunaomba *furniture* ziwekwe ili kuwapa heshima walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la malimbikizo ya madeni ya likizo na uhamisho, hata Mheshimiwa Kikwete alipokuja, yalikuwa ndiyo malalamiko makubwa. Wakati mwingine mtu analipwa mshahara mwezi huu, mwezi huu halipiwi na akianza kufuatilia anahangaika sana huko Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wengi wamejitolea na *list* ya hawa walimu ninayo, nitaomba niilete. Leo Mheshimiwa Waziri Simbachawene amesema kwamba, wanatakiwa waajiriwe, nitaleta *list* yote ya Mkoa wa Iringa ili wale waliojitolea na wanafanya kazi vizuri waweze kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kikokotoo, namshukuru sana Katibu Mkuu wetu ambaye amekizungumza katika ziara zake kwamba, anamwona Mheshimiwa Rais ili hiki kikokotoo kiweze kufanyiwa kazi na namuunga mkono. Najua Mheshimiwa Rais wetu kipenzi atalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kurejesha utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Naomba sheria imwangalie mwanamke aliyezaa mtoto mwenye ulemavu, hayuko popote, huyu mama anapata shida na hawezi kukopesheka kwa wanawake wala kwa watu wenye ulemavu ili aweze kusomesha mtoto wake mwenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kuhusiana na mifumo ya malipo, ni changamoto kubwa sana katika halmashauri zetu. Unakuta pesa zinakuja, lakini hazitoki, mkurugenzi anashindwa kufanya chochote na miradi inachelewa. Naomba hii mifumo iangaliwe na changamoto hizi ziondolewe ili pesa ikija iweze kutumika kwa wakati, siyo miezi mitatu hadi miezi sita pesa ipo, lakini haitumiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Serikali iweke mpango mkakati kuhakikisha maboma yanamaliziwa kujengwa. Maboma ya vituo vya afya, zahanati, kwenye shule ambazo baadhi unakuta ni wananchi wamejitolea kujenga. Kuna shule nyingine zile...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kabati, kengele ya pili.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi naomba niunge mkono hoja. Namshukuru Mungu na Mwenyezi Mungu aendelee kunilinda. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Felix, tutamalizia na Mheshimiwa Rehema.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya. Wananchi wa Buhigwe wamenituma nishukuru sana kwa fedha nyingi ambazo zimekuja kwenye masuala ya elimu, afya, miundombinu ya barabara, maji na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mchengerwa, kwa kazi kubwa anayoifanya. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Dugange, Naibu Waziri, kwa kazi kubwa sana, ametugusa Wanabuhigwe kwenye upande wa afya. Nampongeza sana na kumtakia kila la heri dada yangu Mheshimiwa Zainab Katimba kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais. Sina shaka na yeye, yeye ni jembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naanza na *TARURA*. Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nimepitia hotuba yako, ni hotuba nzuri sana. Nakupongeza kwa kazi kubwa ambayo imefanywa na *TARURA* nchi nzima, hususan katika Jimbo la Buhigwe. Nampongeza Mkurugenzi Mkuu wa *TARURA*, *Engineer* Seff, kwa kazi kubwa anayoifanya na kwa jinsi anavyotupokea na kutusikiliza vyema. Nampongeza *Engineer* wangu wa Mkoa, Ndugu Goodluck Mbanga, ambaye ni Meneja wa *TARURA,* Mkoa wa Kigoma kwa kweli, anapiga kazi. Pia, nawapongeza na kuwashukuru kwa kuwa, waliniletea *Engineer* kijana Ndugu Enock Gambishi, ambaye ni Meneja wa *TARURA* Buhigwe, kazi anayofanya ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa barabara nyingi zimetengenezwa kwenye jimbo langu, lakini na sisi tumepata athari ya hizi mvua za *El-Nino*. Nashukuru nimepata fedha ya dharura kwa ajili ya kurudisha mawasiliano ya Kijiji cha Kigogwe, Murungu na sehemu ya pili ya Wilaya ya Kigoma Vijijini, kwa hakika tunashukuru sana, lakini bado tuna uhitaji mkubwa sana kwa sababu, mvua imenyesha na mafuriko yamepita. Mheshimiwa Waziri, pole sana kwa mafuriko yaliyotokea kule Rufiji, tutavuka, Mungu ni mwema hatatuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna uhitaji mkubwa wa kutengenezewa madaraja ili kuweza kuunganisha maeneo yetu. Tunahitaji kujengewa daraja katika Mto Mkoza ambao unakatisha kwenye Barabara inayounganisha Kata ya Mubanga na Kata ya Rusaba. Vilevile tunahitaji daraja katika Mto Jujilo, ambayo ni Barabara ya Kibande kwenda Kitambuka, daraja lililokuwepo lilikatika na likachukuliwa kabisa na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kujengewa Daraja la Mto Mitegwe katika barabara inayounganisha Janda na Mhunga, kwenye Jimbo la Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako. Katika Barabara ya Mkatanga *Head Mission* tuna Mto Mtunguruzi, hapa lilikuwepo daraja ambalo lilikuwa limetengenezwa na wananchi, mvua zilizonyesha zimelibeba na mawasiliano yamekatika. Tunaomba fedha ya kutosha ipelekwe *TARURA* ili waweze kututengenezea daraja hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji Daraja la Mto Luiche kwa ajili ya kuunganisha Barabara ya Kigogwe mpaka Murungu na pia tupate daraja lingine kwenye Mto Mbuza, ambayo ni Barabara ya Muhinda kwenda Mwilika. Tukipata madaraja haya tutashukuru sana na nina imani Serikali imesikia, haitatuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka *TARURA* sasa niende upande wa afya. Nashukuru kwa muda huu tumefanikiwa kupata vituo vya afya vipya vitatu na pia, tumepata fedha nyingi ambazo zimesaidia kumalizia maboma ya zahanati sita. Bado tuna

hitaji fedha nyingine ili kumalizia maboma ya zahanati na shule za msingi. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kama walivyosema, nasi Buhigwe ni wahitaji pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye huduma ya afya. Sera ya Afya inasema, huduma ya afya kwa mama, mtoto na wazee ni bure, watu hawa wanapaswa kutibiwa bure, lakini utekelezaji wake kwenye wilaya yangu umekuwa ni mgumu sana, sijui kwingineko. Wizara ya Afya ni watunga sera na watekelezaji ni halmashauri zetu, nashauri kila halmashauri ianishe chanzo cha mapato kwa ajili ya kulipia gharama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la elimu nikiunganisha na afya. Kumekuwa na changamoto kubwa sana hasa kwenye upande wa watumishi. Kama Biblia inavyosema kwamba; "Bwana utakapowazuru watu wengine usiniache na mimi," basi katika hizi nafasi zaidi ya 12,000 za walimu ambao wataajiriwa na sisi Wilaya ya Buhigwe tunaomba tupate idadi kubwa ya walimu kwani tuna upungufu wa takribani asilimia 47. Ombi hili linakwenda sambamba na ajira za watumishi wa afya ambao Mheshimiwa Waziri, asubuhi, amesema zaidi ya 10,000 wataajiriwa kwani pia tuna upungufu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye elimu, namwomba Mheshimiwa Waziri, fedha iongezwe kwenye ujenzi wa nyumba za walimu waweze kuwa na makazi mazuri, wawe na mazingira bora ya kufundishia ili wawe *motivated*. Bila kusahau maabara na maktaba katika shule za sekondari.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, jioni tunaanza na Mheshimiwa Stella Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Kalogeris,

Mheshimiwa Regina Ndege na Mheshimiwa Aloyce Kwezi. Sasa namwita Mheshimiwa Rehema Migila.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwa asubuhi ya leo. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa zawadi ya uhai ya kuwemo humu ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naendelea kumshukuru kipenzi chetu Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa anayoyafanya kwa wananchi wake wa Tanzania. Tunaona ameboresha maeneo kila sehemu hakuna ambaye hajui Dkt. Mama Samia amefanya nini. Wenye macho wanaona na wenye masikio wanasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo nitaanza kujikita kwenye sekta ya afya. Kama walivyochangia watangulizi wenzangu, tunaona namna gani Mama Samia ameweza kuboresha sekta ya afya katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, nikianzia kwenye Jimbo langu la Ulyankulu lenye kata 15, wakati Mama Samia anaingia madarakani, lilikuwa lina kituo kimoja tu cha afya ambacho kinafanya kazi, ambacho ni Kituo cha Afya Ulyankulu. Mpaka hivi tunavyoongea, kuna vituo vinne ambavyo vinafanya kazi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyojali afya za wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona pia ameweza kututengea shilingi milioni 600 kwa ajili ya kununua vifaa tiba kwenye Kituo cha Afya cha Ileje na Uyowa, lakini pia tumeweza kupatiwa *ambulance* kwa ajili ya kuwasaidia akinamama wajawazito pamoja na jokofu kwenye kituo changu cha afya cha Ulyankulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya yote mazuri, Mheshimiwa Waziri, bado kuna changamoto kubwa sana kwenye vituo vyangu vya afya. Tatizo la kwanza ni uhaba wa watumishi, yaani huwezi kuwa na majengo ya afya, *just* vituo ambavyo hazina watumishi. Leo hii kituo changu cha afya cha Uyowa kina watumishi watano, Kituo cha Ileje kina watumishi wanne, Mwongozo watatu na Ulyankulu watano. Kama tunavyojua sera ya afya, watumishi wanaotakiwa kuwepo kwenye kituo cha afya ni lazima wawe 25 na zaidi, lakini kwa idadi hii hakuna kazi inayofanyika, wananchi wanaenda pale hawatibiwi inavyotakiwa. Kwa hiyo, hata juhudi hizi ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Rais zinaweza zisionekane. Hivyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri anapokuja kwenye bajeti yake tunaomba watumishi waongezeke, hasa kwenye vituo vyangu hivi vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kituo cha Afya cha Ulyankulu, kile ndio kituo changu kikubwa kabisa ambacho kinahudumia karibu jimbo zima, hivi vingine ni vipya, havijaanza kutoa huduma inavyotakiwa. Kituo hiki tunavyoongea hapa kinahudumia jimbo zima, lakini hakina wodi za kulaza akinamama, watoto wala akinababa. Sasa hawa watu wanatoka maeneo mbalimbali na ukizingatia jimbo langu ni la kijijini. Namwomba Mheshimiwa Waziri, atenge bajeti kwa ajili ya kujenga wodi za kulaza hawa wagonjwa wangu katika Kituo cha Afya cha Ulyankulu. Najua hilo liko ndani ya uwezo wako na usipofanya hivyo, najua nini kitatokea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto ya watoto walio chini ya miaka mitano ambao bado wanaendelea kutozwa gharama za matibabu na isitoshe hata akina mama wajawazito wanaendelea kutozwa hata kadi ya kliniki, yaani karne ya 21, mazuri yote Mheshimiwa Dkt. Mama Samia anayoyafanya, lakini tunapata aibu kwa kutoza kadi ya kliniki ambayo ni shilingi 500, *this is very shameful*. Nafikiri kuna haja ya kuangalia namna ya kupeleka hivi vifaatiba kwenye hivi vituo vyetu vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kwenye upande wa pili, upande wa *TARURA*. Naungana na watangulizi wangu, ni kweli

*TARURA* wanafanya kazi nzuri sana. Kuna mambo mengi sana ambayo *TARURA* wanaendelea kuyafanya ili kuhakikisha barabara zetu zinapitika kipindi chote. Kwenye jimbo langu wameweza kunijengea daraja kubwa sana pale katikati kati ya Kata ya Nhwande na Kata ya Ichemba kuna mto, daraja lile limegharimu shilingi bilioni moja. Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mama Samia na *TARURA, Engineer* Seff, wanafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wametupandishia hadhi baadhi ya barabara ambazo, kama tunavyojua Jimbo letu na Wilaya yetu ya Kaliua asilimia kubwa ilikuwa ni hifadhi, lakini baada ya kutupandishia hadhi hizi barabara zetu zimeendelea kupitika. Sasa naomba sana, kuna kiasi cha fedha cha shilingi milioni 300 kwenye bajeti yangu ya matengenezo, zimechukuliwa na *TARURA*. *Engineer* Seff, naomba unisikilize vizuri baba yangu, naamini kabisa hili suala liko ndani ya uwezo wako, hizi fedha tunaomba zirudi ili zikafanye *maintenance* kwenye hizi barabara zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zangu nyingi kwa sasa hazipitiki; Barabara za Taba – Keza, Sasu – Nhwande, Ichemba – Nhwande, Sasu – Ileje na Milambo – Kalindo, hazipitiki. Pia, kuna barabara naomba ipandishwe hadhi, Barabara ya Kipendamoyo – Mwanduti, kutokea pale *Forest*. Naomba sana, hii barabara ni ya muhimu kwa sababu inapitisha mazao ya biashara, watu na bidhaa za aina mbalimbali. Hivyo, naomba haya maombi yangu yaweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi lingine kwa Wizara, kuna mto mkubwa sana ambao unatenganisha Kata ya Mwongozo na Kijiji cha Mwanduti. Pale tukijengewa daraja litaenda kuokoa watu wengi ambao kwa sasa wanatumia vimitumbwi ambavyo vinawabinua kila siku wanakufa. Tunaomba sana, kama tunaweza kushughulikia maeneo mengine yaweze kupitika, basi nakuomba Mheshimiwa Waziri, hili daraja na lenyewe liende likajengwe huko Mwanduti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye sekta ya elimu; kiukweli namshukuru Mwenyezi Mungu, katika zile ahadi ambazo ziko ndani ya Ilani ya Uchaguzi sasa hivi Kata zangu zote za Jimbo la Ulyankulu zina shule za sekondari, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mama Samia. Pia, kuna shule za msingi zimejengwa kule Mnange, awali zilikuwa na msongamano mkubwa, lakini kwa sasa hali imekuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hii nzuri iliyofanyika bado kuna changamoto kubwa sana kwenye upande wa elimu. Kwanza, kuna uhaba wa walimu na bado hata matundu ya vyoo hakuna. Tunaomba walimu waajiriwe, pia naomba mwongozo wa walimu wa kujitolea na wenyewe ujulikane mapema na uanze kazi. Vilevile kuna hii *smart class* ambayo tumeona sasa hivi imeanzishwa na walii-*launch,* basi isiishie tu Kibaha na Dodoma Sekondari, nataka hata kule kwenye Shule yangu ya Sekondari ya Ulyankulu, Kanoge na Ichemba, kote kwenyewe ifike hii programu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo wenzangu wameliongelea sana, suala la kikokotoo. Kikokotoo ni suala ambalo linawanyima usingizi watumishi wetu, hususan walimu. Sasa hivi walimu na watumishi wanashindwa kufanya kazi vizuri, kila wakilala wakiwaza, wanawaza kikokotoo. Sasa Mheshimiwa Waziri, hivi tuseme ukweli, hiki kikokotoo hivi hii hela ni ya kwao au ni ya nani? Kama mnawakata kwenye mishahara yao, *why* inapofika wakati wa kuwalipa mnawapangia masharti, mnawapa asilimia 33 halafu nyingine mnawalipa kidogo kidogo? Kama mtu alichangia na kama hii siyo bima kwa nini msimpe mtu mzigo wake wote? Leo mtu hajajenga, anasubiri astaafu ndiyo ajenge. Halafu kama ilikuwa apate milioni 50 unampa milioni 25. Anaenda kujenga nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnawapa *stress* wafanyakazi, wanakaa hawafanyi kazi inavyotakiwa kwa sababu ya hiki kikokotoo. Mbaya zaidi hiki kikokotoo hata fao la kujitoa hamtaki kulirudisha, ni bora mrudishe fao la kujitoa. Kama hiyo haitoshi basi ni bora hata…

Waheshimiwa Mawaziri naomba tusikilizane, hili suala la kikokotoo ni nyeti sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama fao la kujitoa halipo, basi tunaomba hata kwenye pensheni yao, kama ilivyo sisi Wabunge, ukifika muda unaweza ukachukua kiasi fulani na hawa watumishi wapewe hiyo *room,* kwamba, ukifika muda fulani wamefanya kazi, waweze kuchukua cha kwao mapema. Siyo wengine wanakufa kabla ya muda na hawajachukua mzigo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili suala la kikokotoo liangaliwe kwa jicho la tatu. Wafanyakazi wafanye kazi wakiwa wana furaha tele, kuliko sasa hivi wanafanya kazi kwa *stress* sana. Hili suala kwa kweli mimi mwenyewe nilikuwa mfanyakazi, limenitesa sana. Naomba sana, nadhani tunasikilizana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni fedha za 10%. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuturudishia 10% kwa ajili ya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu. Naomba kwa sababu, wameanza na halmashauri kumi kama mfano, naomba sasa hizi halmashauri nyingine ambazo bado hazipo kwenye majaribio mpango uende haraka. Kwa sasa hivi vijana na akinamama wame-*stuck* na biashara zao haziendi kwa sababu wamekosa mitaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema, ahsante.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, nilishamtaja Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, wajiandae Mheshimiwa Innocent na Mheshimiwa Regina Ndege.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara hii muhimu sana Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Awali ya yote, nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai. Pia, niungane na wenzangu kumpongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wanaomsaidia Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote hususani Waziri Mchengerwa wa Wizara hii ambayo leo tuko nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue nafasi hii kumkaribisha Mkuu wetu wa Mkoa mpya Mheshimiwa Abbas pamoja na *DC* wetu Mheshimiwa Magiri katika Mkoa wetu wa Ruvuma, lakini katika Wilaya yangu ya Nyasa. Sambamba na hilo, niwashukuru wale ambao walihudumia katika Wilaya yangu ya Nyasa, Mheshimiwa Kanali Thomas pamoja na Mheshimiwa Filberto Sanga kwa kazi ambayo wameifanya wakati wakiwa katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitakuwa na maneno pengine siyo mengi sana kwa sababu, kwanza nimefurahishwa kuona kwamba Bajeti ya Wizara hii imeendelea kuwa kubwa kiasi cha kujua kwamba inawajali wananchi, kwa sababu, Wizara hii ndiyo ambayo ni mhimili wa nchi yetu kwa misingi ya kwamba ndiyo wananchi wenyewe wanaposhiriki katika kufanya maamuzi lakini pia kujiletea maendeleo wao wenyewe wakisaidiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu Bajeti ya Wizara hii iko takribani shilingi trilioni 10 siyo kawaida na haijawahi kutokea. Ninavyofahamu ni kwamba hayo ni makadirio, lakini sisi Watanzania wote tunao wajibu wa kufanya kazi, kulipa kodi zetu ili kuhakikisha kwamba matarajio haya yanafikiwa, kwa sababu, haitoshi tukawa na matarajio makubwa halafu tusiweze kuyafikia hayo malengo. Kwa hiyo, niwaombe Watanzania wote kushirikiana kila mtu kadiri atakavyoweza ili kuona kwamba dhamira hiyo inafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi katika hilo niende moja kwa moja kwenye Jimbo langu. Kwanza, Jimbo letu la Nyasa lipo katika bonde la ufa na wakati huo huo liko chini ya Milima ya Livingstone. Wakati mwingine hata mvua zinapokuwa nyingi sisi tunaathirika zaidi kwa sababu barabara zetu zimepita kandokando ya hiyo milima na Ziwa Nyasa, lakini pia kuna mito mikubwa inayotoka milimani kwenda huko na hata katika maeneo ya juu ambayo yana udongo wa mfinyanzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya dharura naomba sana jimbo langu lisiachwe, naomba sana. Hivi karibuni nikitoa pia pole kwa wenzetu wa Rufiji, Mbeya na maeneo mengine na sisi kule Nyasa tulikumbwa na mafuriko eneo la *Mbamba Bay* na Lituhi kiasi kwamba mazao ya chakula kwa kweli yameharibika. Kwa hiyo, tutahitaji msaada wa mbegu pamoja na chakula kwa ajili ya wale waathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo niombe, kuna madaraja mengine kwa mfano daraja linalovusha wanafunzi wa Shule ya Msingi Mkali B, limebomoka kabisa. Kwa hiyo ni machache

nayataja lakini kimsingi jimbo langu linahitaji fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hasa hizo za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa kusogeza huduma za afya vijijini. Nilikuwa nauliza kila siku damu za watu wanaoishi vijijini zenyewe hazisikii maumivu, kwa nini hospitali nzuri zinakuwa mjini, vijijini hakuna, lakini jibu hili sasa hivi limepatikana kwa kiwango kikubwa. Sasa ninaloomba vituo hivyo vingine havijakamilika. Vifaatiba vimepatikana lakini vya aina moja, aina nyingine havipo. Watu siku hizi wameshaanza kupata huduma hata za upasuaji kwenye maeneo ya vijijini mfano Mkili, pale Kihagara, *Mbamba Bay* yenyewe. Sasa tunatarajia tuanze Kingerikiti na Liparamba, lakini vifaatiba bado havijaweza kupatikana vyote, sababu kubwa ni nini? Wizara ilishatoa fedha, Mheshimiwa Rais ametoa fedha za kutosha kununua vifaa, lakini *MSD* inaonekana uwezo wake ni mdogo ku-*supply* hivyo vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye jimbo langu tuna zaidi ya shilingi milioni mia tatu na kitu hazijatumika kutoka kwenye zile milioni 500 tulizopewa. Naomba Wizara ifikirie kuruhusu halmashauri kununua vifaa hivyo hata kwa Wazabuni wengine ili hospitali hizo ziweze kufanya kazi iliyokuwa imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, niseme tu kwamba kuna maboma ya zahanati, kwa mfano, mwaka huu kwenye jimbo langu, zahanati hazijatengewa kabisa fedha za kuendeleza maboma yake. Naomba sana Zahanati ya Nkaya, Zahanati ya Mipotopoto, Zahanati ya Hongi, angalau hizo zahanati nne ziweze kupata fedha. Hawa watu wanaoishi huko inawezekana wasiwe wengi sana kwa idadi lakini wanateseka na wanatembea mwendo mrefu kupata huduma hizo. Tunaomba sana p*lanning* ya siku hizi isiangalie tu idadi ya watu iangalie pia jinsi hawa watu walivyokaa na wanavyoweza kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tumejengewa jengo la halmashauri zuri limekamilika na hospitali ya wilaya kubwa nzuri imekamilika. Changamoto iliyopo lile jengo la halmashauri halina

*furniture*. Tunaomba sana, tumeteseka sana kwa muda mrefu wale watumishi wamefanya kazi hata kwenye *corridor* wamevumilia sana toka halmashauri ile inaanza, basi tukamilishiwe. Kwa sasa zinapotoka fedha zinaenda tena maeneo tu mengine kulekule ambako wamekuwa wanapata, sisi tunabaki tena tuna jengo zuri halafu hatuna pa kukaa, watumishi hao wanakosa moyo, ndiyo maana wanahama kila siku. Naomba sana *furniture* za Jengo la Halmashauri ya Nyasa ziweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji pia uzio kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Nyasa. Hospitali ile imekaa eneo ambalo ni la kipekee lakini mahali pazuri sana kwa bahati linakaribiana pia na maeneo ya hifadhi. Pia, hata wadau wengine wajanja wajanja, vibaka vibaka wanapita mule, wanaiba vitu vidogo vidogo lakini vingine vinaweza vikaonekana ni vitu vidogo kumbe ni muhimu sana katika matumizi ya hospitali. Kwa hiyo, naomba pia tupate fedha kwa ajili ya uzio wa Hospitali ya Nyasa pale Nangombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi sasa kwenye shule, naipongeza sana Serikali yangu chini ya uongozi wake Mheshimiwa Rais wetu mpendwa sana Mama Samia. Tumepata shule nzuri na kubwa lakini kutokana na hali halisi ya mazingira, unakuta una shule nzuri kwa mpangilio uliopo, madarasa mazuri, lakini inashindwa kuchukua wanafunzi wake vizuri kwa sababu ya kukosa mabweni. Kata zetu kule vijijini ni kubwa sana kwa hiyo hata ukiweka sekondari hiyo ya kata bado wanafunzi wanatoka umbali mrefu, unaweza kukuta umbali ni kilometa sita inabidi atembee asubuhi mpaka jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuweka *efficiency* na matumizi sahihi na mazuri ya hizo shule ni vyema tuweke angalau bweni moja kwa ajili ya watoto wa kike na bweni moja kwa ajili ya watoto wa kiume, ili hizo shule sasa ziweze kuwa na matumizi bora zaidi kiasi kwamba hata watu wa maeneo mengine ambao shule zao ziko mbali wanaweza kwenda kwenye shule hizo, kwa sababu miundombinu iko ya kutosha na wataweza kupata elimu inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, iko haja ya kuangalia sasa, badala tu ya kuendelea kujenga shule mpya kuna haja ya kubomoa kabisa zile shule ambazo zinaonekana siyo shule. Kwa sababu, wale watoto wanajisikia vibaya wanapoona Serikali yao inajenga shule nzuri na watoto wengine wanakaa vizuri kwenye shule zao, halafu vishule vingine vipo vya ajabu ajabu vinawakosesha raha, bomoa kabisa, bomoa tujenge shule nzuri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent, wajiandae Mheshimiwa Regina, Mheshimiwa Kwezi na Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ambayo imebeba dhamana kubwa ya maisha ya Watanzania. Pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha nyingi katika halmashauri zetu ikiwemo Halmashauri ya Morogoro Vijijini kwenye nyanja mbalimbali za elimu, afya, umeme, maji na barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, mdogo wangu Mchengerwa na pole sana kwake kwa mafuriko ambayo yamempata katika jimbo lake, *by the way* ni pacha wangu. Vilevile niwapongeze Manaibu wote wawili Dkt. Dugange na Dada yangu Zainab kwa kuteuliwa kwake. Ni imani yangu kabisa kwamba atamsaidia Mheshimiwa Waziri, lakini atamsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza maono yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza *RC* wangu, *DC* wangu lakini na Sekretarieti ya Mkoa, Ndugu yangu Malima na Dada yangu Rebecca kwa kazi kubwa ya usimamizi wa fedha hizi ambazo sisi kama Bunge tunazipitisha na zinakwenda kwenye mikoa na wilaya zetu katika kutekeleza na kuweza kuleta matokeo chanya kwa Watanzania. Nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Ndugu yangu *Engineer* Seff wa *TARURA* na watendaji wake wote wa ngazi ya mikoa na wilaya kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika suala la barabara ambalo ndilo linaleta uchumi katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *TARURA*, niendelee kuipongeza Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Jemedari wetu Mama Samia Suluhu Hassan, kwangu ndani ya jimbo langu, ndani ya kipindi cha miaka mitatu kumekuwa na ongezeko la fedha. mwaka wa fedha 2021/2022 tulipata bilioni 1.275, lakini mwaka wa fedha 2022/2023 tumepata bilioni 1.769 na mwaka wa fedha 2023/2024 tumepata bilioni 1.9725, ni ongezeko kubwa. Pamoja na ongezeko hilo bado kuna uhitaji mkubwa wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo langu liko ndani ya Wilaya ya Morogoro. Wilaya ya Morogoro ambayo ina kilometa za barabara 750 za wilaya yote, lakini, jimbo langu tupu lina kilometa 245 *almost* ni asilimia 40 ya urefu wa barabara ile. Kwa fedha hii tunayoipata kwa kweli ni kwamba hatuwezi kutengeneza barabara zikaweza kufika pale tunapoweza kupahitaji. Ombi langu kwa Serikali tuangalie jinsi gani tutaweza kupata fedha ambazo tutaongeza kwenye Mfuko wa *TARURA* ili iweze kutengeneza barabara kwa uhakika na ziweze kupitika mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitaji la barabara kwenye halmashauri yangu na jimbo langu kwa mwaka tunahitaji *almost* bilioni sita, sasa tunapata bilioni mbili ni fedha ndogo sana. Kuna barabara ya Kiswila –Konde, barabara ya Kibogwa – Tawa, barabara ya Tawa – Kibungo Juu, barabara ya Mvuha – Bungu, barabara ya Dutumi – Kasanga, barabara ya Dakawa – Bwakila Juu,

barabara ya Mngazi – Singisa, barabara ya Sesenga – Lumba Chini na barabara ya Gomelo – Nyarutanga – Mdokonyole, Kilengezi – Kongwa – Lukooni - Chamanyani – Tunguo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zote ninazozizungumzia ni barabara ambazo zinakwenda kwenye milima. Jimbo langu lina kata 17, lakini kata zote kumi ziko milimani ndiyo hizi kilometa ninazoenda 245. Utengenezaji wa barabara kwenye maeneo hayo unahitaji utaalam wa zege au kujenga kwa mawe. Kwa hiyo, tunahitaji fedha nyingi ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na adha hii ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, hebu tuone tunafaya utaratibu gani Wizara ya Fedha kuongeza fedha *TARURA* ili tuweze kutengeneza barabara za uhakika na zipitike mwaka mzima, hasa ukitilia maanani kwa mwaka huu tumepata mvua za *El-Nino* ambazo zimefanya uharibifu mkubwa. Hata hivyo, fedha zile ambazo zimetengwa bado pia hazijafika, lakini hata fedha ambazo zimeombwa kwa matengenezo ya dharura hazijafika. Ombi langu kwa Serikali, Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa lakini tuendelee kumsaidia kutatua changamoto za barabara katika eneo la *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la afya, tuna kila sababu ya kumpongeza Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye suala la afya. Kwenye jimbo langu ndani ya kipindi cha miaka mitatu tumepata vituo vya afya vitatu; Kisaki, Kisemu na Kasanga. Pia, tumeweza kukamilisha zahanati nne ambazo baada ya wananchi kujenga kwa kutumia nguvu zao tumepeleka milioni hamsini hamsini na zahanati hizo zimekamilika; Kisila, Lubasazi, Mwambani pamoja na Sesenga. Sasa hivi bado tuna Zahanati ya Ngongolo tumeipelekea fedha, kuna Zahanati ya Malani tumepelekea fedha, lakini kuna Zahanati ya Dolo tumepelekea fedha milioni hamsini, hamsini, ni imani yetu ndani ya kipindi kifupi cha mwaka huu kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha zitakuwa zimekwisha na tutaweza kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo bado zipo changamoto ambazo ningependa kumwambia Mheshimiwa Waziri aone jinsi gani anatusaidia. Bado kuna uhitaji mkubwa wa vituo vya afya kwenye Kata za Mlimani, Kata ya Singisa na Kata ya Bwakila Juu. Mwaka jana tuliandika hapa na nilizitaja kata hizo sasa sijajua katika bajeti ya mwaka huu kama limepitishwa hilo, je, watatusaidia vipi kuweza kuwasaidia wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna uhitaji kwenye Kituo cha Afya cha Tawa. Hiki ni kituo cha zamani, kuna uhitaji wa ukarabati mkubwa, lakini ujenzi wa jengo la mama na mtoto, jengo la upasuaji, jengo la kuhifadhi maiti, kufulia na maabara. Vilevile, tuna uhitaji mkubwa wa uzio kwenye Kituo cha Afya cha Dutumi. Kwenye hospitali ya wilaya bado tuna changamoto kubwa ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto, uzio, lakini vilevile na jengo la VVU. Ombi langu kwa Serikali, waangalie jinsi gani wataweza kutusaidia sisi Wilaya ya Morogoro Vijijini, Halmashauri ya Morogoro Vijijini, Jimbo la Morogoro Kusini, tukafanikisha mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la vifaatiba, naona Dada yangu *Engineer* Manyanya amezungumza, ni ukweli usiopingika fedha zinakwenda kwenye *MSD*, kwa miaka miwili tumepeleka *almost 1.2 billion* Halmashauri ya Morogoro Vijiji, lakini mpaka leo tunavyozungumza bado vifaatiba havijafika. Nadhani tuna wajibu na umuhimu wa kuona tunafanya vipi ili ikiwezekana tutafute wadau wengine au tutafute wazabuni wengine waweze kusaidia kazi hii *MSD*, kwa maana inaonekana imeshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la shule, niendelee kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika ujenzi wa shule. Tuna shule mpya tumepata ya wasichana ya mkoa ambayo tumepata *almost* bilioni nne, lakini kuna Shule mbili za Bungu na Kisaki. Ombi langu kwa Serikali, bado tuna uhitaji wa shule kama tatu katika Jimbo la Morogoro Kusini kwenye Kata ya Bwakila Chini, kwenye Kata ya Kisemu na kwenye

Kata ya Mvuha. Wanafunzi ni wengi na wanakwenda umbali mrefu kiasi ambacho inawachanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la shule niombe, sisi kama nilivyotangulia kusema, Jimbo la Morogoro Kusini liko katika maeneo ya milimani. Ombi langu kwa Serikali wangetusaidia kupata mabweni kwenye kata ambazo zipo milimani; Kata ya Kibogwa, Kata ya Bwakila Juu, Kata ya Singisa, Kata ya Kolelo, Kata ya Kasanga na Kata ya Tawa. Ili vijana wetu hasa wa kike badala ya kwenda kupanga kwenye nyumba za watu binafsi wakae kwenye makao salama ili waweze kupata elimu inayostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba nyumba za walimu ziendelee kujengwa, pia naomba tupate walimu na watumishi kwa sababu kiuhalisia kazi zote hizi pamoja na jitihada zinahitaji watumishi, bado tuna changamoto ya watumishi na naamini kwamba tukiwapata haya matarajio ambayo Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan anayataka kwenye nyanja za elimu, kwenye nyanja za afya na kwenye nyanja za barabara wanaweza wakatufikisha mahali ambapo tunapataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Regina, wajiandae Mheshimiwa Kwezi na Mheshimiwa Halima.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hii bajeti ya TAMISEMI. Kwanza nianze kwa kupongeza Ofisi hii ya TAMISEMI ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri wetu Mchengerwa pamoja na Waheshimiwa Naibu Mawaziri wake wote wawili. Nimpongeze vilevile Mheshimiwa Zainab Katimba kwa kuteuliwa na tunaamini anaweza kazi, tunamtakia kila la kheri, akachape kazi, yeye bado ni kijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan toka ameingia madarakani ni miaka mitatu sasa, lakini kila Mtanzania ni shahidi ni kwa namna gani Mheshimiwa Rais ameendelea kufanya kazi na kuhakikisha kwanza miradi inaenda mpaka chini kwenye maneo ya vijiji vyetu. Kwa hiyo, nimtie moyo Mheshimiwa Rais kwamba aendelee kufanya kazi, sisi akinamama pamoja na Watanzania tuna imani kubwa kwamba Mama bado anaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na *TARURA*, kwanza niipongeze *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana, lakini bado kulingana na hali iliyopo mwaka huu, tunayo changamoto kubwa. Changamoto hii nitaisemea kwa upande wa mkoa wangu. Mkoa wetu kijiografia ulivyo kwanza kwa upande wa barabara tupo nyuma sana, maeneo mengi barabara bado tupo nyuma barabara zetu bado ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia taarifa ya Kamati, Kamati ilikwenda kukagua miradi katika mkoa wetu, tunayo barabara ya Nakwa ambayo inatakiwa ijengwe katika kiwango cha lami. Ipo Babati Mjini, barabara hii ni urefu wa kilometa tisa, lakini mpango wa Serikali ni kwenda kujenga barabara kwa awamu tano na mpaka sasa barabara ile imejengwa kilometa 0.7. Kwa unyeti wa barabara hii naomba ichukuliwe kwa umuhimu kwa sababu barabara hii inatoka Babati Mjini inakwenda Babati Vijijini, lakini barabara hii inakwenda mpaka Katesh Wilayani Hanang.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunapozungumza hapa kuna barabara zinatoka vijijini kwenda kuungana na barabara hii ambayo ni kilometa tisa, Mjini Babati inayotakiwa kujengwa kwa kiwango cha lami, maeneo mengi hayapitiki kwa sababu ya mvua kunyesha. Tunaelekea msimu wa kwenda kwenye mavuno hata wananchi wetu wakivuna hawawezi kwenda kufanya biashara mjini na wananchi wengi katika maeneo yetu wanategemea kufanya biashara zao mjini na hata mahitaji yao wanayapata Babati Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji leo hii mvua ikinyesha pikipiki haipitiki, bajaji haipitiki wala gari halipitiki katika maeneo hayo. Changamoto iliyopo hata leo mama akipata uchungu kwa sababu hospitali wanayotegemea ni hospitali ya Babati Mjini hawawezi kwenda. Wapo akinamama walijifungulia barabarani kipindi hiki cha mvua na wapo watu walipoteza maisha katika kipindi hiki cha mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana Ofisi ya TAMISEMI, hii barabara inayotoka Babati Mjini kuelekea maeneo ya vijijini ikiwepo Kata ya Riroda mpaka kwenda Katesh iwekewe kipaumbele ili kuokoa maisha ya watu wetu, lakini kurahisisha na kupandisha maendeleo katika maeneo yetu. Mheshimiwa Rais alifanya jitihada kubwa sana kujenga vyumba vya madarasa mengi tu katika maeneo mengi, lakini bado kuna maeneo yanahitaji kufanyiwa kazi hasa maeneo yenye msongamano mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano tunayo sekondari yetu ya Mkapa katika eneo la Mji wa Mererani. Sekondari hii ninapozungumza hapa ina wanafunzi 1,400, ina walimu 23, lakini ina vyumba 13 tu vya madarasa. Nishukuru Serikali imepeleka 56,000,000 na sekondari hii imekubaliwa kupandishwa hadhi kuwa na kidato cha tano na cha sita, mwaka huu ndiyo inakwenda kuanza, lakini hofu yetu ni kwamba hao wanafunzi wanakwenda kusomea wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna madarasa mawili ya kuanza *form five* na *form six* lakini hakuna bwalo, hakuna bweni, walimu hatuna sasa tunaenda kufanya nini pale katika sekondari ile. Kwa hiyo, naomba Serikali ituongezee fedha katika shule hii ya Sekondari ya Benjamin Mkapa iliyopo Mererani ili kuona namna gani wanafunzi wetu wanaweza kuishi pale, wanafunzi wanapata madarasa ya kutosha, lakini pia na kupata wanafunzi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna wingi wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Mererani, shule kongwe ya Mererani. Shule hii ina wanafunzi zaidi ya 1,102, lakini tatizo lipo pale

pale hawana madarasa ya kutosha, kuna msongamano mkubwa wa wanafunzi madarasani. Kama tunavyofahamu huwezi kufundisha darasa lenye wanafunzi 200 wakaelewa. Kwa hiyo ni lazima tuangalie ku-*balance* tunapo- *enroll* wanafunzi katika shule zetu ikiwa ni pamoja na kuangalia *resource ability* tuliyonayo, kwamba tuna *access* ya vyumba vingapi vya madarasa ili kuona kwamba kila mwanafunzi anaweza kuingia darasani na akamsikiliza mwalimu. Bila kufanya hivyo tutaendelea kuingiza wanafunzi mashuleni, lakini mwanafunzi anaweza akasoma darasa la kwanza mpaka la saba na hajajua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo na Waheshimiwa wengi wameshalisemea hili na mimi niseme tu kwamba, kwenye Mkoa wangu kuna shule kongwe nyingi ambazo zimeanzishwa kabla ya uhuru. Shule hizi ukienda huwezi amini kama mwanafunzi amekaa darasani, kwanza wanafunzi waliopo darasani wanahatarisha maisha kwa sababu shule zenyewe zipo katika hatari ya kuanguka. Shule yenyewe unakuta madirisha yamefanana na milango, mwanafunzi anaingilia dirishani, mwingine anaingilia mlangoni. Kwa hiyo, niombe programu ya Serikali ya kwenda kuhakikisha kwamba zile shule kongwe zinakwenda kuboreshwa na kuwa katika hali nzuri na kujenga shule mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sasa Serikali, iliweza kujenga madarasa ya kutosha, leo hii tuna madarasa ya kutosha katika shule nyingi, lakini tukumbuke kwamba kulingana na jiografia iliyopo katika Mkoa wangu, hivi ninavyozungumza kuna baadhi ya Kata hazina kabisa sekondari wanategemea sekondari zilizojengwa kwenye tarafa. Sekondari zilizopo kwenye tarafa zinafanya mwanafunzi atembee umbali wa kilometa 80 kwenda kwenye shule hizo. Hivyo, inawalazimu kwanza waanze maisha ya geto, lakini wengine wanaishi kwenye hosteli bubu ambazo hazina usalama. Ukosefu huu wa hosteli unasababisha wanafunzi wengi kuacha masomo, wanafunzi wengi wa kike kwenda kuolewa na wanafunzi wengi wa kike kubebeshwa mimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na hili na watoto wetu wasome vizuri, niombe sasa liwekewe kipaumbele suala la ujenzi wa mabweni katika shule zetu na naomba hili lianze hasa na Mkoa wangu wa Manyara kwa sababu mazingira mengi tuliyonayo ni jamii ya kifugaji, ni mazingira ambayo bado maendeleo ya elimu yapo chini. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri alichukue na watupe kipaumbele ili watoto wetu wa jamii ya kifugaji waweze kusoma na wawe na maisha mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi, nashukuru Serikali inaendelea kutoa ajira mwaka hadi mwaka, nimwombe Mheshimiwa Waziri katika ajira hizi tuangalie zile shule ambazo wapo vijana ambao wamejitolea kwa muda mrefu katika shule hizo na katika vituo vyetu vya afya. Vijana hawa wamejitolea kwa miaka mitano wengine mpaka miaka saba, mpaka wengine wamekata tamaa na kuacha kabisa. Niombe sasa kipaumbele kianze pale, Serikali iwe na *database* ya watu wanaojitolea ili wapewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ushauri sasa katika Ofisi hii ya TAMISEMI, suala zima la makusanyo ya mapato, naiomba Serikali ione namna gani inahakikisha kwamba kunakuwa na mfumo wa eletroniki katika ukusanyaji wa mapato katika halmashauri zetu hasa katika vijiji vyetu. Tukiweka mfumo huu ukusanyaji wa mapato wa ndani utakuwa wa kikamilifu lakini kutakuwa hakuna wizi. Siku hizi ukienda kwenye vijiji vyetu tuna *M-PESA* kuna *Airtel Money* kule, tuachane na risiti twende kwenye eletroniki, watu walipe kwa *control number* ili tuweze kukusanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba halmashauri zetu zipewe elimu ya kuanzisha miradi ambayo ni chanzo cha mapato siyo ya kikodi ili hata kodi ikifutwa halmashauri haiwezi kutetereka wataendelea kufanya kazi kwa sababu wanakuwa na mapato, badala ya kutegemea chanzo cha kikodi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, kuna suala zima la mabinti wetu ambao Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan ili kuona kila binti wa Kitanzania anaenda kutimiza ndoto zake aliamua kuwarudisha waendelee na masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vituo niombe Mheshimiwa Waziri waviangalie, vituo hivi kama dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kila Mtanzania anatimiza ndoto yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kwezi, wajiandae, Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Kilave na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, hayupo ataingia Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi watabadilishana nafasi.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwasilisha mchango kwenye bajeti yetu hii ya Ofisi ya TAMISEMI. Awali ya yote, naomba nisiwe mchoyo wa fadhila, nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, lakini najua kuna taasisi kule inaitwa *TARURA* binafsi kwa kweli tunamshukuru sana Mtendaji Mkuu pale, ni Mtendaji makini sana tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kaliua, Jimbo lenye wapiga kura 400,000 na Jimbo linaloongoza kwa idadi kubwa ya watu katika Mkoa wa Tabora ambao ni Mkoa wa tatu, kufikisha shukrani za dhati za wananchi wa Jimbo lile kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Jimbo la Kaliua aliyoyafanya ni makubwa na ni maajabu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana kwa sababu Mheshimiwa Rais ametutendea mema kwenye barabara, ameweza kubadilisha *ceiling* ya bajeti yetu ambayo ilikuwa ni shilingi

922,000,000 mpaka karibu shilingi 4,000,000,000 kwa mwaka. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ameweza kutusaidia kwenye masuala ya madarasa, Jimbo la Kaliua hivi ninaongea miaka mitatu ya Mheshimiwa Dkt. Samia tumeweza kujenga shule mpya tisa. Katika shule mpya tisa, shule ya Mkoa yenye thamani ya shilingi bilioni nne imejengwa katika Jimbo la Kaliua, ndiyo maana nasimama kifua mbele kusema kwamba tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hapo tu, Jimbo la Kaliua lenye idadi kubwa ya watu zipo Kata ambazo hazikuwa na vituo vya afya, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Kwa mfano, ipo Kata inaitwa Usinge, Kata ya Usinge ndiyo Kata ya pili yenye idadi kubwa ya watu, watu 70,000, nadhani Kata hiyo tu ukiangalia unaweza ukaona ni sawa na majimbo mengine, mheshimiwa Rais ameweza kutupatia fedha tukakamilisha kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Igagala yenye watu 46,000, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kutusaidia tukaweza kujenga kituo cha afya na tayari kimekamilika na huduma zinatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kupitia mapato ya halmashauri tumeanza ujenzi wa vituo vya afya viwili, Ukumbisiganga yenye watu 24,000, kituo cha afya kinaendelea na bado Ugunga tumeanza. Nina ombi kwa Mheshimiwa Waziri kwenye kituo cha afya, kwanza kabisa nimpe pole kwa kweli mimi mwenyewe niwaambie wananchi wa Kaliua nawapa pole sana kwa sababu tayari tunavyozungumza kuna nyumba zaidi ya 250 zimedondoka juzi, lakini ukiangalia barabara sehemu kubwa zimekatika, si kwamba Mheshimiwa Rais alikuwa hajatusaidia alikuwa amefanya mapinduzi makubwa sana kwenye hizi sekta. Kwa hiyo, nadhani mvua ni neema tushukuru tu, lakini kwetu sisi kwa upande mwingine kama ilivyotokea kwa Mheshimiwa Waziri, tumpe pole lakini madhara ni makubwa, lakini hatuna namna tuendelee kusimama na kuwafariji wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu Kata kubwa kabisa yenye idadi kubwa ya watu ina watu 73,000, kata hiyo inaitwa Igwisi. Sasa hii Kata ndiyo ya kwanza kuwa na idadi kubwa ya watu, tulipeleka orodha pale watusaidie ili tuweze kupata kituo cha afya. Watu 73,000 kukaa bila kituo cha afya kwa kweli, kidogo tunakuwa hatufanyi vizuri. Nimwombe kwa heshima zote kwa sababu sisi tumeanza kwa mapato ya ndani, Ugunga pamoja na Ukumbisiganga, tuipatie Igwisi kupata kituo cha afya ili ku-*cover* hii idadi kubwa ya watu pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwenye upande wa barabara, mimi kidogo hapa nitaishauri Serikali. Katika ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ametuambia kwamba 45% ya fedha ya *TARURA* ndiyo ambayo imefika, nikawa najiuliza hivi Hazina kuna shida gani? Fedha ya barabara ambayo sisi ndiyo uchumi na ndiyo tunayoitegemea, TAMISEMI wamepeleka *TARURA* 45%! Waheshimiwa Wabunge nataka niwashauri kitu hapo, 45% tunaongea bado miezi miwili mwaka ukatike, hizi fedha tulizozipanga mwaka mzima kwenda *TARURA* Wizara ya Fedha wameziweka wapi? Miongoni mwa vyanzo vyake ni pamoja na mafuta, sasa shida ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, 45% ukitoka mwezi Julai tarehe Mosi mpaka mwezi wa Juni mwaka huu tunakwenda kumaliza mwaka, tunataka ile 55% iliyobakia tuweze kukamilisha barabara zetu. Kwa hiyo, kwenye jambo hilo nimwombe Mheshimiwa Waziri, najua yeye ni mchapakazi, watu wanamwita mtu kazi, nimwombe sana, akabe hizi fedha, ahakikishe zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nje ya hili kwenye barabara ambalo ni ombi langu kubwa ni hii bajeti ya dharura. Jamani kwa kweli barabara zimekatika sana, Mheshimiwa Waziri aelewe, wananchi wetu, mazao yao yanapita kwenye maji mpaka sasa tunavyoongea. Kwa hiyo Serikali lazima wajipange kuja na majibu ya kutosha kwamba ile *emergency fund* iende *TARURA* ya kutosha ili wananchi waweze kunufaika na fedha hizi. Hatuna wasiwasi na matumizi ya *TARURA*, tunajua Mtendaji Mkuu sijui kwa sababu

alikuwa *TANROADS the best man* pale anafanya kazi nzuri sana, nimkumbushe tu Mtendaji Mkuu asisahau zile kilometa tatu Kaliua za lami wanazisubiri wananchi wa Kaliua, Wanyamwezi wale kwa hamu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashauri jambo lingine ambalo ni kubwa sana. Jambo hili sitaki kulisema sana, nusu ya watumishi katika nchi yetu wapo kwa Mheshimiwa Waziri, tena ni zaidi ya nusu, kwa sababu akipiga halmashauri *almost* anaweza akakuta kuna 3,000,000 au 3,500,000, kadhaa aki-*cut across* anakuta ana watumishi zaidi ya 400,000. Sasa kama ndivyo ilivyo namshauri Mheshimiwa Waziri asimame kwenye jambo hili, walimu wake kule kwa kweli niseme wale wastaafu tusiwakatishe tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la kikokotoo walipitie upya, kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu ni msikivu na yupo tayari, shaka ni nini? Nimwambie Mheshimiwa Rais, atembee kifua mbele, nitampa mfano mdogo sana, sisi kule wafuga kuku huwa kuku anataga mayai mengi sana, lakini anapototoa yale mayai, kuna mayai mawili matatu yanabaki pale, sasa asiogope yale maneno ya yale mayai yaliyo baki baki pale, *they have nothing to do!* Yale aliyoyafanya ni *wonders*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemtajia Mheshimiwa Waziri takwimu za madarasa kwenye jimbo langu yaliyojengwa katika kipindi cha miaka mitatu ni madarasa 404, ni bilioni ngapi hizo? Shule za msingi karibu sita na sekondari tisa, vituo vya afya vinaendelea vine, hivi tunataka tuseme nini? Tunaogopa nini kama ni jimbo lenye vijiji 55 umeme tumebakiza vijiji viwili, *distribution* inaendelea tuna haja gani ya kuogopa? Kwani wananchi hawajui kama ni mvua, si wanafahamu, twende kazi! Naomba nimtie moyo Mheshimiwa Rais kwenye jambo hilo asikate tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni la shule chakavu za msingi, naomba sana tuziangalie shule za msingi maana yake tume-*concentrate* kwenye sekondari lakini kuna shule za msingi ambazo hata sisi tumesoma. Shule ya Msingi Kazaroho, Shule ya

Msingi Usimba, Shule ya Msingi Igwisi, Shule ya Msingi Ulindwanoni aliposoma Mzee wangu Profesa Juma Kapuya, Mheshimiwa Waziri mstaafu aliyetumikia nchi vizuri na zenyewe zimechoka kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba waziangalie zile shule kongwe za msingi angalau hata kumi siyo mbaya tutakwenda vizuri. Binafsi nataka niseme yale yaliyofanyika na Mheshimiwa Rais kwani tulikuwa na Mfuko wa Jimbo ambao tunapewa milioni 500, 500 iliwahi kutokea, kwa hiyo sisi hatuoni ni kwa nini tunashindwa kuwaambia kule? Tunapelekewa milioni 500 ambazo tunazipanga sisi, tunakaa na Madiwani wetu hii milioni 500 Waheshimiwa Madiwani kwa niaba ya wananchi wetu tunapeleka wapi, wanasema hapo piga lami, wanasema hapa piga kitu fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwathibitishieni hilo, kazi iliyofanyika kwa kweli haki ya Mungu *I swear,* siwezi ku-*compare* mimi binafsi, lakini nakiri mbele ya Mungu kwamba kazi iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan *it has never happen,* kwa hiyo wasiwepo watu wanaom-*demoralize* Mheshimiwa Rais na kama wapo wajichukulie ndiyo yale mayai yaliyobakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema mengi, lakini na maombi yangu yote nimeyawasilisha hususan lile la kikokotoo la watumishi wangu wa Kaliua na watumishi wa nchi nzima. Wapo pia wengine na kwa sababu najua Serikali ni sikivu, jambo hilo najua limekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nimalizie kuwapongeza sana nyie wote, lakini nimpongeze sana Mkuu wangu wa Wilaya Rashid Chuachua. Mheshimiwa Rais, pale anaye mwakilishi sahihi, lakini nimpongeze sana Mkurugenzi wangu wa Wilaya ya Kaliua Jerry Mwaga. Kama mnahitaji kuja kujifunza na kama mlivyoona ile shule ya bilioni nne iliisha *on time* njooni Kaliua. Kuna vitu ambavyo mtajifunza, mambo ni mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawatolea mfano mdogo tu kwenye lami. Mheshimiwa Rais amenipa kilometa saba na nusu

kwenda Singa, hivi nani ananishawishi nimseme vibaya? Pale Kaliua Mjini hatukuwa na lami, sisi tumejenga kilometa 21 na taa za barabarani kilometa nane. Sasa nani kayafanya kwani lami zilikuwepo Kaliua? Sasa kwa nini tusimshukuru Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ni *proud* kuwa na mama, ni *proud* kumsemea Mheshimiwa Rais kwa mazuri yote aliyoyafanya. Mimi niwahakikishieni Kaliua iko wazi, njooni mjifunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee, wajiandae Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mheshimiwa Shekilindi, Mheshimiwa Bilakwate na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nitajikita zaidi kwenye ukurasa wa 89 hadi 91 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inayozungumzia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi wakizungumzia usimamizi wa mikopo ya 10%. Nime-*highlight* maeneo kadhaa, eneo la kwanza, utaratibu kuanza Julai, 2024 kwa halmashauri 10 za majaribio kupitia benki, halmashauri nyingine 174 kwa mfumo ambao inasemekana umeboreshwa kwa kuanzisha kamati mbalimbali za mkoa mpaka ngazi ya kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni ajira kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wapya 787 ambayo inaaminika uwepo wao utasaidia zoezi hili liende vizuri zaidi. Mwisho, ni Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kurekebisha sheria inayosimamia mikopo hiyo na kanuni zake ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii sentensi ya mwisho inanionesha kwamba sasa hivi tuko kwenye Bunge la Bajeti. Muda ambao mchakato huu utaanza maana yake ni kuanzia tarehe Mosi, Julai mwaka mpya wa fedha. Wakati huo huo wakati tunaenda

kuanza mpango mpya kumbe TAMISEMI haijarekebisha sheria, kanuni wala taratibu ambazo tunatarajia ziweze kusimamia huu mchakato. Kwa hiyo, pamoja na umakini wa Waziri unaosemwa, hotuba yake inaonesha kwamba tumekurupuka kwenye hili jambo. Hatujajiandaa na ndiyo maana hatuna sheria *in place,* hatuna kanuni *in place* ili hizo kanuni ziweze kutoa mwongozo na maelekezo kwa hivi vitu vipya ambavyo tumesema tunaviunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Angellah Kairuki alizungumza na hapa ninazungumzia ile mikopo chechefu haijalipwa. Mheshimiwa Waziri kwa makusudi najua kwenye hotuba yake hajaandika kabisa chochote kuhusiana na mikopo chechefu. Naamini kwamba fedha za wananchi ni fedha ambazo lazima ziwe *accounted for,* hawezi kufunika kombe ili mwanaharamu apite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka wa fedha uliopita 2021/2022, ilikuwa inaonesha wazi kabisa katika halmashauri 180 shilingi bilioni 88 zilikuwa hazijarejeshwa. Hiyo ilikuwa ni ripoti ya mwaka jana na ni ripoti hiyo iliyopelekea kusitishwa kwa muda, ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hapa tutasitisha kwa muda ili tuunde kikosi kazi cha wataalam kitakachotoa mapendekezo ya utoaji mikopo na urejeshwaji. Kazi ikikamilika itawasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi ili tupate uelewa wa pamoja. Leo mwaka mmoja baadaye tunakuja tunasomewa kwenye hotuba vitu havieleweki bila kujua kikosi kazi kilichofanya kazi kiligundua nini, changamoto ni nini na tunaelekea mbele vipi. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, aliyekuwa Waziri mwaka jana baada ya Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alisema hapa Bungeni na ilikuwa mwezi Aprili kwamba tunatoa maelekezo kwa wakurugenzi wote wa halmashauri zote ndani ya miezi mitatu, mikopo ile ya shilingi bilioni 88 ambayo tunaita chechefu, ziwe zimekusanywa zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Julai mpaka tunaahirisha Bunge hakusema kitu. Mwaka mmoja baadaye hakuna kitu ambacho kimefanyika, mwezi…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana, naomba ni…

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, natambua mchango wa Mheshimiwa Halima Mdee lakini naomba nimpe taarifa kwamba baada ya kusitishwa kwa mikopo ya 10% mwaka jana April, Kamati ilifanya kazi yake kama alivyosema, ilileta ripoti tukagundua sababu na ndizo ambazo zimetumika kuandaa mpango mpya ambao tutaanza kutumia Julai mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kwamba fedha ambazo zilionekana kwenye ripoti ya *CAG*, shilingi bilioni 81 ambazo zilikuwa hazijarejeshwa, mpaka Machi 30 shilingi bilioni 63 zimesharejeshwa na ziko kwenye akaunti za halmashauri zitaungana na zile zilizotengwa kwenda kukopesha. Kwa hiyo, naomba nimpe taarifa hiyo kwamba kazi inaendelea vizuri na tutahakikisha tunarudisha fedha zote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mdee, taarifa hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mawaziri watulie ili wawe wanatujibu wakati wakitakiwa kutujibu. Nilisema hivi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hapa baada ya kikosi kazi kufanya kazi yake wataleta taarifa Bungeni na kuweka wazi

kwa wananchi ili tujue *findings* tuweze kushauri, ili tutoke na kitu bora, lakini hakuna kilicholetwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC,* sijui chochote. Nina uhakika yuko hapa mjumbe wa Kamati ya USEMI, hajui chochote. Wanatoka huko wanakuja kutupa hotuba ya jumla jumla ambayo haieleweki, hilo la kwanza. Kwa nini nasema haieleweki? Tukiwa tunaongea taratibu wakiwa wanatu-*interrupt* wanatupa mizuka. Hii Sheria ambayo tunaitekeleza sasa ina kanuni zake za mwaka 2019. Kuna kanuni zingine zilifanyiwa *amendment* mwaka 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kanuni ambazo zimetufikisha hapa kulikuwa kuna utambuzi wa vikundi kuanzia ngazi ya Mtendaji wa Kijiji, Mtendaji wa Kata, unakuja Mkurugenzi na Menejimenti yake, unakuja Kamati ya Fedha Halmashauri, unakuja Mkutano Mkuu wa Baraza la Madiwani, unakuja TAMISEMI yenyewe unakuja mikoa. Hivi vitu vyote viko hapa. Sasa kama mli-*fail* katika muktadha huu ndiyo maana tunasema, kwa nini hawakuleta hizo *findings* ili tujue kinagaubaga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, nina Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Machi, 2024, ukurasa wa 103 inasema; "Mikopo ambayo haijarejeshwa kutoka kwenye vikundi ni shilingi bilioni 79.76." Ili nikusaidie nenda kwenye kielelezo kinaitwa kiambatanisho namba 27 kimechambua halmashauri zote 149 ambazo zina hii *query* maana tunazo halmashauri 184. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema, mikopo ya muda mrefu ambayo ndiyo hoja yangu hapa ya msingi, sizungumzii ile pesa ambayo iko kwenye mzunguko inarejeshwa kawaida, nazungumza mikopo ya muda mrefu shilingi bilioni 79.7. Maana yake katika ile 88 mwaka wenu mzima wote waliweza kurudisha nane tu, sijui saba ndiyo maana zikabaki 79. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema mikopo mipya ya 2022/2023, wasisahau kwamba walizuia mwezi Aprili, 2023 lakini wakati huo mwaka wa fedha 2022/2023 tayari ulikuwa umeshaanza. Kwa hiyo, kuna watu waligawiwa na shilingi bilioni zaidi ya 75 zilitoka. Katika hizo fedha tunaambiwa mikopo mipya bilioni 27.6 ambayo ilitakiwa irejee haijarejea. Kwa hiyo, jumla ya pesa ambazo ziko nje ni shilingi bilioni 107. Sasa tunajiuliza tunaenda kwenye huu utaratibu mpya, utaratibu huu mpya kwenye hizi halmashauri 174 mnazozisema hauna tofauti na wa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ndugu zetu wa Dar es Salaam hawa, mimi natoka Dar es Salaam, kwangu kule Kinondoni wanadaiwa zaidi ya shilingi bilioni sita, wametoa kumi na tano, 6.2 ziko mtaani. Temeke kwa dada yangu hapa…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya pili mtu mmoja?

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Halima Mdee kwamba, kwanza akumbuke hiyo *reference* ya mikopo ya 2022/2023 si mikopo yote inayorudishwa ndani ya mwaka mmoja wa fedha. Kwa hiyo, kuna mikopo ambayo bado muda wake wa ku-*mature* unaendelea na Serikali itaendelea ku-*recover* mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, utaratibu wa sasa utakaoanza Julai, 2024, si sawa na utaratibu uliopita na ndiyo maana kuna ajira za Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kutakuwa na

Kamati za Mikopo za Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji, lakini tumeajiri wataalam wengi. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba utakuwa bora kuliko ule uliopita.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo vitu anavyovizungumza akasome kanuni. Unajua tatizo letu hatuna utamaduni wa kusoma. Wakati mimi nazungumza *total* ya hii shilingi bilioni 107, nilizungumza kuna hii mikopo ya zamani na kuna hii mikopo mipya. Lazima wajifunze kuelewa na ndiyo maana tunasema utaratibu huu nadhani, Waziri amekiri kabisa kwamba mpaka sasa hakuna sheria wala kanuni. Anatoaje miongozo wakati hana msingi wa kumwongoza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, kengele ya pili, ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, kengele ya pili, uandike…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu yakiwa yanajibiwa…

**NAIBU SPIKA:** Utaratibu unaandika kwa Waziri, ndiyo utaratibu wetu, kaa chini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili niweze kuongea kuhusiana na TAMISEMI. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameweza kunifanya niwe na afya na kusimama mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu wa TAMISEMI pamoja na Naibu Mawaziri wote. Mimi ni mjumbe ndani ya Kamati ya TAMISEMI, hivyo nafahamu kazi nzuri wanazozifanya kwa jinsi ambavyo wanakuja na kutusikiliza na hata kuchukua maoni mengi tu ambayo yanaenda kufanyiwa kazi. Hivyo, niwashukuru na kuwapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Temeke wamenituma salamu kubwa sana na nzuri sana kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Salamu hizi ni za pongezi na shukrani. Kwanza tunampongeza kwa kazi nzuri sana anayoifanya katika Nchi yetu yote ya Tanzania na tumeona jinsi gani ambavyo amekuwa ni mama ambaye ni mnyenyekevu, mtiifu na ameweza kufanya mambo mengi ambayo ameyasikia kutoka kwa wananchi wake na hata sasa yanafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe pongezi nyingi sana kwa jinsi ambavyo amefanyia kazi Jimbo letu la Temeke. Wananchi wa Temeke wanamshukuru sana na pongezi kubwa sana kwake na kumtia moyo haya yanayopita ni mambo ya zamani na asitie maanani kwa sababu sisi Wanatemeke tunasema Mama kwanza na miaka mitano zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi kwa kweli nadhani mimi pamoja na ninyi Wabunge wenzangu tunastahili sana kuzisemea kila tunaposimama na kila tunapofanyiwa jambo jema ambapo Mheshimiwa Rais wetu amekuwa ni mfano. Sisi kwetu Temeke kwa miaka yake hii mitatu tunaweza kusema hakika kazi hii aliyoifanya ndani ya Jimbo letu la Temeke, sisi tunamshukuru na tunazidi kumwombea dua siku hadi siku aendelee kuitumikia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na suala zima la afya. Ndugu zetu kama mnavyojua sisi Temeke tunazaliana sana, lakini tumekuwa na vituo vya afya pamoja na zahanati. Nina kata 13 na katika kata hizi nadhani nimebakiza kata mbili tu kupata zahanati

nazo ziko tayari zinaanza kutengenezwa. Nimshukuru sana mkurugenzi pamoja na Mkuu wetu wa Wilaya kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi nzuri ili tuweze kuendelea kupata hizi zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ametuletea zahanati kubwa tatu. Zahanati moja niliiulizia hapa asubuhi, Zahanati yetu ambayo tumezoea kuiita Malawi iko Yombo Vituka ambayo wametuahidi hapa kwamba watatuletea jengo la dharura. Kwa hiyo, nishukuru sana kwa zahanati hiyo ambayo sasa hivi ni zahanati kubwa katika Jimbo letu la Temeke. Pamoja na kwamba tuna Hospitali ya Temeke, lakini Jimbo letu la Temeke, hospitali hii ambayo ni Kituo cha Afya cha Malawi kinafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuletea sisi Wanatemeke Kituo cha Afya cha Buza, *specific* mama na mtoto. Kwa hiyo, sasa hivi tunasema hata kule Temeke tumepungua sana kwenda kuzalia Temeke, tunazalia kwetu wenyewe pale Buza. Kwa hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi ambavyo anaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu juzi wametuletea vifaa vingi sana katika Kituo chetu cha Afya Kilakala. Hivyo, nizidi kusema kwa kweli kwa jinsi ambavyo mama huyu anafanya kazi pamoja na Ofisi yake ya TAMISEMI, nampa pongezi na *big up* sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sana kuhusiana na elimu. Kama nilivyosema sisi Wanatemeke tuko wengi nadhani ni jimbo la tatu au la nne kwa nchi nzima kwa kuwa na watu wengi, lakini niseme ukweli shule za sekondari tumepata. Tena najivunia kwa sababu tunajenga shule za sekondari za maghorofa. Hivyo, tunamshukuru sana na tunashukuru kwa Wizara kwa kutupa vibali kwa sababu tunajua hata mazingira yetu ya Temeke hatuna nafasi za kujenga shule za msambazo, lakini tumepata jinsi gani ya kuweza kujenga kwa maghorofa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nafasi ni chache, lakini tunatamani sana tuendelee kupata hizi shule za sekondari ambazo katika Jimbo langu katika kata 13 nimebakiza Kata ya Makangarawe. Niombe sana, pamoja na Kata ya Chang'ombe hatuna shule za sekondari lakini tayari tuna eneo la kujenga shule hizi za sekondari. Hivyo basi, Mheshimiwa Waziri, nikuombe sana, sisi tuko tayari na tumepata eneo, tunaomba sana fedha za kuendelea kujenga sekondari zetu hizi za Jimbo la Temeke katika Kata ya Makangarawe pamoja na Chang'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na maji. Niseme kuhusiana na maji tumefikia karibu 85% ambayo tunayo maji ndani ya Jimbo letu la Temeke, kwa hiyo, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu *TARURA*. Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kushusha fedha nyingi za barabara ambazo hata sisi zimetukuta wananchi wa Jimbo letu la Temeke. Fedha ni nyingi na kweli barabara tumeziona zinatengenezwa. Nakushukuru sana kwa jinsi ambavyo *Engineer* Seff kwa kutusikiliza. Si hilo tu, watendaji wako wa Mkoa wa Dar es Salaam, watu wa *TARURA,* Mkoa wa Dar es Salaam wamekuwa ni watii na wamefanya kazi nzuri sana na kupelekea Temeke yetu kupata fedha za kuweza kujenga barabara za *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* wamekuwa ni msaada mkubwa sana katika Jimbo letu la Temeke. Tumeweza kuunganisha kata kwa kata hata vile vituo vya afya ambavyo tulikuwa tunapita kwenye barabara ambazo hazipendezi sana lakini sasa hivi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fedha alizozishusha kuhusiana na *TARURA*. Watu wa *TARURA* ndani ya Jimbo la Temeke hasa *Engineer* wangu Paul Mhere anafanya kazi nzuri pamoja na timu yake nzima ya Jimbo lile la Temeke. Namshukuru sana kwa sababu amekuwa ni kiunganishi na amekuwa akisimama sana na Madiwani wetu wa Jimbo la Temeke na kufanya nao kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, niombe sasa, ziko barabara ambazo ni chache tunatamani ziweze kupitiwa na haiwezekani bila

kuongezewa fedha, fedha hizo walizopewa *TARURA* ni chache sana. Tuliomba hapa na nasimama kuomba tena kwa ajili ya *TARURA* kwamba waongezewe fedha ili tuone mambo mazuri yanaendelea kufanyika. Kwa sababu kwa fedha hizi chache wameweza kufanya makubwa, je, tukiwaongezea fedha? Nadhani na naona mbele yetu iko vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzoni Mheshimiwa Rais anaposikia haya anafurahishwa kwa sababu tunaomba fedha ziweze kuongezeka ili sasa *TARURA* watengeneze barabara hata kama kuna mvua zitakazokuja miaka inayokuja, basi barabara zetu ziwe imara na ziweze kupitika wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumwa na ndugu zangu Wanatemeke na nimesimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Temeke. Siombi majosho, mbolea, mbegu wala *scheme* ya umwagiliaji. Nimekuja hapa la kwanza naomba barabara, tunaomba tena barabara, tunaomba barabara, mara tatu. Barabara zetu ziwe unganishi katika kata zetu zote 13 pamoja na zinazotuzunguka. Hivyo basi, niombe sana fedha hizi za *TARURA* zikiongezwa, Jimbo letu la Temeke tuongezewe fedha ili tuweze kumalizia barabara zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho walilonituma hapa, Wanatemeke wanauliza kwamba, je, Mradi wa *DMDP* unakwenda kuanza lini? Hilo ni swali kubwa kabisa ambalo hapa nimetumiwa *message* nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba niishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo wameweza kusikia namna ambavyo tumeisemea sana *CSR* hapa ndani ya Bunge. Niishukuru Serikali yangu kwa sababu wamekuwa wasikivu. Pia, wamesema wamesimamisha baadhi, kama vile hapa Dodoma, wamesimamisha ule mradi usiendelee ili tuweze kuziangalia tena sheria zitakazoweza kufanya kazi ili tupate sheria ambazo zitatuwekea vizuri hii *CSR* ili tija na malengo mazuri kwa ajili ya miundombinu yapatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ila naomba wakumbuke kuwa, siombi mbolea bali naomba barabara. Ahsanteni sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi, wajiandae Mheshimiwa Bilakwate na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Ofisi hii ya TAMISEMI. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii inayoongozwa na Mheshimiwa Mchengerwa, mtu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kwani mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Nabii Mussa alikwenda kwa Mwenyezi Mungu akamwambia kwamba; "Naomba uniombee dua ili niweze kupendwa na watu wote." Mwenyezi Mungu akamwambia Nabii Mussa kwamba, "Hiki ulichoomba ni kitu ambacho sijakiumba." Mwenyezi Mungu akamuuliza Nabii Mussa kwamba, je, wewe si ni kiongozi, wewe si una wazazi, wewe si unaongoza watu wengi? Je, watu wote wananipenda?" Nabii Mussa akasema; "Hapana, hawakupendi." Basi Mwenyezi Mungu akamwambia; "Ni kitu ambacho hakiwezekani, sema nikuombee dua upendwe na watu wengi."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Rais, anapendwa na watu wengi sana na ndiyo maana kila anayesimama hapa anasema na kushukuru kama Mwenyezi Mungu alivyoshusha aya "*Man laa yashkur nnas laa yashkur Allah.*" Usiposhukuru watu, basi hata Mwenyezi Mungu hutamshukuru. Ndiyo maana kila anayesimama hapa anamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Naamini kila jimbo limepekewa miradi

mikubwa sana. Kwa hiyo, sina shaka na hilo na Mheshimiwa Rais asiwe na wasiwasi, apige kazi, sisi tupo tunamsemea, Wabunge wake wote, Mawaziri, Naibu Mawaziri, viongozi wote wanamsemea vizuri Mheshimiwa Rais na wote wapo na yeye, wala asiwe na wasiwasi. Hawa wachache ambao wanamsema vibaya ni asilimia ndogo sana, labda ni 0.05%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu amekwishabainisha tayari kwamba, wakati unaumbwa tayari anakuwa amekwishakuandalia maadui na maadui hao amekuandalia ili ujihami nao. Laiti kama hawa maadui wangejificha basi wangemuumiza Rais wetu, lakini hawa wameonekana moja kwa moja ili aweze kujihami dhidi yao. Kwa hiyo asiwe na shaka, tuko pamoja naye. Wanalushoto wamenituma nimwambie Mheshimiwa Rais kwamba, tunamshukuru sana kwa miradi mingi ambayo ameileta katika Jimbo la Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye mchango na naomba nianze na *TARURA*. Niendelee kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa pia nimshukuru Mheshimiwa Dugange, Mheshimiwa Zainab, *Engineer* Seff na watalaam wote, kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika pale Lushoto Mjini sasa hivi ni lami tupu, ule mji mzima umezungukwa na lami. Mheshimiwa Mchengerwa alikuwa pale Hija, sasa hivi ile Barabara kuanzia pale Hija – Utondolo kwenda mpaka kule halmashauri sasa hivi ni lami, tunateleza tu. Kwa hiyo, tunamshukuru sana na Mungu ambariki sana. Ndiyo maana tunasema *ahibbal-nnas maa tuhibbul-nafsika* yaani huangalii nafsi yako unaangalia nafsi za watu, Mheshimiwa Mchengerwa, mtu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, barabara zetu nyingi zinapitika isipokuwa kuna barabara chache tu. Barabara inayoanzia Malibwi – Kwekanga kupitia Makole – Ngwelo, ile barabara kwa sababu ya mvua imeharibika mno kiasi kwamba gari hazipiti na hivyo wananchi wangu hawafiki nyumbani kwao. Kwa

hiyo niombe hii nayo aiweke kwenye bajeti ya safari hii ili iweze kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Barabara inayoanza pale Gare kwenda Kwemashai hadi Lushoto, barabara hii imeharibika sana. Ninaposema Gare ndipo ninapoishi mimi, pale ninapoishi hata gari haiwezi kupita. Wananchi wanalalamika kuwa, wewe Mbunge unaishi hapa lakini barabara yako iko hivi, sisi tunafanyaje? Kwa hiyo rafiki yangu Mheshimiwa Mchengerwa, ni aibu Mbunge wake kukaa sehemu ambayo hata barabara haipitiki. Nimwombe sasa kwenye bajeti hii aiweke ili iweze kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna barabara ambayo inatoka Migambo kwenda Kifungilo. Kifungilo ni shule ya sekondari kubwa sana ambayo inajulikana Tanzania nzima. Sekondari ile kwa kweli imeleta chachu ya kiuchumi ndani ya Wilaya ya Lushoto. Niombe ile barabara nayo iwekwe kwenye bajeti ili iweze kupata fedha nayo iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna Barabara ambayo inatoka Ngulwi – Kwemsala – Kwabonda – Ndekai. Barabara hii anaishi aliyekuwa Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu. Mheshimiwa Shekifu hafiki kwake kwa sababu barabara ni mbovu sana, hii ni aibu. Tumuenzi mtu huyu ambaye amefanya mambo mengi sana na amelitumikia sana Taifa hili. Kwa hiyo, niombe barabara ile iweze kutengenezwa ili mzee wangu akienda nyumbani kwake afike bila wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara yetu ambayo inaanzia pale Migambo kupitia kwa Mzee wetu marehemu Mkapa kwenda sehemu inayoitwa Gare – Mmanyai; hii nayo naomba aichukue. Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wangu msikivu (mtu kazi), tunaomba atuongezee taa pale Lushoto Mjini kwani sasa hivi mji unapendeza kwa zile taa chache walizotupatia, lakini wakituongeza tukaanzia Doti mpaka Magamba, basi mji utapendeza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niende tena kwenye afya. Nashukuru tumepewa vituo viwili vya afya ambavyo ni Kituo cha Afya Kwekanga na Kituo cha Afya Ngwelo. Kituo cha afya Kwekanga kimekamilika, tumepewa shilingi milioni 500, lakini hiki cha Ngwelo tumepewa shilingi milioni 250, bado hatujapewa shilingi milioni 250 za kumalizia. Kwa hiyo naomba hii nayo Mheshimiwa Mchengerwa aichukue aiweke kwenye bajeti yake. Pia, tunamshukuru kwa kutupatia gari ya wagonjwa ambayo nimekwenda kuikabidhi kwenye Kituo cha Afya Mlola. Namshukuru sana na wananchi wanamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hiyo niliongea naye kwamba hospitali ya wilaya haina gari la wagonjwa na kama anavyofahamu, kwamba ile hospitali ya wilaya ni kubwa sana na inahudumia wilaya nyingine za jirani. Nimwombe sana Mheshimiwa Mchengerwa na niko chini ya miguu yake, tunaomba gari nyingine ya wagonjwa kwa ajili ya hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Lushoto haina Kituo cha Afya hata kimoja. Pale Gare, wananchi wamejenga Kituo cha afya lakini bado hakijakamilika na kwa sasa tumekifungua kama zahanati. Pamoja na kujaza fomu basi nimwombe safari hii kile kituo cha afya kiweze kutengewa fedha ili wananchi waweze kupata huduma karibu na wanapoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli bado watumishi wa afya ni wachache sana. Tunamwomba Waziri atuongeze watumishi wa afya pamoja na vifaatiba katika zahanati zetu na vituo vyetu vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye elimu. Rais ametupatia fedha nyingi sana za elimu. Ninaposema hapa, pale Lushoto kuna chuo tayari kimekwishafunguliwa. Chuo hicho kiko Mlola, Tarafa ya Mlola. Tumepewa fedha bilioni moja na milioni mia nane na ushee, sasa hivi watoto wetu wanasoma stadi za kazi. Kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna maboma yetu ambayo tumepewa fedha na yamekwisha. Kama Waziri anavyoifahamu Wilaya ya Lushoto ina shule nyingi za msingi na sekondari nadhani kuliko hata mikoa mingine. Kwa kuwa shule hizi ni chakavu mno. Nimwombe angalau nitaje shule chache au zote ili zikae kwenye *Hansard* ili Mheshimiwa Mchengerwa akitaka kuzichukua au kuzisaidia shule hizi basi anakwenda kuvuta *Hansard* inamwonesha kwamba hapa ni shule kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kutaja, shule ya kwanza ni Shule ya Msingi Kwemashai, Shule ya Msingi Kilangwi, Shule ya Msingi Chumbageni Ngulu, Shule ya Msingi Ngulwi, Shule ya Msingi Mzizi, Shule ya Msingi Gare "B", Shule ya Msingi Makanka, Shule ya Msingi Masange, Shule ya Msingi Kizara, Shule ya Msingi Kwabosa Miyegeyo, Shule ya Msingi Ubiri, Shule ya Msingi Mbula "A", Shule ya Msingi Kitopeni, Shule ya Msingi Lushoto, Shule ya Msingi Mihelo, Shule ya Msingi Kwembago, Shule ya Msingi Kwesimu, Shule ya Msingi Kwai, Shule ya Msingi Kireti, Shule ya Msingi Dindila, Shule ya Msingi Malibwi, Shule ya Msingi Ntambwe, Shule ya Msingi Mazumbai, Shule ya Msingi Nghaloyi, Shule ya Msingi Matego, Shule ya Msingi Kwekanga, Shule ya Msingi Mzimkuu, Shule ya Msingi Kwaboi, Shule ya Msingi Mkuzi, Shule ya Msingi Milunguyi, Shule ya Msingi Kweboma, Shule ya Msingi Makole, Shule ya Msingi Mbeleyi, Shule ya Msingi Hondelo, Shule ya Msingi Mlola, Shule ya Msingi Ndambo, shule shikizi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi, kengele ya pili, kaa chini. Sasa namwita Mheshimiwa Bilakwate na Mheshimiwa Jonas ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, wanafanya kazi kubwa

sana na kwa kweli Mheshimiwa Mchengerwa kila anapokwenda anapatendea haki. Vilevile kipekee tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, anafanya kazi kubwa, Watanzania tunaiona kwa sababu inaonekana kwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitatu ambayo nimekuwepo hapa Bungeni nilikuja kutafuta miradi na hii miradi siitafuti kwa mwingine bali naitafuta kwa Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu. Sasa, mwaka huu ni mwaka wa nne, hivyo nataka niseme kile ambacho Mama Samia amekileta Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze katika upande wa elimu msingi. Mama Samia, amejenga vyumba ya madarasa 99, matundu ya vyoo 385, majengo ya utawala matatu, nyumba nne za watumishi, shule mpya ya Mkunyu kwa shilingi milioni 540, Shule mpya ya Chanyangabwa kwa shilingi milioni 348. Kwenye upande wa elimu msingi, Mama Samia ameleta shilingi 5,762,000,000. Hiyo ni katika upande wa *primary*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa shule za sekondari. Mama Samia amejenga vyumba vya madarasa 185, amekamilisha vyumba 39, amejenga matundu ya vyoo 80, amejenga shule tatu mpya za sekondari kwa gharama ya shilingi 6,814,000,000. Mama Samia amekamilisha jengo la utawala kwa gharama ya shilingi 3,550,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija katika upande wa afya, Mama Samia amejenga nyumba ya watumishi kwa shilingi milioni 90, kituo cha afya kwa shilingi milioni 500, ameleta shilingi 1,100,000,000 kwa ajili ya kujenga wodi ya akinamama, wanaume na watoto. Ameleta vifaatiba kwa gharama ya shilingi milioni 750, amejenga maboma ya zahanati kwa shilingi milioni 200. Jumla ni shilingi 2,640,000,000. Kwenye upande wa barabara, kwa miaka mitatu Mama samia ameleta shilingi 8,388,000,000. Mama Samia, oyee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu nimesema kwamba, miaka mitatu nilikuwa natafuta fedha na nilikuwa nazitafuta kwa

Mama Samia ambapo kwa upande wa TAMISEMI fedha hii aliyoileta Kyerwa ni jumla ya shilingi bilioni 24 na hapa sijaongelea maji na miradi mingine. Kwa hiyo ndugu zangu tuna kila sababu ya kumpongeza sana Mama Samia kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaweza wakaongea. Hata hivyo, mimi niseme hivi, kazi aliyoiomba Mama Samia kwa Watanzania mojawapo ni kuwaletea maendeleo. Kazi hii ameifanya kwa uaminifu na naamini kwamba kama ameifanya kwa uaminifu, Biblia inasema hivi; "Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki na masikio yake husikia kilio chao." Hizo kelele zinazopigwa huko nje naamini hazitamdhuru Mama Samia, kwa sababu ametenda haki ya kuwaletea maendeleo wana Kyerwa. Hapo nilikuwa naeleza miradi iliyoletwa na sasa nakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya Mheshimiwa Mchengerwa sasa nipeleke maombi. Kazi nzuri ambayo ameifanya kwa upande wa barabara ni kazi nzuri sana. Tunampongeza mkurugenzi, amefanya kazi nzuri sana. Kwa upande wa Kyerwa kwa kweli amefanya kazi nzuri sana ya kufungua barabara. Bajeti yetu ya barabara kwa upande wa Kyerwa ilikuwa ni bilioni moja na milioni kama mia nane, lakini alipoingia Mama Samia bajeti imepanda kwa zaidi ya shilingi bilioni tatu, kwa hiyo tumefungua barabara nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto tuliyonayo ni ambayo Mheshimiwa Mchengerwa ameieleza kwenye bajeti yake na akasema wanawekeza kwenye barabara za vijijini. Kwa hiyo niombe sana kwa sababu huku ndiko kuna uzalishaji mkubwa, Kyerwa kuna kilometa zaidi ya 1,200 ambazo tayari tumekwishazifungua. Hata hivyo, barabara zenye changarawe ni kilometa 300 tu peke yake. Kwa hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Mchengerwa, niombe sana aongeze nguvu kwenye upande wa bajeti ya barabara. Vijijini ndiko kuna uzalishaji mkubwa, ndiko kwenye wakulima, hivyo tukiboresha barabara tutawarahisishia hao wakulima ili waweze kusafirisha mazao yao vizuri na kuyapeleka sokoni na naamini Serikali itapata kipato hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija upande wa elimu, tumepongeza kazi nzuri iliyofanywa, lakini Mheshimiwa Mchengerwa wameleta vyumba vingi vya madarasa. Sasa nimwombe sana, bado tunayo mahitaji, wananchi wameanzisha maboma mengi sana, lakini maboma haya hayajakamilika. Kwa upande wa elimu msingi kuna maboma 42 hayajakamilishwa na yapo kwa miaka mingi. Kwa upande wa sekondari tuna maboma 21 ambayo nayo yanahitaji kukamilishwa. Kwa upande wa afya tunayo maboma zaidi ya 12 ambayo wananchi wameweka nguvu kubwa lakini maboma haya hayajakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine ni kwamba Wilaya ya Kyerwa ni wilaya changa, ni wilaya mpya, kwa hiyo wanapotenga bajeti hizi wilaya changa waziangalie na kuziongezea bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya tunaomba sana, sisi tunazo tarafa nne lakini tuna *ambulance* mbili. Sasa niombe watuongezee *ambulance* nyingine mbili ili kila tarafa iweze kuwa na *ambulance* moja. Kwa upande wa vituo vya afya, tunazo kata 24, lakini vituo vya afya tulivyonavyo ni vitano. Kwa hiyo niombe sana tuongezewe vituo vya afya hasa kwenye Kata ya Songambele ambapo kuna msongano mkubwa na upande wa Tarafa ya Murongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo niombe sana ni suala la watumishi. Kwa sababu ya wilaya hizi kuwa changa watumishi wengi wanaoletwa Kyerwa, wanahama kwa sababu mazingira siyo rafiki. Kwa hiyo, niombe sana tuboreshe mazingira hasa pawepo na nyumba za watumishi. Pia kwenye hizi wilaya ambazo ni mpya ikiwezekana kuwe na namna ya kuwavutia hawa watumishi ili wasikimbie. Hili la watumishi naomba tuliangalie sana. Haya ambayo nimeyaomba, naomba yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana pia, Wilaya zetu zina vipindi virefu vya mvua tukiondoa hii mvua ya *El-Nino* ambayo imenyeesha, lakini wilaya nyingi kama Wilaya za Kyerwa tuna vipindi virefu vya mvua. Kwa hiyo hata tunapotenga bajeti katika wilaya

hizi tuwe tunaziangalia, vinginevyo tutakuwa tunapeleka fedha lakini itaonekana hazijafanya kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niendelee kuwapongeza, lakini kipekee nimshukuru sana Mkuu wetu wa Mkoa, anafanya kazi nzuri na Mkuu wetu wa Wilaya, mkurugenzi pamoja na watumishi wote wanafanya kazi nzuri kwa Kyerwa, tuko vizuri na Mkoa wa Kagera. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas, wajiandae Mheshimiwa Jafari Chege, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali na Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi hii ya uzima. Pia nichukue nafasi hii nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambazo anazifanya katika nchi yetu, lakini kwa kutupa miradi mingi sana ya maendeleo katika Wilaya yetu ya Mvomero. Tunamshukuru sana sisi watu wa Mvomero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia nitoe pole sana kwa wahanga wote waliopata mafuriko wakiwemo wananchi wangu wa Jimbo la Mvomero, ziko baadhi ya kata ambazo zilipata mafuriko lakini pia mafuriko haya yamesababisha kupoteza madaraja makubwa mawili, daraja la kutoka Turiani kuelekea Kata ya Pemba, Kata ya Kibati na Wilaya jirani ya Kilindi, lakini pia tumepoteza daraja la kutoka Turiani kwenda Mziha na kwenda Wilaya jirani ya Handeni. Niishukuru Serikali naona kazi imeanza, tuna imani baada ya muda mfupi watarudisha mawasiliano ya hizi barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na *TARURA* na nichukue fursa hii nimpongeze sana Mtendaji wa *TARURA Engineer* Seff. Kama kuna mtihani ameupata basi ni mwaka huu ana mtihani mkubwa

sana wa kuhakikisha barabara zote ambazo ziko chini ya *TARURA* zinarudi kama zilivyokuwa awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mvomero *TARURA* wanahudumia barabara zenye urefu wa kilometa 1,300 kuanzia 2020 kila mwaka bajeti yetu inapanda na katika bajeti inayokuja ya mwaka 2024/2025 tumeomba kupatiwa shilingi bilioni 2.9 na niombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Waheshimiwa Naibu Mawaziri, tuna imani na kazi kubwa ambazo wanazifanya na tunawaamini sana. Wasije wakatupunguzia fedha za *TARURA* hasa sisi watu wa Mvomero ambao tumepata madhara makubwa sana ya mvua kutokana na mafuriko ambayo yanaendelea katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zetu sisi pamoja na kwamba tunasubiri sasa bajeti ijayo lakini tumeomba fedha za *emergence* kwa ajili ya kuzirudishia barabara ambazo hazipitiki kabisa, tumeomba shilingi bilioni moja na milioni mia moja. Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Naibu Mawaziri, naomba watutazame Mvomero tumeomba bilioni moja na milioni mia moja ili tuweze kuzirudishia barabara ambazo sasa hivi hazipitiki, mfano kule Kibati, kuna barabara ya kutoka kwa Tembo Mchafu kwenda Diburuma Pandambili, barabara ile haipitiki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya kutoka Salawe - Diburuma, barabara ya kutoka Kwatembo Mchafu - Pemba – Gonja, barabara ambazo ziko Madizini pale mfano kutoka Manyinga – Madizini, barabara hizi hazipitiki kabisa. Tuna kipande cha lami ambacho tulikitengeneza chenye urefu wa mita kama 500 hivi lakini na chenyewe kwa sababu ya usimamizi mbovu kipande kile kimeharibika na imekuwa kero kubwa lakini kipande ambacho kimebakia ni kipande cha mita 500 tu ili tuweze kuunganisha kipande cha lami kutoka Manyinga mpaka Madizini, tunaomba sana tupatiwe fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambazo ziko katika Kata ya Diongoya, barabara ambazo ziko pale Manyinga zote zimekufa,

barabara ambazo ziko katika Kijiji cha Kilimanjaro na Kisara zimekufa, barabara ya kutoka Mbogo kwenda Mlaguzi imekufa, barabara ya kutoka Mbogo kwenda Kisimaguru na yenyewe imekufa, lakini tuna barabara ziko pale Mvomero, barabara za mtaa ambazo ziko chini ya *TARURA* na zenyewe hazifai zimekufa. Tuna barabara Dakawa pale zimekufa, tuna barabara kutoka Mzumbe kwenda Tangeni na pale Mzumbe Mjini ambapo ndio kwenye Chuo Kikuu kile cha Kihistoria, zimekufa na barabara nyingi siwezi kuzitaja zote kwa sababu ya muda. Tunaomba kwa Mheshimiwa Waziri tupate fedha ili tuweze kuzirudishia hizi barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika bajeti yetu ambayo tumeileta, tungeomba kutengenezewa Daraja la Mto Mjonga ambalo linaunganisha Kijiji cha Digoma na Digalama, tumeomba milioni 750, tuna imani Mheshimiwa Waziri atatoa hizi fedha ili tuweze kujenga hili daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna stendi ya mabasi ambayo iko pale Turiani, Kijiji cha Manyinga, ni stendi kubwa sana kwa sababu mabasi yote yanayotoka Tanga, Arusha yanayotoka Handeni, Kilindi yanaingia pale ndio stendi yetu kubwa, stendi ile sasa hivi mabasi yanapakia nje badala ya kupakia ndani ya stendi kwa sababu ya ubovu wa stendi. Katika bajeti yetu tumeomba tupate fedha kwa ajili ya kuikarabati hii stendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana kwa Mheshimiwa Waziri wasije wakatunyima fedha kwa ajili ya kutengeneza hii stendi, ni aibu Watendaji wa Vijiji wanakata ushuru magari ambayo yako nje, yanapakilia barabarani badala ya kupakia ndani ya stendi. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atupe fedha ili tuweze kuitengeneza ile stendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeomba kupatiwa soko la kimkakati pale Dakawa, Dakawa ni mji ambao unakua kwa kasi sana na pale wananchi wengi wanajishughulisha na shughuli mbalimbali za kilimo na shughuli nyingine za kibiashara. Tunaomba tupate fedha kwa ajili ya kujenga soko kubwa na soko la kisasa.

Katika bajeti yetu tumeomba maombi ya kujengewa hilo soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana, kwenye miji ambayo inakua hizi barabara ambazo tunazijenga na baadhi ya maeneo tumeanza kujenga kwa vipande vya lami, tunaomba watupe fedha tuweze kuweka na taa. Hizi barabara ni nzuri lakini hazipendezi kama hazina taa, niombe sana Mheshimiwa Waziri watupe fedha tuweze kuweka hizi taa za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwenye sekta ya elimu ametufanyia mambo mengi sana na sisi Mvomero tumeshakubaliana Mheshimiwa Rais anatudai mambo mawili tu. Jambo la kwanza ni kumwombea tu afya njema, lakini jambo la pili ni kumpa kura zote za ndio mwaka 2025. Hayo ndiyo mambo mawili tu ya kumfanyia Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa na mazuri ambayo ametufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaeleze kuhusu elimu, ametupa fedha tumejenga sekondari nne katika kipindi cha miaka mitatu, bado tumebakisha sekondari mbili tu tuwe tumekamilisha kata zote 30 kuwa na sekondari. Tumepokea zaidi ya bilioni nne, tumejenga vyumba vya madarasa 180. Tumepokea fedha za kujenga shule za msingi mbili, tumejenga Dakawa pale kwa Mhuzi na tumejenga na katika Kijiji cha Mlali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumepokea zaidi ya shilingi milioni 700 tunakwenda kupandisha hadhi sekondari zetu nne zinakuwa sekondari za kidato cha tano na sita kule Tarafa ya Mgeta. Kilikuwa ni kilio cha miaka nenda, rudi, tarafa nzima haikuwa na *High School*. Leo Sekondari kongwe ya Mgeta tunakwenda kuipandisha hadhi, tunakwenda kujenga kidato cha tano na cha sita, lakini pia tunakwenda kuipandisha hadhi Sekondari ya Doma, wananchi wa Tarafa nzima ya Mlali walikuwa hawana *High School* na wenyewe wamepata fedha tunakwenda kujenga *High School* katika Tarafa ya Mlali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Tarafa ya Turiani tunajenga Sungaji pale Sekondari ya *High School,* Tarafa ya Mvomero tunajenga pale katika Kata ya Mvomero, Sekondari ya *High School* ndio maana nasema sisi Mvomero hatumdai Mama, sisi ndio tunatakiwa tuhakikishe tunamwombea afya njema tunampa na kura zote za ndio 2025 ndio kazi kubwa ambayo ipo upande wetu sisi anayotudai yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niombe sasa mambo machache sana ambayo Mheshimiwa Waziri atusaidie, tuna nyumba za walimu ambazo zimejengwa na nguvu ya wananchi, ni maboma ya muda mrefu, tunaomba watupe fedha tuyamalizie, lakini pia tuna shule kongwe nyingi sana kwa sababu ya muda siwezi kutaja shule moja moja isipokuwa tunaomba watupe fedha tuweze kuzikarabati hizi shule, ikiwezekana tuweze kujenga vyumba vipya kabisa vya madarasa. Pia tunaomba watupe fedha za kumalizia sekondari hizi mbili nilizosema, Kata ya Mkindo hatuna sekondari na Kata ya Kikeo hatuna sekondari, hivyo, tunaomba fedha tuweze kujenga sekondari mbili katika hizi kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye upande wa afya, tumepokea miradi mingi sana kwenye upande wa afya, hivi karibuni nimekwenda kupokea vifaatiba vyenye thamani ya shilingi bilioni moja na milioni mia nne. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Jonas kengele ya pili, Mheshimiwa Chege…

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** …wajiandae Mheshimiwa Gulamali na Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa afya ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Wilaya na Halmashauri ya Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri kwa namna wanavyoendelea kufanya *reform* ya Ofisi hii ya TAMISEMI na namna anavyoendelea kujitoa katika kushughulika na Ofisi hii hasa ukitambua ofisi hii ndio ofisi mama inayogusa maeneo mengi yanayogusa wananchi wanyonge kwenye maeneo yetu tunayotoka. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo nichukue nafasi pia kabla sijaanza mchango wangu kumshukuru sana, kumpongeza na kumtakia kila la kheri aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda kwa kazi kubwa ambayo alikuwa akiendelea kuifanya kwa Mkoa wetu wa Mara, kutuunganisha lakini pia alijua namna ya kwenda na watu wa Mkoa wa Mara. Kiukweli tutamkumbuka sana tuwaombe watu wa Mkoa wa Mwanza huko alikokwenda wampokee na wamtendee mema sana. Niendelee tu kushauri mamlaka za uteuzi kama atawashinda watu wa Mkoa wa Mwanza, basi waturudishie sisi Mkoa wa Mara kwa sababu bado tunamhitaji kwelikweli. Ni mtu mwema na ni mtu mzuri sana, Mwenyezi Mungu amtangulie kwenye majukumu anayokwenda kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumkaribisha sana Kanali Evance Mtambi ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara na sisi kama Wabunge tunamuahidi tutampa ushirikiano mzuri kwa namna ambavyo yeye atakuwa anahitaji ushirikiano wetu, tuko tayari kumpa ushirikiano kama Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza Mkuu wangu wa Wilaya Juma Chikoka kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na Wakurugenzi na Wakuu wa Idara.

Wakati Juma chikoka analetwa Wilaya ya Rorya, wengi tulimchukulia kama msanii, hatukujua kipaji na uwezo alionao kwa namna ya kusimamia na kuiongoza ile wilaya, nimtakie kila la kheri na sisi tuko nyuma yake, aendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi mizuri, mikubwa ambayo anaifanya ndani ya Wilaya yetu ya Rorya hasa miradi inayogusa wananchi wanyonge hasa akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo madaraja mengi kama ambavyo nilikuwa nikisema hapa wananchi hasa akinamama walikuwa hawawezi kuvuka kutoka upande mmoja kwenda upande wa pili, Mheshimiwa Rais ametupa fedha, tumejenga madaraja hayo na sasa hivi wananchi wanapita vizuri sana. Tumejengewa pia shule mpya zaidi ya sita, zahanati zaidi ya 12, vituo vya afya viwili kwenye muda wake wa miaka mitatu pekee na ndani ya miaka mitatu ambayo tunakwenda, ametupa fedha zaidi ya bilioni 134 kwenye miradi ya utekelezaji wa maji. Kiukweli Mheshimiwa Rais ametutendea mema na yapo mengine ambayo siwezi kuyataja kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo utajikita katika maeneo mawili. La kwanza, nianze kuomba, kipo Kituo cha Afya cha *Labour* ambacho Mheshimiwa Rais ametupa zaidi ya shilingi milioni 500, kituo kile kimekwenda kimefikia zaidi ya asilimia 80 mpaka 85 hakijakamilika. Tunaomba fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hiki ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nimwombe Mheshimiwa Waziri aone namna ya kuwatazama Watendaji wa vijiji na Watendaji wa Kata angalau kuwajali kwenye maslahi kwa sababu tunakwenda kwenye uchaguzi watu wale kimsingi tumewasahau kwa muda mrefu sana tuone namna ambavyo tunaweza tukawajali kwenye maslahi yao ili angalau waendelee kupiga kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba kwenye Kituo cha Afya cha Nyamagaro, Mheshimiwa Rais ametupa fedha katika vituo viwili ninavyozungumza vya Wilaya ya Rorya ni pamoja na Nyamagaro, kimeanza kutoa huduma lakini hakina mochwari na baadhi ya majengo mengine hayajakamilika, Waziri atusaidie kupeleka fedha ili kukamilisha kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimshauri sana Mheshimiwa Waziri kufanya tathmini nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Rorya kugundua na kujua idadi ya wanafunzi, idadi ya vijana wanaojitolea kutoa huduma mbalimbali za kielimu kwenye shule za msingi na shule za sekondari ili angalau tuweze kupata idadi kamili ya hawa vijana ili zinapotokea ajira waweze kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni vema Mheshimiwa Waziri akafanya tathmini kwenye Wizara yake akajua changamoto kwenye shule zote ambazo zinawakabili wanafunzi hasa changamoto ya vyoo ili angalau fedha iende. Ni aibu sana tunavyokwenda kuendelea kuzungumzia kwamba shule fulani ina changamoto ya choo au tunauliza Waheshimiwa Wabunge kwenye maswali ya nyongeza au maswali ya msingi kuhusiana na choo cha shule fulani.  Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri haya ayafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye mchango wangu ni fedha za miradi ya kimkakati.  Wilaya ya Rorya inavyo vyanzo vikuu vya mapato ambavyo kikubwa ni uvuvi, lakini wewe ni shahidi na bahati nzuri unatoka kwenye maeneo ambayo yanafanya shughuli za uvuvi, ni shahidi namna ambavyo uvuvi umeathirika kutokana na sababu mbalimbali.  Moja inaweza ikawa ni mabadiliko ya tabianchi, lakini pia samaki hawapatikani ziwani kwa sababu mbalimbali tu, kwa hiyo, chanzo hiki kimekuwa siyo imara sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri halmashauri ambazo zinafanya shughuli ambazo zinategemea vyanzo ambavyo siyo *stable* sana na nimekuwa nikisema sana, hii ni mara ya tatu Mheshimiwa Waziri nazungumza, halmashauri ambazo vyanzo vyake

siyo *stable,* siyo *sustainable,* havidumu kwa muda mrefu na vimekuwa vyanzo kwa miaka zaidi ya 40 au 50 na ndivyo vyanzo ambavyo halmashauri wanavitegemea kujiongezea mapato, hawa ndio tuwape fedha za miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwaka wa tatu nimekuwa nikiomba wilaya yangu angalau kupata fedha za mradi wa kimkakati, lakini unaweza ukaona vyanzo vya mapato, ukiacha uvuvi na kilimo, hatuna mradi mwingine wowote wa kimkakati ambao Serikali imeuweka unaozalisha uchumi kwenye eneo lile. Kwa hiyo, hata kama watawaelekeza wakurugenzi kwamba, wabuni chanzo kingine cha mapato atabuni chanzo, lakini hana fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Rorya inakusanya shilingi bilioni 1.5 kwa mwaka, kwa mwezi ni shilingi milioni 120, huyu mtu ukimwambia buni mradi wa mkakati wa shilingi bilioni 100 hawezi kufanya. Kwa hiyo, mwisho wa siku utajikuta chanzo chake anategemea akachukue ushuru kwa wananchi, akakusanye vitu ambavyo kimsingi haviko *stable*. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye fedha za miradi ya kimkakati, tuwapelekee halmashauri hizi ambazo vyanzo vyake siyo *stable* ikiwemo na Halmashauri yangu ya Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo nimekuwa nikimfuata nikimwomba sana tupate Soko la Samaki pale Shirati, Shirati ni mji unaokua. Leo Mheshimiwa Waziri akiniambia anakuja Rorya nitampeleka shirati, lakini hatuna soko la kisasa la samaki na ndio eneo ambalo linatokea sehemu ambayo uzalishaji wa samaki ni sehemu kubwa ya shughuli ya kiuchumi. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri atusaidie tupate soko kubwa la samaki ili liweze kutusaidia kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tungeomba tupate Soko la Dagaa kule Mkengwa Kinesi, tukipata soko la dagaa kule Mkengwa kwa haya mawili yatatusaidia angalau kuonesha namna ambavyo tutakuwa tunawasaidia hawa wavuvi kwa sababu wanavua, lakini

hawana soko la uhakika. Leo mvuvi anavua, anapeleka bidhaa zake Mwanza au Kenya, maana yake hana soko la uhakika na bado huyu anatakiwa alipe ushuru. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri kwenye eneo lile aweze kutusaidia. Siyo hayo tu, ingewezekana atusaidie Mkoa mzima wa Mara tupate Soko kubwa la Samaki kwa sababu shughuli zetu za kiuchumi kwenye Mkoa wa Mara ni pamoja na uvuvi, lakini hatuna soko kubwa la samaki au la dagaa ambalo tunajivunia. kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri wakati anaitazama Rorya pia atazame namna ya kufanya kwa Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kilongwe mpakani tumekuwa tukiomba tupate fedha ya Mradi wa Kimkakati, tujenge Soko la Kibiashara eneo la Kilongwe. Kilongwe ni sehemu inayopakana na Kenya na Tanzania, leo tunaomba lami iende mpaka Kilongwe lakini hatuna uzalishaji kwenye eneo lile. Tunaomba sana angalau kwenye fedha zao za miradi ya kimkakati na sisi wananchi wa Rorya tuweze kupata. Ni mwaka wa tatu nimekuwa nikiomba hili na hakuna utekelezaji. Nimwombe kwa kuwa naamini yeye ni mtekelezaji na ni mfuatiliaji mzuri, wananchi wangu wapate fedha za miradi ya kimkakati angalau katika hizo nilizozitaja hata kama ni mmoja wa kuanzia ili waweze kusogea kwenda hatua ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni *TARURA*, nilichangia bajeti iliyopita na nikasema Mkoa mzima wa Mara, tunazungumzia bajeti ya mwaka uliopita, mpaka ninavyozungumza yawezekana ni mwezi wa tatu, mpaka mwezi wa tatu, kwa upande wa barabara kwa bajeti ya mwaka 2023/2024, hakuna mkandarasi aliyekuwa *site* hata mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko sababu mbalimbali na namshukuru sana Mkurugenzi wa *TARURA* kwa kazi nzuri kubwa anayoifanya, lakini hebu fuatilia ujue kwa nini hawajaingia *site,* lakini zipo barabara pamoja na kuingia *site,* barabara za mwaka ulioisha na mwaka huu tunaokwenda hazipitiki. Mfano nitataja chache; Barabara ya kwanza Bukama - Nyamagaro, huko Nyamagaro ndio chanzo cha mapato, lakini barabara haipitiki na huwezi kwenda.

Barabara ya Kinesi - Bitirio hapitiki, ukitoka Shirati kwenda Rwang'enyi haipitiki kabisa, Barabara ya Ingiri Juu kwenda Kitembe huwezi kupita na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kwa Mkoa wa Mara zimesimama kwa muda mrefu, sijajua sababu ni nini? Inawezekana baadaye Mheshimiwa Waziri anapokuja kufanya majumuisho atatuambia sisi watu wa Mkoa wa Mara ni kwa nini barabara zimechelewa sana kuanza. Kama tatizo ni fedha tujue, kama tatizo ni wakandarasi tujue, ni kwa nini mpaka mwaka huu mwezi wa Tatu hakuna mkandarasi *site?* Yaani tunakwenda kuimaliza bajeti, lakini hatuoni mkandarasi *site*. Kwa hiyo, ni vyema sisi wananchi tukapata majibu ili tunapokwenda tujue tunawaambia nini wale wananchi, kwa nini barabara zao zimechelewa, tutakwenda kujadili bajeti ya awamu ya pili, leo inapitishwa bajeti ya mwaka wa pili, mwaka unaisha wakandarasi wa barabara hawajaonekana *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili kipekee pamoja na kwamba hili limechelewa, yawezeka ilikuwa ni tatizo la kifedha, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa *TARURA,* sisi watu wa Rorya ametufaa sana. Leo nikianza kutaja miradi mikubwa ambayo imefanywa, namtaja Mkurugenzi wa *TARURA* kwa sababu madaraja tunayoyazungumza, ni yeye ndiye aliyetupa fedha. Juzi tulikuwa na daraja ambalo linawaunganisha wananchi, wamekaa zaidi ya miaka 40 wakasema hawajawahi kuona kiongozi na hawawezi kuvuka upande mmoja kwenda upande wa pili kwa sababu wametenganishwa na mto, lakini ametupa fedha milioni 95 na daraja lile linajengwa. Kwa hiyo Mkurugenzi huyu wa *TARURA* tumpe *compliment,* tuhakikishe kwamba analindwa na anapewa fedha ili aweze kutekeleza haya ambayo ameyapanga. Tukimkwamisha maana yake atashindwa kutekeleza haya ambayo ameyasema kwenye utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni usimamizi wa fedha za miradi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, upo Waraka wa mwaka 2009 ambao unawaondoa Madiwani. Watu wanaotajwa kwenye waraka huu kwenye kusimamia fedha za miradi Madiwani

hawatajwi kwenye usimamizi wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Mfano, tunasema mama amepeleka fedha halmashauri halafu kutokana na ule Waraka wa mwaka 2009, Madiwani kupitia Kamati zao hawaruhusiwi kwenda kukagua miradi ya kimaendeleo. Ndiyo maana leo miradi mingi utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inayoruhusiwa kufanya ukaguzi ni Kamati ya Fedha pekee; Kamati ya Fedha peke yake haiwezi ikaleta taarifa kwenye Baraza la Madiwani, kama kuna ubadhirifu umefanyika maana yake wanatoa taarifa kabla ya ukaguzi. Naomba kwa nafasi ya Mheshimiwa Waziri, anaweza kuuondoa Waraka huu wa mwaka 2009 na kama inawezekana aufute. Atoe waraka ambao utaendana na kasi ya fedha anazopeleka Mheshimiwa Rais kwa sababu, wakati huo mwaka 2009 inawezekana fedha za miradi zilikuwa ni chache sana, leo fedha zinazokwenda ni nyingi, ni lazima tuwe na jicho la chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati za Bunge zinapokwenda ziende kukagua sehemu ambazo Madiwani wamejiridhisha kwamba, fedha ile ni kweli, imetumika sawasawa. Huu waraka ndiyo umekuwa kigezo cha kutokuwakubalia Madiwani kwenda kukagua miradi. Namwomba Waziri afanye *review* ya huu waraka, Madiwani kupitia Kamati zao kama zilivyo Kamati za Kibunge waende wakakague miradi yote ambayo Serikali imepeleka fedha. Mheshimiwa Waziri ataona ufanisi kwenye maeneo haya na ataona, kweli kazi inafanyika na ubadhirifu huu wa fedha tunaozungumza hautakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gulamali, wajiandae Mheshimiwa Maimuna Mtanda na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hii Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza binafsi napenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya ndani ya nchi yetu, hususan ndani ya Wilaya yetu ya Igunga. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Ofisi hii Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya hasa katika usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya fedha ambazo wanazitoa. Kubwa nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa mara ya kwanza ameniletea mkurugenzi ambaye ni makini sana, nampongeza sana. Sikuwahi kupata mkurugenzi toka niwe Mbunge, hii ni kwa mara ya kwanza nimepata mkurugenzi mzuri. Hapa na-*declare interest* kwamba, mama ameupiga mwingi sana kutuletea mkurugenzi, kama alivyoupiga mwingi kunipatia Mkuu wa Wilaya, kwa kweli sasa wilaya yetu itakimbia mwendo wa spidi 160 kama Yanga vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza *TARURA* kwa kazi nzuri ambazo wameendelea kuzifanya. Nawapongeza na nampongeza Mheshimiwa Rais kwa nia yake ya dhati, mwanzo mimi binafsi nilikuwa napokea fedha ndani ya Jimbo langu la Manonga shilingi milioni 300 kwa mwaka. Fedha hizi tulikuwa tunazipokea na kutengeneza barabara ndani ya jimbo letu na kama mnavyotambua Wilaya ya Igunga tuna zaidi ya kilometa 1,500 zinazotengenezwa na *TARURA*. Fedha tulizokuwa tunapewa kama wilaya ni shilingi bilioni moja na ndani ya jimbo langu nilikuwa napokea shilingi milioni 300, lakini tangu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameongeza fedha tumetoka kwenye kupokea shilingi milioni 300 mpaka shilingi 1,500,000,000 ndani ya Jimbo langu la Manonga. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi nyingi zimeleta mabadiliko makubwa sana. Ndani ya kipindi cha miaka mitatu

tumeweza kufanya mabadiliko makubwa ya ujenzi wa madaraja makubwa ya Mto Manonga, Mto wa Mazila kule Igoweko na pia, tumeweza kujenga barabara nyingi kwa kiwango bora kabisa. Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongeza fedha

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri kwenye bajeti hii ya safari hii. Kwa kweli, sijui tumekwama wapi, miaka miwili tumepokea fedha nyingi, lakini mwaka huu mpaka dakika hii tumepokea na kufanya kazi kwa asilimia 50 ya bajeti tuliyotengewa, kwa maana ya kupokea *1.5 billion.* Asilimia 50 nyingine ya kazi zote zilizotakiwa kutangazwa mpaka muda huu hazijatangazwa, bado ziko *pending* na wala mikataba haijatiwa saini. Namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake watupatie fedha zilizobaki, watu wa *TARURA* waweze kutia saini mikataba na wakandarasi ili kazi iliyosalia iweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumeona mvua nyingi imetokea na kuleta athari kubwa ndani ya jimbo letu. Miundombinu haijatengenezwa na fedha ambazo tulikuwa tumetenga na kuwaahidi wananchi kwamba, barabara zingetengenezwa mpaka muda huu hatujatengeneza. Kwa hiyo, naomba Wizara ilisukume jambo hili, lakini nawaomba kwa sababu katika zile fedha tulizopitisha, tulipitisha fedha za dharura zaidi ya shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kupeleka katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutatua madhara yanayotokana na mvua ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ndani ya Jimbo letu la Manonga hatujapokea fedha za dharura na tumekuwa ni wahanga wa maafa au majanga ya mvua. Tunaomba na sisi tupewe hizo fedha ili tuweze kukarabati miundombinu. Kwa mfano, tuliwahi kupeleka mpaka kwa Mkurugenzi Mkuu wa *TARURA* andiko la kuomba kiasi cha shilingi milioni 700 ili tuweze kujenga daraja ambalo halipo, wananchi wanahangaika, wanavuka kwa mtumbwi wengine wanatumbukia katika Mto Manonga na madhara yake ni makubwa kiasi cha wengine kupoteza uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba tupate fedha. Namshukuru Mkurugenzi wa *TARURA,* Ndugu yetu Victor Seff aliahidi

kwamba, fedha hizi tutazipata kabla ya mwezi Februari na kazi itaweza kuanza, lakini mpaka sasa hivi hatujapokea fedha. Tumeahidiwa tena kwamba, kabla ya mwezi Juni fedha hizi tutazipata. Naomba *TARURA* na Wizara waweze kutupatia fedha hizi haraka kwa sababu mahitaji ya wananchi ni makubwa na tunahitaji kujenga daraja katika Mto Manonga kwenye Kijiji cha Mwashiku kuhakikisha kwamba tunawarahisishia wananchi wetu kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekosa fedha za dharura, basi tunaomba tupate hizi shilingi milioni 700 ili zitusaidie kuvuka katika kipindi hiki ambacho tunaenda kumalizia mwaka wa bajeti. Hata hivyo, 50% ya kazi ambazo hazijasainiwa na zenyewe zisainiwe. Mheshimiwa Waziri hayupo, lakini Naibu Mawaziri wanaandika hapo, tunaomba watupatie fedha hizi ambazo ni 50% ya fedha zote tuweze kuendelea na hizi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali, kazi kubwa imefanyika kwenye ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari nchi nzima. Tunawapongeza sana kazi ni nzuri, hata uhaba wa madarasa kwa watoto wetu wa sekondari umefutika. Nashauri kwamba, nguvu kubwa tuliyowekeza kwenye ujenzi wa madarasa ya sekondari tuielekeze kwenye ujenzi wa madarasa shule za msingi. Shule zetu za msingi nchi nzima ziko hoi *bin* taabani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa tufungue macho, kuna shule za msingi zina madarasa manne, shule ilijengwa mwaka 1950, 1960 au 1970 zina madarasa manne miaka yote, ndani ya Jimbo langu la Manonga zaidi ya shule 70 ziko hoi *bin* taabani. Kwa hiyo, naomba Serikali iingize fedha tujenge shule za kisasa kwa *level* ya shule za msingi au tuongeze madarasa ya kisasa ili watoto hawa ambao wanaanza shule ya msingi waingie kwenye madarasa bora na yenye afya kwa watoto wetu kwa sababu, majengo haya ukiyaangalia yalivyochoka unaweza ukakimbia ukasema hapa siyo jimboni kwangu labda ni nchi jirani, kumbe ni Tanzania. Ukilinganisha shule za msingi na sekondari zimeachana mbali sana, kwa hiyo,

tufanye uwekezaji. Najua kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, linawezekana. Kama tumeweza kwenye shule za sekondari basi, hata kwenye shule za msingi linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashauri watu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wao ndiyo wazalishaji wakubwa wa ajira kwa vijana wetu, ndiyo wanaowapika. Nawaomba watazame upande wa miundombinu ya michezo kwenye shule zetu za sekondari waiboreshe. Siyo watengeneze kwenye shule zote, hapana, lakini kwenye kila wilaya au kila jimbo wachague shule moja waweke miundombinu mizuri ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona Simba na Yanga zinafanikiwa, lakini nyuma ya Simba na Yanga kuna wachezaji ambao wamesajiliwa kutoka mataifa mbalimbali ambao ndio wanaocheza na kukuza *brand* ya hizi timu. Wachezaji wetu bado hawajatoka kwa wingi kwenda nje ya nchi, tatizo kubwa ni kwa sababu, hatujatengeneza mazingira ya kuwaandaa. Nchi hii ikitaka kupata uchumi wa utalii ni lazima tuandae vijana. Vijana hawa wanaandaliwa na Ofisi hii ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuhakikisha kwamba, miundombinu bora inaanzia katika shule zetu ili kuhakikisha tunafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, naishukuru sana Serikali kwa kutupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ziba ingawa bado hakijakamilika, naiomba Wizara ituletee fedha tuweze kukikamilisha vizuri. Mheshimiwa Mchengerwa hapa karibuni alitupatia karatasi tuandike na tuwaambie wananchi tunajenga vituo vya afya. Niliandikia Kituo cha Afya cha Uswaya, lakini sijaona watu wake wakija jimboni kwenye Kijiji cha Uswaya kuwaahidi wale wananchi kwamba, tunajenga kituo cha afya. Nilienda kule nikawaambia Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri wametupatia kituo kingine cha afya. Sasa Mheshimiwa Waziri hili lisije kuwa bomu lingine tena. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kile kituo cha afya alichoniambia nikiandike na niende nikawaambie wananchi kwamba, watakijenga, sasa tunaomba hizo fedha zije ili tuweze kufanikisha ujenzi wa kituo hicho cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, pale Wilayani kwetu Igunga tuna mapato ya kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni tano kwa mwaka, tunakusanya sana. Tuna dhahabu, tuna kilimo cha pamba na tuna mifugo mingi, lakini makao makuu yetu ya wilaya hayafanani, tunaomba kujengewa lami. Tunaona wilaya nyingine zinapewa lami katika miji yao, sisi wilaya yetu haina lami. Tunaomba tupatiwe lami ili na sisi mji wetu upendeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunaomba stendi ya kisasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili imelia hiyo.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tunaomba stendi ya kisasa katika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa mengine andika, kengele ya pili.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda, wajiandae Mheshimiwa Mchungahela na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Pia naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kila siku. Rais wetu amekuwa akizunguka huku na huku kutafuta fedha ili maeneo yetu yapate kwenda vizuri. Tunashukuru kwa fedha na miradi tunaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na timu yake yote.

Pia nampa pole kwa mafuriko ambayo yamemkuta kule Rufiji na maeneo yote ambayo yamekumbwa na mafuriko nawapa pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la watumishi. Kumekuwa na uchache wa watumishi kwenye maeneo ya pembezoni. Naiomba sana Wizara, inapoenda kutangaza ajira za watumishi basi itupie jicho halmashauri za pembezoni kwa sababu, hali ni mbaya, hali siyo nzuri sana. Nikichukulia mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala, ukienda kwenye afya peke yake upungufu ni mkubwa sana, mahitaji ni watumishi wa afya 675 waliopo ni 170 tu, sawa na 25.18%. Hali hii haileti tija kwa sababu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndiyo Wizara mama, sote hapa tunahudumiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kama watumishi kule chini hawapo tafsiri yake ni kwamba, hata huduma haziwezi kutolewa vile ambavyo tunatarajia. Kwa hiyo, tunaomba sana Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mgawo utakapoanza tutupie macho zaidi kwenye halmashauri za pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye elimu, Halmashauri ya Wilaya ya Newala upande wa elimu ya msingi mahitaji ni walimu 751, lakini walimu waliopo ni 473 pekee. Elimu ya sekondari mahitaji ni walimu 402, lakini waliopo ni 212. Kwa hiyo, kwa ujumla ni kwamba, hali ya watumishi kwenye halmashauri za pembezoni siyo ya kuridhisha. Tutupie macho ili halmashauri hizi ziweze kufanya kazi kama vile ambavyo Serikali inatarajia kutoka kwa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana mwaka jana nili-*experience* kitu ambacho sikukipenda kwenye halmashauri yangu ya *Newala DC*. Watumishi wanakuja wanaripoti, hasa walimu, pale wanaenda kupata *check number* tu na kwa bahati mbaya hata mkurugenzi hajapitisha uhamisho, lakini uhamisho unashuka wanaondoka. Kwa hiyo, changamoto unakuta bado inaendelea kuwa kubwa badala ya kutibu kile ambacho tulikuwa tunatakiwa kukitibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nataka kuongelea kwa upnde wa suala la watumishi ni kuhusu upandaji wa madaraja. Watumishi wengi wamekuwa wakitumika kwa muda mrefu, lakini madaraja hawapandi, madaraja kwa mtiririko ule ambao tunautarajia. Tunajua vipo vigezo vya mtumishi kupandishwa daraja, wako wengi sana ambao wamekidhi vigezo, lakini hawapandi daraja. Unakuta mtumishi ana miaka saba mpaka kumi hajapanda daraja, hii siyo sawa kwa sababu, inamuumiza hata kwenye maslahi yake. Badala ya kupata kile ambacho alikuwa anatakiwa kupata, anaendelea kupata kidogo kwa sababu ya mtiririko ambao siyo mzuri wa upandaji wa madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee suala la likizo pamoja na uhamisho. Watumishi wengi hawapati stahiki zao ambazo wanatakiwa kupata wanapoenda likizo au wanapohama, imekuwa ni kero na madeni ni mengi. Naiomba sana Wizara ifanye uchunguzi, waende kule halmashauri waangalie, hali siyo nzuri kiasi kwamba, watumishi wanakosa morali ya kufanya kazi vizuri kwa sababu, stahiki zao hawazipati vile ambavyo walikuwa wanatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, watoe maelekezo mahususi kwa wakurugenzi ili kutatua changamoto hizi za kimaslahi kwa watumishi wao. Pia, Tume ya Utumishi wa Walimu nayo iangalie namna ambavyo madaraja yanapanda kule chini, inawezekana taarifa wanazozipata siyo sahihi, malalamiko yapo mengi sana. Naomba watu wapande madaraja kwa sababu ni haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masuala yanayohusu utumishi naomba nizungumze kidogo kuhusu *TARURA*. Tunaipongeza sana *TARURA* imekuwa ikifanya kazi kubwa sana kupitia uongozi wa *Engineer* Seff, tunampongeza. *TARURA* ina kazi kubwa sana, hasa vijijini, kwa mfano ukienda Wilaya ya Newala mtandao wote wa barabara ni kilometa 1,436 ambapo barabara za *TARURA* ni asilimia 90, wana kilometa 1,360. Hawa watu wana meneja mmoja ambaye anahudumia mjini na vijijini na kwa bahati mbaya sana mwaka huu

tumepata mvua za *El-Nino* ambazo zimebomoa barabara zote na hazipitiki, kwa hiyo, hawa watu wana mzigo mkubwa. Naishauri Serikali irudishe ule utaratibu wa zamani ambao kila halmashauri ilikuwa na meneja wake wa *TARURA* ili kurahisisha kazi, barabara ni mbovu kupita maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Newala Mjini kulitokea mafuriko kwenye Kata ya *Mcholi II*, mafuriko ambayo yaliharibu miundombinu ya barabara ya Mpilipili na Chikwendu hakupitiki. Huko ni Newala Mji, lakini anayetakiwa kuhudumia ni meneja huyu huyu ambaye akitoka Newala Mji anaenda Newala Vijijini ambako barabara zimekatika sana. Ukienda Mpalu – Malatu Chini, Namdimba – Chiwata, *Mkoma II* – Chimemena, Lihanga – Lochinu, Mikumbi – Mpanyani, Chihangu – Mtongwele mpaka Maputi, Ngalu – Mdimba, Mkwedu – Mtunguru na Chiwonga – Mulunga huku kote barabara zimekatika hazipitiki, lakini anayetakiwa kushughulikia ni meneja huyo mmoja ambaye anatakiwa kusimamia Newala Vijijini na Newala Mjini ambako hali ya barabara kwa kweli siyo nzuri. Kwa hiyo, wakati mwingine inawezekana tukawalaumu, lakini kwa sababu ya uzito wa mzigo walionao kazi inaweza kuwa ngumu sana. Tutafute namna ambavyo tutawapunguzia mzigo mameneja wetu ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee mikataba ya utendaji kazi ya *TARURA*. Katika maeneo mengi mikataba ile haijasainiwa mpaka leo, kama alivyoongea Mheshimiwa Gulamali. Hali hii pia ipo Newala, mikataba haijasainiwa na huu ni mwezi Aprili na kwa sababu ilikuwa kwenye mwaka wa fedha wa 2023/2024, kama mpaka leo haijasainiwa tumebakiza miezi miwili, tunatarajia nini? Naiomba sana Serikali itupie jicho maana kwa bahati mbaya barabara ndiyo hizo ambazo zimeharibika, kwa hiyo, tufanye jitihada za makusudi, mikataba isainiwe na wakandarasi waende *site* ili wakarekebishe barabara zetu, sasa hivi mvua zinaenda mwishoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi pia katika Wilaya ya Newala hatujapata fedha za dharura, hatujapata hata shilingi moja.

Niiombe Ofisi ya TAMISEMI kupitia Waziri Mchengerwa watuangalie na sisi Wananewala tupate fedha za dharura ili tukakarabati zile barabara ambazo zimeharibika. Nyingine zilikuwa hazipo kwenye mpango wa mwaka huu, lakini zimeharibiwa haziwezi kupitika. Suluhisho pekee ni kupata fedha ambazo zitaenda kunusuru usalama wa barabara hizi ili wananchi waweze kupita na kusafirisha mazao yao. Mwisho wa siku na huku mjini, basi tupate mazao na wananchi wale uchumi wao uweze kupanda juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Newala Vijijini na Newala Mji ni wilaya kongwe ya muda mrefu na shule zake nyingi sana ni kongwe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ukarabati wa zile shule kongwe. Naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, wajiandae Mheshimiwa Ulenge na Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa uhai. Naanza kwa kusema kwamba, tuna msemo kule kwetu wa moja ya kabila linaitwa kabila ya Kiyao.

**NAIBU SPIKA:** Kwenu wapi?

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu kule Mtwara, Lulindi. Huo msemo unasema; "*Pumonelele mzungu mumnamuchile popopo.*" Msemo huu maana yake ni kwamba ukishamuona Mzungu usipoteze muda, msalimie hapo hapo au mwombe hapo hapo. Leo hapa nimekuja katika muktadha wa kuomba, kwa leo sitazungumzia sana mambo ya Kitaifa hapa lakini

nitazungumzia suala la ustawi wa Jimbo langu. Kama nitapata nafasi basi nitaigawa kuipeleka katika masuala ya Kitaifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ustaarabu kwamba kabla hujaomba lazima ushukuru kwa kile ulichokipata hapo mwanzo. Sitakuwa mtovu wa shukrani lazima nianze kwa kushukuru vile ambavyo vimeshapatikana katika eneo langu. Kipekee kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na misaada mingi aliyotupa sisi Wanalulindi kama Jimbo ambayo inatuwezesha sasa kutoka katika hali ambayo tulikuwa nayo mwanzo na kuonekana kuwa ni miongoni mwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nitachomokea jambo ambalo haliko moja kwa moja kuhusiana na TAMISEMI, ni jambo kubwa sana ambalo linaendelea pale katika eneo langu ni barabara. Ni barabara kubwa ambayo ilikuwa ikizungumzwa miaka nenda, rudi tangu dunia hii iumbwe, barabara ya kutoka Msanga kuelekea Newala. Barabara hii sasa hivi inajengwa, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni barabara kubwa na yenye pesa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa jitihada zake binafsi alizozifanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hii inapatikana. Nilitumia muda mwingi sana kwenda kumwona ofisini kwake lakini na wasaidizi wake katika Wizara nyingine. Kwa kweli namshukuru Mwenyezi Mungu, lakini namshukuru yeye Makamu wa Rais na wasaidizi wote kwa maana ya Wizara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Waziri wa Ujenzi wakati huo Profesa Mbarawa kwa ushirikiano mkubwa alionipa kuhakikisha kwamba pesa kwenye barabara hii zinapatikana. Kwa kweli sina cha kuwalipa hawa wote wakiongozwa na Mheshimiwa Rais, ninachoweza kusema ni kwamba, malipo ya kile

walichotupatia Wanalulindi watakwenda kukiona mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema baada ya shukrani nitaomba, kama ilivyokuwa ada na ustaarabu wa sisi Watanzania, lakini na ustaarabu wa watu waungwana. Maombi yangu, kwanza yatajielekeza kwenye eneo la barabara, ukiangalia kwa hali ilivyokuwa sasa hivi kwenye jimbo langu ni changamoto kubwa. Nilipata bahati juzi nilivyokwenda kugawa kiasi cha pesa ambacho Mheshimiwa Jenista alinipatia cha maafa, nilibahatika kupita katika maeneo yaliyoathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla ni kama barabara zote kwenye jimbo lile zime-*collapse*, mawasiliano yamekuwa ni magumu sana. Jimbo lile lina kata takribani 18, lakini hakuna kata hata moja katika hizo ambayo imesalimika. Mawasiliano yamekatika kabisa kati ya kata na kata, hii inatokana na mvua kubwa iliyonyesha. Watu wote wanajua, wananchi wangu wanafahamu kwamba ni mvua ndiyo, hatuna jinsi ya kufanya ni jambo la Mwenyezi Mungu lakini cha kufanya ni nini? Ni kuendelea kuiomba Serikali itutazame kwa jicho la huruma kwa sababu hali imekuwa si nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa kuonyesha uharibifu huo ni nyumba zilizoharibika. Kwa mfano, Kijiji kimoja tu cha Chiungutwa ambacho nilikiombea pesa za maafa kutoka kwa Mheshimiwa Jenista, kulikuwa na nyumba takribani 248 zilizoangushwa na mvua. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi athari ilivyokuwa kubwa, kwa kijiji kimoja tu. Vijiji vingine kama Mijelejele, Mputeni, Sindano na maeneo mengine kuna athari kubwa. Kwa uchache, takribani nyumba zisizopungua kama 400 na kitu zimeathirika na mvua. Ni janga kubwa japo wanasema kwamba ni vigumu kuvumilia janga hilo. Hawavumi lakini wamo, kwamba na sisi tumepata majanga makubwa lakini hatusikiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala la barabara, napenda maombi yangu mengine niyaelekeze katika elimu. Jimboni kwangu kuna changamoto kubwa sana, ni jimbo

ambalo suala la elimu lilianza muda mrefu, kwa hiyo shule nyingi zilijengwa zamani sana. Miaka ya huko nyuma kabla ya mwaka 1920 hivi utakuta ziko shule za namna hiyo. Shule hizi zimechoka na ni nyingi sana, kwa orodha nikianza kuzitaja hapa itakuwa ni vigumu. Kwa bahati nzuri nimeshaandika mara nyingi sana kuiandikia Ofisi ya Mheshimiwa Mchengerwa kuhusiana na jambo hili la shule chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchache nina shule chakavu kwenye jimbo langu zisizopungua 32, ni chakavu kabisa. Ni chakavu kiasi cha walimu kuamua sasa kutokana na hatari iliyojitokeza, kutokana na ubovu huo, wanatumia mikorosho pamoja na miembe kama madarasa. Kwa kweli ni hali mbaya, ni vigumu hata kuizungumzia hapa kwa sababu ni jambo gumu na ni jambo la aibu, lakini kuna wakati sasa hakuna jinsi inabidi lazima tuzungumze kusudi ieleweke.

Wanasema; *"mficha uchi hazai."* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimeamua nizungumze hili kwenye *public* hapa angalau tupate jicho la huruma. Tuna changamoto kubwa sana katika eneo hili. Hali kadhalika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hiyo siyo lugha ya Kibunge, hebu toa maneno yako hayo.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufuta hiyo kauli.

**NAIBU SPIKA:** Endelea.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea, nizungumzie kuhusu suala la afya. Katika jimbo langu nina kata takribani 18, lakini tumekuwa na uhitaji mkubwa sana wa vituo vya afya. Nilishawahi kumwandikia Waziri kuhusiana na uhitaji huo akaniahidi Kituo cha Afya cha Namwanga, mpaka sasa hivi

sijajua *status* yake ikoje. Vilevile, Kituo cha Afya cha Mkululu, ningependa wakati wa ku-*wind-up* Mheshimiwa Waziri aje anipe ahueni angalau watu wa Lulindi na wenyewe wapone, waone kwamba ni kitu gani wanakitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kumekuwa na changamoto kubwa sana ya watumishi katika maeneo yote, kwa maana ya vituo vya afya na shule ambazo zipo kwa sasa. Nikitolea mfano tu, kwenye Kituo cha Afya cha Chikoropola kina watumishi hawazidi watatu, hicho ni kituo cha afya, unaweza ukaona jambo hili jinsi lilivyokuwa gumu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mchungahela, ahsante sana.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Namwita Mheshimiwa *Engineer* Ulenge na tunamalizia na Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi, muda na wakati kama huu. Awali ya yote naipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyoifanya katika Wizara hii ya TAMISEMI kuhakikisha inapeleka huduma kwenye jamii na kuchochea maendeleo kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawapongeza sana watendaji pamoja na Mawaziri wa Wizara hii kubwa na pana kabisa kwa nchi yetu. Kipekee bila kusema uongo kwa kweli msifieni mtu anapokuwa hai kabla hajafa. Mheshimiwa Mchengerwa mahali popote ambapo amepewa nafasi kwa hakika ameitendea haki nafasi hii, amewajali walengwa wa nchi hii, kiukweli anastahili pongezi. Kwa kuongezewa hapo Wakili Msomi mwenzake

Mheshimiwa Zainab Katimba na Dkt. Festo, hapo nina hakika mambo yanakwenda kuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuchangia. Nimeipitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Kwa kuzingatia vipaumbele vya mpango wa bajeti wa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na jukumu la TAMISEMI la kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi shindani kwa maendeleo ya watu. Sambamba na lile jukumu la kuratibu mikopo ya 10%. Mchango wangu leo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naishukuru Serikali kwa kurudisha utaratibu wa mikopo kwa vikundi vya 10%. Kwa kipekee kabisa kwa niaba ya wanawake wa Halmashauri ya Bumbuli, tunashukuru sana kuiingiza Halmashauri ya Bumbuli katika halmashauri zile kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hii itatolewa na benki, nasema ni shukrani kwa sababu itakwenda kupunguza ile mianya iliyosababisha walengwa wengi zaidi wasifikiwe. Suala la mikopo hii kutolewa na benki ni jambo moja, tunaamini muda wote ambao Serikali imekaa na fedha hizi zilizowekwa kwa utaratibu wa kisheria, lazima kutakuwa na mkakati mwingine mahsusi kabisa wa kuhakikisha fedha hizi zinakwenda kuleta tija na thamani halisi kwa wananchi walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri nimefika kabisa Halmashauri ya Bumbuli na nilikaa chini pamoja na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Bumbuli. Unaambiwa mwaka fulani Halmashauri ya Bumbuli ilikuwa ina makusanyo kidogo lakini fedha zile zilikuwa zinabaki. Hapa nataka kuzungumza nini? Ni kwamba bila kutengeneza utaratibu mzuri wa kuwepo Maafisa Maendeleo ya Jamii wazuri wanaojua majukumu yao, licha ya kuirudisha Halmashauri ya Bumbuli katika utaratibu wa kupata fedha zile, lakini walengwa wanaweza wasifikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii Kata ni wachache mno katika Halmashauri ya Bumbuli. Nimekwenda nikazungumza ana kwa ana pamoja na mkurugenzi yule aliyeondoka. Tunaomba kwa heshima, unyenyekevu mkubwa na usikivu mkubwa wa Serikali hii ya Mama Samia Suluhu Hassan, wakati wanaturudishia huo uwezo wa kukopa Julai, 2024, Maafisa Maendeleo Jamii Kata wawe wameongezwa katika Halmashauri ya Bumbuli ili wanawake wale walionipa dhamana mimi waweze kunufaika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nipo *very* makini na niko *very serious* na jukumu walilonipa. Nahakikisha na natamani wanawake wale wa Halmashauri ya Bumbuli wakue kiuchumi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake hili nalo liwe kipaumbele. Hizo halmashauri zote ambazo zinarudishiwa hizi fedha tuhakikishe kwamba tumeweka taratibu nzuri mahsusi kuhakikisha walengwa wanafikiwa ili ule uchumi shindani kule chini uweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine kwa mujibu wa Kanuni ile ya Fedha, Sura 290, zinamtaka Afisa Masuuli ambaye ni Mkurugenzi kuanzisha mafunzo kabla ya kuwapa fedha wale wanawake, lakini jambo hili limekuwa halifanyiki ipasavyo. Kumpa fedha bila kumpa mafunzo ni sawasawa na kumpa samaki badala ya kumpa ndoano. Wanawake wa Tanga tunahitaji ndoano na wala hatuhitaji samaki. Tuna uwezo wa kufanya kazi na kuweza kuzalisha zaidi. Naomba sana wanapotuletea fedha hizi utaratibu mzuri ufanyike kuhakikisha tunapata mafunzo. Mafunzo ya kuhakikisha namna gani tunakwenda kuanzisha vikundi na biashara na miradi itakayoleta tija kwa wanawake wale wa Bumbuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niwakumbushe, kanuni pia inamtaka Mtendaji Kata aandike barua ya utambulisho ili mwanamke yule aweze kutambuliwa katika halmashauri husika ili kuweza kupata mikopo. Kumekuwa na changamoto, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakaposimama hili alisemee na alikomeshe. Maafisa Watendaji Kata wana tabia ya kuwadai hela wanawake wanapokwenda kuomba zile barua za

utambulisho. Naomba sana Mheshimiwa Waziri alitolee tamko jambo hili likome *accordingly* ili wanawake hawa wasisumbuliwe na waweze kunufaika na fedha za Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alishahimiza kutengeneza majukwaa ya kiuchumi kwenye kila mkoa, wilaya na kata. Hizi fedha ndiyo maana yake, zitakwenda kusaidia ile dhamira kuu ya Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuinua wanawake kiuchumi. Sasa kama watendaji wanafelisha dhamira hii nzuri ya Mama, Mheshimiwa Mchengerwa naamini anaweza aka-*deal* nao *accordingly* ili dhamira ya Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile kusema kwamba, kumekuwa na utaratibu wa watu ndani ya halmashauri husika kutengeneza ndugu zao zaidi na ndio wanaokuwa wananufaika na mikopo ile. Naomba na hili Waziri alitolee kauli kwamba mikopo ile siyo kwa wale watu ambao wana ajira rasmi, ni kwa wanawake wengine waliopo mitaani wasiokuwa na ajira rasmi, hao ndio walengwa. Tafadhali Mheshimiwa Waziri, tunaomba atoe tamko hili ili mikopo ile iende ikawanufaishe walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kuchangia suala zima la Hospitali ya Magunga. Nimetembelea Hospitali ya Magunga, Hospitali ya Magunga imeanzishwa mwaka 1952. Kaka yangu Waziri Mchengerwa katika kufanya kazi kwake amejibainisha vizuri kwamba yeye ni *Pan-Africanist* na yeye amekuwa akidumisha fikra za viongozi na waasisi wa Taifa letu. Basi katika kuhakikisha hilo vilevile usizisahau hospitali hizi kongwe zilizoanzishwa na waasisi wa Taifa letu ikiwepo Hospitali ya Magunga pale Wilayani Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Magunga ina hali ngumu, ni chakavu mno. Imetengewa hela katika miaka miwili mfululizo nakumbuka, mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023//2024

ilitengewa shilingi milioni 900, lakini fedha hii hamkuipeleka. Nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri hapo mbele, waache basi kutudanganya. Wananchi wa Korogwe tumechoka kudanganywa, tunahitaji fedha wanazozitenga kwa ajili ya Hospitali ya Magunga, wazitoe tafadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali imekuwa chakavu, paa lake ni fupi, ni ya kizamani, inaharibu taswira nzuri ya kazi nzuri ya Mheshimiwa Mama, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoifanya katika hospitali. Mheshimiwa Mama Samia amefanya kazi kubwa na nzuri ya kujaza hospitali nzuri kabisa na kuboresha huduma ya jamii, lakini hospitali hizi kongwe zisipofanyiwa marekebisho makubwa zinapunguza ubora wa kazi nzuri ya Mheshimiwa Mama, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuendelee kuheshimisha kazi nzuri zilizofanywa na Mheshimiwa Mama, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha hospitali hizi kongwe zinafanyiwa marekebisho makubwa yanayotakikana. Moja ya changamoto kubwa katika hospitali hii ni kukosekana kwa *complex maternity ward*. Utakuta *maternity ward* ile ipo mbali na…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante *Engineer* Ulenge, kengele ya pili. Karibu Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia wa mwisho katika michango ya leo…

**NAIBU SPIKA:** Umekuwa wa mwisho kwa sababu umepangwa mwisho.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawa na nimefurahi sana. Kabla ya yote, napenda kumshukuru Waziri Mchengerwa pamoja na timu yake na namshukuru

Mheshimiwa Mchengerwa kwa uungwana alioonesha. Kipindi fulani alituandikia barua ya kutushukuru kutokana na michango yetu, tunamshukuru kwa kutambua michango hii. Ni kitendo cha uungwana ambacho sijakiona muda wote ambao nimekaa ndani ya Bunge, nawashukuru pamoja na timu yake. Namkaribisha Mheshimiwa Zainab. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoka kwenye Kamati ya *LAAC*. Unajua mnapokwenda kwenye shule unapokuwa mwalimu wa nidhamu mara nyingi unaitwa mnoko. Kwa hiyo, kwenye Kamati yetu hakuna unoko lakini tunasema karibuni. Mheshimiwa Waziri tangu apate Uwaziri hajaja kututembelea huko kwenye Kamati yetu, aje, karibu sana kumenoga kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI imetoa pesa nyingi kipindi hiki katika bajeti, shilingi trilioni tatu na zaidi kwa ajili ya maendeleo. Shida si kwamba pesa hizi ni nyingi au ndogo, kinacho-*matter* hapa ni kwamba, je, zinasimamiwaje? Nakuwa na wasiwasi juu ya usimamizi wa pesa hizi kutokana na hali ilivyo ndani ya halmashauri, kutokana na jinsi wakurugenzi wanavyoweza kusimamia pesa hii. Naomba tutazame na uwezo wa wakurugenzi. Hawa wakurugenzi kuna ambao wanafanya kazi vizuri na kuna ambao hawana uwezo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona wakurugenzi hawa, kama Maafisa Masuuli tuwachukue kama ma-*CEO* wa kampuni. Tuchukue halmashauri kama kampuni kwamba umemtoa *CEO* umempeleka pale, lazima utampa malengo ili aweze kutekeleza malengo yale, aweze kuinua ile kampuni yake, ni sawa na halmashauri hizi. Lazima mkurugenzi, kama hatuwezi kuingilia mfumo wao wa kuteuliwa basi kuwepo na mfumo thabiti wa kuwasimamia. Mfumo huo ni pamoja na kuhakikisha tunapata *professionals* hasa wakurugenzi pamoja na maafisa mipango. Wale ambao wanaweza kusimamia na kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo zinapelekwa kule, zinasimamiwa ipasavyo na zinaleta matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili, napenda kuongelea kuhusu miradi inayotekelezwa katika halmashauri, lakini inahitaji utekelezaji wa mamlaka nyingine. Kwa mfano, unakwenda kujenga shule, lakini lazima kuwepo na barabara, maji na umeme. Sasa anakwenda kujenga shule mahali ambapo hata Mradi wa *REA* haupo. Sisi kama Kamati ya *LAAC* tunakutana na mambo kama haya. Miradi inajengwa, ni mizuri, lakini ninyi ambao ni *planners* mnashirikianaje sasa na mamlaka nyingine ambazo zinapaswa kuhusika katika kuhakikisha kwamba ule mradi unatekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye halmashauri nyingine mtu anakwambia mimi natumia shilingi milioni 10 kusomba maji. Je, idara ya maji ilihusishwaje wakati wa kuandaa mradi ule? Hakuna barabara na katika bajeti mkurugenzi anakuwa hajapewa hela ya kutengeza barabara, kwa hiyo anatenga pesa ambayo wamempa kujenga shule au kujenga hospitali anatoa sehemu anaenda kutengeneza barabara. Je, yule wa barabara alihusika vipi katika mipango yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa ardhi, wakati mwingine wajue kwamba vijiji vingi Tanzania wameuza ardhi. Halmashauri zimepima viwanja na kuuza, hakuna maeneo ya kujenga hospitali, hakuna maeneo ya kujenga shule. Kwa hiyo, jambo kama hili linafanya bajeti ya TAMISEMI, kwa mfano unampa mtu shilingi 1,300,000,000 ajenge hospitali, lakini hukumwekea hela ya barabara, umeme wala maji, anafanyaje ili kuhakikisha huu mradi unatekelezeka? Kwa hiyo tunaomba *planners* wahakikishe sasa inafika mahali wanapofanya mipango, wahakikishe kwamba mamlaka nyingine zote ambazo zinahusika katika kuhakikisha mradi huu unatekelezeka na unaleta tija, basi na wenyewe wahusike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kuhusu pesa nyingi ambazo halmashauri zinalipa kwa *MSD* ili waweze kununua vifaa pale wanapojenga hospitali. Halmashauri zinaweka pesa zinakaa muda mrefu *MSD,* lakini sisi tuliweza kuwaita *MSD* na kuwauliza kwa

nini wanaweka hizi pesa? Lawama ipo pande mbili, unajenga hospitali mpaka inaisha, wewe hujaagiza vifaa *MSD*, wewe unachotegemea ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba TAMISEMI wawaeleze wakurugenzi hawa wanapojenga hospitali hasa zinazohitaji vifaa, waagize vifaa mapema mwaka mmoja kabla hospitali haijaisha ili waweze kuhakikisha vifaa vinapatikana na hospitali zinafunguliwa. Tumekuta hospitali nyingi hazikufunguliwa, majengo yapo pale *idle* kwa sababu wameomba vifaa, wamechelewa na *MSD* inachukua karibu miezi sita kuleta vifaa. Kwa hiyo hospitali zinakaa na wananchi hawafaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukosefu wa *engineers*, kwa muda mrefu tumekuwa tukisema kwamba hii miradi inayotekelezwa ambayo wanapeleka fedha nyingi inatekelezwa chini ya viwango kwa sababu haina wasimamizi wazuri. Tumekuta kwenye halmashauri nyingine wamejiongeza, wameweza ku-*hire*, yaani wanaingia mkataba na *engineers* wale waliomaliza shule, wanaingia nao mikataba ya miezi sita mpaka mwaka mmoja na wamesimamia kazi vizuri sana. Tumekwenda kule Wilaya ya Misenyi tumekuta hospitali imejengwa na kijana mdogo kabisa *engineer* ambaye yupo pale kwa mkataba. Tumeenda Tarime tumekuta wamejenga shule vizuri kabisa na anayesimamia ni *engineer* ambaye ameingia kwenye mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wa-*encourage* halmashauri yaani wale wakurugenzi na wao wajiongeze. Hatuna *engineer*, hatuna *engineer,* huna *engineer* si unaweza kutumia mapato ya halmashauri uka-*hire engineer* pale kwa muda, akasimamia kazi ikaenda vizuri? Yenyewe hiyo inataka nini? Inataka mtu uwe umesoma mpaka kiasi gani? Hapana, kwa hiyo ni namna ya kujiongeza kuhakikisha kwamba kazi yako wewe kama *CEO* wa kampuni inaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo, maneno yangu yasiwe mengi sana. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge huyu ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo. Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.27 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 18 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*